

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 28 Aprili, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa, tukae. Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

Na.110

Vigezo vya Kurasimisha Vibali vya Ajira na Kuishi Nchini

MHE. STANSLAUS S. MABULA (K.n.y. MHE. ESTER M. MMASI) aliuliza:-

Pamoja na juhudini za Serikali katika kulinda ajira za vijana wa Kitanzania, Serikali kupitia Sheria ya Ajira ya Wageni Na. 1 ya mwaka 2015 ilirasimisha vibali vya kuishi na ajira kwa wageni batili wapatao 317 kati ya 779.

Je, ni vigezo gani viliviyotumika katika urasimishaji wa vibali hivyo wakati vijana wengi wa Kitanzania hususan

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wahitimu wa vyuo vikuu wanahangaika katika kupata ajira ili wafurahie faida ya taaluma zao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ester Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Kuratibu Ajira kwa Wageni Nchini Na.1 ya mwaka 2015 ilianza kutumika tangu tarehe 15/9/2015. Sheria hii imeweka utaratibu maalum kwa mtu anayetaka kumuajiri raia wa kigeni kuomba kibali cha ajira kwa Kamishna wa Kazi ambaye ndiye mwenye mamlaka pekee ya utoaji wa vibali vya ajira kwa wageni nchini. Kamishna wa Kazi alianza kazi ya kutoa vibali kwa wageni kuanzia tarehe 1/10/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vinavyotumika kurasimisha vibali kwa wageni vimeainishwa katika kifungu cha 6(1) katika Sheria ya Kuratibu Ajira ya Wageni Na.1 ya mwaka 2015 ambapo masharti mbalimbali yameainishwa kwa mwombaji kukidhi kabla ya Kamishna wa Kazi hajatoa vibali. Mojawapo ya sharti ni kumtaka mwajiri atoe ushahidi wa kuridhisha kwamba ametafuta mtaalam huyo kwenye soko la ajira la ndani na hakupata mtu mwenye sifa husika na vilevile azingatie suala la mpango wa urithishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa itaendelea kusimamia Sheria hii Na.1 ya mwaka 2015 ili kulinda nafasi za ajira za Watanzania wenye fani na taaluma mbalimbali. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swalii la nyongeza.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa hawa waajiriwa 779 walikuwa tayari wapo nchini wanafanya kazi kinyume na utaratibu jambo ambalo ni batili, ni hatua gani ambazo Serikali ilikwishachukua dhidi yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la pili, je, anafahamu kwamba utoaji wa vibali unaoendelea, unaendelea kunyima fursa vijana wengi wa Kitanzania kama alivyokiri kwamba wanazo sifa na wamemaliza vyuo vikuu, lakini wanakosa fursa za kuajiriwa kwa wakati kutokana na waajiriwa wengi kutoka nje kupata nafasi? Nakushukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Antony Mavunde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, swal la kwanza anahoji juu ya watu hawa takribani 770 ambaao waliomba vibali vyaa kazi na kwamba uwepo wao ulikuwa ni batili.

Kwa mujibu wa taratibu na sheria yetu inavyosema, watu hawa wakiomba vibali maana yake ni kwamba anaanza katika Ofisi ya Kazi na baadaye anakwenda kupewa kibali cha ukaazi. Kama alikataliwa katika Ofisi ya Kazi kimsingi hapo yeye hastahili kuwepo nchini kwa sababu hiyo pia inamfanya asipate kibali cha ukaazi. Ndiyo maana tumekuwa tukifanya ziara mbalimbali na kaguzi za kuhakikisha kwamba tunawabaini watu wote wale ambaao wanaishi nchini kinyume cha sheria na ambaao wanafanya kazi kinyume cha utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu utoaji wa vibali, kwa mujibu wa sheria yetu pia inamuelekeza Kamishna lazima ajiridhishe kibali anachokitoa ujuzi huo haupatikani nchini au mwajiri athibitishe kwa Kamishna kwamba alitafutwa mtu mwenye fani hiyo hakupatikana. Kwa hiyo, kwa suala la vibali, Kamishna anatoa vibali kulingana na

sheria inavyomwelekeza na ni kweli kwamba Kamishna anafanya kazi hii kuhakikisha kwamba vijana wengi wa Kitanzania ambao wamesoma vizuri wao ndio wanufaika na nafasi za kazi za ndani. Ukiangalia katika mtiririko tumejitahidi sana kuzuia wageni katika kazi za kawaida ili vijana wetu wa Kitanzania wapate nafasi za kufanya kazi katika nchi yao.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa utaratibu wa Serikali wa kuajiri unaeleweka kwa kufuata taratibu mbalimbali na wapo vijana ambao wana sifa hizo, elimu, uzoefu na vitu vingine. Ni lini Serikali itawapa ajira vijana wa Kitanzania ili kuwaepusha kujilingiza kwenye masuala ya ukabaji, wizi na mambo mengine?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutoa nafasi za ajira kwa vijana kwa nafasi ambazo zimekuwa zikitangazwa. Pia kuititia Wizara ya Kazi tumeendelea kutoa msisitizo wa kuanza kuwabadilisha mtazamo vijana na kuwaaminisha kwamba si lazima vijana wote waende kufanya kazi za maofisini hii inatokana pia na takwimu iliyofanyika mwaka 2014 (*Intergrated Labour Force Survey*) iliyotuambia kwamba kundi kubwa la vijana wanaoingia katika soko la ajira kila mwaka ni kubwa zaidi kuliko nafasi za ajira ambazo zinazalishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali tumekuja na mipango kadhaa kuhakikisha kwamba tunamfanya kijana huyu wa Kitanzania asiendelee kufikiria kuhusu kuajiriwa tu ofisini mojawapo ikiwa ni kumsaidia kupata ujuzi ili wawewe

kujajiri na kuajiri vijana wengine. Pia kuwafanya vijana wa nchi hii sasa washiriki kwenye kilimo, ufugaji na biashara ikiwa pia ni sehemu ya ajira.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Venance Methusalah Mwamoto, Mbunge wa Kilolo, sasa aulize swali lake.

Na. 111

Ujenzi wa Mabwawa Kilolo

MHE. VENANCE M. MWAMOTO aliuliza:-

Vyanzo vingi vya maji vinavyojaza Bwawa la Kihansi vinatoka Wilaya ya Kilolo.

Je, Wilaya hii inanufaika vipi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Venance Methusalah Mwamoto, Mbunge wa Jimbo la Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli vyanzo vingi vya maji vinavyojaza Bwawa la Kihansi vinatoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa Bwawa la Kihansi unategemea sana vyanzo hivyo muhimu ambapo Taifa linanufaika kutokana na shughuli kubwa inayofanyika katika bwawa hilo ya kufua umeme. Uhifadhi wa Bwawa la Kihansi unatokana na vijiji 22; kutoka Wilaya za Mufindi vijiji nane, Wilaya ya Kilolo vijiji nane na Kilombero vijiji nane ambapo kwa sasa kuna mradi maalum unaosimamiwa na Baraza la Mazingira la Taifa kwa ajili ya uhifadhi mzima wa Bonde la Mto Kihansi.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo inanufaika na bwawa hilo kwa kupata umeme ambao umesambazwa na Wakala wa Umeme Vijijini (*REA*) katika maeneo mengi ya vijijini ambapo katika Wilaya ya Kilolo vijiji vilivyonufaika ni pamoja na Masisiwe, Boma la Ng'ombe, Mwatasi, Ng'ingula na Wangama. Pia uwepo wa Bwawa la Kihansi umesababisha mashirika mbalimbali kuanzishwa kwa lengo la kusaidia jamii katika mambo mbalimbali kama vile upandaji wa miti kwa lengo la kuhifadhi mazingira, ufugaji wa nguruwe, mbuzi pamoja na ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wananchi wa Halmashauri ya Kilolo wameendelea kupata huduma ya maji kuitia miradi mbalimbali iliyotekelizwa chini ya mpango wa miradi ya vijiji kumi, ambapo jumla ya miradi saba ya Irindi, Ihimbo, Mwatasi, Kipaduka, Vitono, Ikuka na Ilamba imekamilika na miradi mingine ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Venance Mwamoto, swali la nyongeza.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini swali langu hasa lilikuwa linahusu upande wa umeme. Naomba niulize maswali mawili madogo, kwa kuwa Waziri wa Nishati yuko hapa kama ataona anaweza kumsaidia basi anaweza akajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, ambalonialekeza Wizara ya Maji; kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba Kilolo kuna vyanzo vingi vya maji, lakini sasa hivi wakulima walio wengi walikuwa wanategemea sana vilimo vya mabondeni, kwa lugha ya kwetu tunaita *vinyungu* ambavyo ndiyo vimewapelekea kuwasomesha watoto zao na kuendesha maisha ya kila siku lakini sasa hivi wamezuiwa. Kwa kuwa Serikali ilipokuwa inazuia ukataji wa miti ilihamasisha watu watumie umeme na kupunguza bei ya gesi sasa Serikali imezuia watu wasilime

kwenye vyanzo vya maji, Wizara imejipangaje ili kuhakikisha wale wananchi wanaendelea kupata fedha kwa kutumia kilimo cha *vinyungu*?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili nilitegemea ningejibowi na watu wa umeme, kwamba kwa kuwa vyanzo vingi vimekwenda Kihansi na Kihansi ndiyo inatoa maji wananchi wa Kilolo wananaufaika vipi kwa sababu wametumia muda mwangi kutunza vyanzo vile? Naomba maswali yangu yajibiwe.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini majibu.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, ufanuzi wa kwanza ni hivi, sio wananchi wa Kilolo peke yake ni suala la dunia nzima, unahitaji maji kuzalisha umeme, lakini unahitaji maji kwa ajili ya umwagiliaji. Huu ni mjadala ambao dunia nzima wataalam wa maji na wa umeme wanaendelea kujadiliana. Kwa hiyo, siyo kitu cha ajabu kwa kwetu hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la umwagiliaji tulivyoenda huko vijijini kusema ukweli zile mbinu wanazotumia ni za kizamani, mtu anakuja anajenga yale mataruma kwa zege, wakati wa mvua anamwagilia, wakati wa kiangazi anamwagilia. Kwa hiyo, nadhani Serikali imefanya utafiti hasa watu wa Kilimo kwamba kuna njia bora za umwagiliaji. Cha kwanza ni kutumia njia bora za umwagiliaji, lakini wote wawili wanahitaji maji, wakulima na watu wa kuzalisha umeme, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la wanafaidikaje, tuna mradi mmoja katika miradi ya REA III ambayo tutakuja kuieleza kwenye bajeti yetu kuna mradi wa kuwapatia watu umeme walio kwenye mkuza mkubwa wa kusafirisha umeme kutoka Iringa - Dodoma mpaka Shinyanga kama ambavyo tulivyofanya kuwapatia watu umeme walio kwenye mkuza wa bomba kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam, huo mradi tayari unatekelezwa.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo, ndugu yangu Mheshimiwa Mwamoto afahamu kwamba ndani ya REA //huo ni mradi mmojawapo, wanaotutunzia vyanzo vya maji watapata umeme ule wa jogoo wawili shilingi 27,000, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa George Lubeleje, swalii la nyongeza.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swalii moja la nyongeza. Kwanza naishukuru sana Serikali kwa kuchimba visima vya maji katika kijiji cha Bumila, Iyoma na Mima. Hata hivyo, sasa ni miezi nane tangu visima vimechimbwa, hakuna pampu zilizowekwa, hakuna mabomba ya kusambaza maji wala matenki. Je, Serikali inasemaje kwa wananchi wa vijiji hivi ambao wana shida kubwa sana ya maji?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, tumetenga fedha katika bajeti ya mwaka 2017/2018 na bajeti hiyo bado inaendelea. Kwa kutumia nafasi hii nimuagize Mkurugenzi wa Mheshimiwa Lubeleje, suala la pampu ni rahisi sana, maeneo yote ambayo visima vimeshachimbwa tunahitaji *quotation* ambayo tunaiweka kama ni *certificate*, ukileta tunatoa hela ili uweze kununua pampu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kama inahitajika miundombinu ya ujenzi wa tenki na mabomba ya kusambaza maji na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji, Mheshimiwa Lubeleje Mkurugenzi wako afanye usanifu wa haraka, atangaze *tender*. Kama ana upungufu wa wataalam Wizara ya Maji tuko tayari, atuandikie barua ili tuweze kumpa *support* ya kumpelekea wataalam ili kazi hiyo ifanyike haraka wananchi wa Jimbo lako Mheshimiwa Lubeleje waweze kupata maji kwa haraka.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa sasa aulize swalii lake.

Na. 112

Kupeleka Umeme – Kata za Wilaya ya Chunya

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye Kata za Ifumbo, Lualaje, Mafyeko na Kambikatoto katika Wilaya ya Chunya?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijiji Awamu ya Tatu umeanza rasmi nchi nzima tangu mwezi Machi, 2017. Mradi huu utajumuisha vipengele-mradi vitatu vya *densification, grid extension* pamoja na *off grid renewable* ambapo inalenga kuongeza wingi wa usambazaji umeme kwenye vijiji ambavyo vimefikiwa na umeme lakini kwenye vitongoji havijaunganishwa. Kata za Ifumbo, Kambikatoto, Lualaje na Mafyeko zimejumuishwa katika mradi wa *REA* Awamu ya Tatu wa *grid extension* ambao utaanza na kukamilika mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kupeleka umeme katika kata hizo itajumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometra 20, ujenzi wa njia ya umeme ya msongo ya kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometra 76, ufungaji wa transforma kumi pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 1,145. Gharama ya kazi hii ni shilingi bilioni 3.142.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Victor Mwambalaswa swalii nyongeza.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo nimeridhika nayo, bado nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa *REA* Awamu ya Kwanza, jimbo langu lilibahatika kupata umeme kwenye vijiji tano au sita na kwa kuwa mradi huu wa Awamu ya Kwanza haukuwa na kipengele cha kuweka umeme kwenye majengo ya huduma za jamii kama shule na vituo vya afya. Baada ya kuona hivyo ilibidi Mbunge nije hapa Bungeni nikope fedha kama shilingi milioni 150 ili nikalipe *TANESCO* waweke umeme kwenye sekondari saba; na kwa kuwa *REA* Awamu ya Pili nimepata vijiji vitano, lakini katika Kata ya Mtanila umeme haujaend kwenye Kituo cha Afya cha Mtanila. Swali langu sasa, je, hii *REA* Awamu ya Pili Mheshimiwa Naibu Waziri ananihakikishia majengo ya huduma za jamii kama vituo vya afya na shule yatapata umeme? La kwanza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa amesema *REA* Awamu ya Tatu karibu itaanza; je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kwenda na mimi Chunya wakati wa ufunguzi wa mradi huo hasa hasa kuanzia Kata ya Ifumbo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Mwambalaswa kwa kufuatilia mahitaji na maslahi ya wananchi wake katika Jimbo la Lupa na tunashirikiana naye kwa ukaribu sana hasa katika vijiji na kata ambazo zimebaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nikubali kwamba katika *REA* Awamu ya Kwanza na ya Pili hatukuchukua maeneo mengi sana na hii ni kwa nchi nzima, siyo katika jimbo la Mheshimiwa. Nimhakikishie Mheshimiwa

Mwambalaswa katika kata sita zilizobaki ambazo ameomba zipatiwe umeme ikiwemo Kata za Mtabila, Ifumbo, Itumbi, Kambikatoto pamoja na Matundasi A na B zote zitapelekewa umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama alivyouliza, *REA Awamu ya Tatu* majukumu yake ya kimsingi pamoja na mambo mengine ni kusambaza umeme katika taasisi zote za umma kama hospitali, vituo vyatya, zahanati, shule, mitambo ya maji, makanisa, misikiti na sokoni.

Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mwambalaswa na nichukue nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote kwenye Halmashauri zetu tuweze sasa kutenga walau pesa kwa ajili ya kuunganisha umeme kwenye taasisi zetu kwa sababu hili ni jukumu letu sote, na ndiyo maana wakandarasi tunapokwenda kuwakabidhi sasa tunawakabidhi Waheshimiwa Wabunge ili waweze kufuatilia utekelezaji wa miradi hii. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwambalaswa nakuhakikishia kwamba vituo vyatya na taasisi nyingine zitapelekwa umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili la kufuatana na Mheshimiwa Mwambalaswa, kwanza kabisa niko tayari lakini kabla sijafuatana nawe mkandarasi tumeshamtuma na tumeshazindua utekelezaji wa *REA Awamu ya Tatu* katika Mkoa wa Mbeya na Songwe. Sasa hivi mkandarasi yuko lleje na tarehe 15 atafika kwako Mheshimiwa Mwambalaswa. Kwa hiyo, tuko pamoja na niko tayari kufuatana na wewe.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa Mbulu Vijiji katika *REA Awamu ya Pili* tumepata viji viwili tu na sasa Mbulu Vijiji hatuna *sub-station* tunapata umeme kutoka Katesh na Mheshimiwa Waziri anafahamu, amekuja, tunapata kutoka Babati na

Mbulu Mjini. Je, mtatuhakikishajie sasa katika awamu hii *REA* itafika maeneo yote ya kata na hasa katika vijiji vyta mwanzo vya Mbulu Vijiini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa Mheshimiwa Flatei nakupongeza, mwaka jana mwezi Novemba tulitembea na wewe kwenye jimbo lako lote na ukaniionesha vijiji vyako vyote 78 ambavyo havijapata umeme pamoja na vijiji vyta karibu kabisa na Wilaya za jirani. Hata hivyo, natambua katika utekelezaji wa *REA* Awamu ya Tatu kazi zinazofanyika ni pamoja na kufunga transfoma. Kinachokosekana katika Jimbo lako Mheshimiwa Flatei ni ufungaji wa transfoma katika vijiji ambavyo umevitaja ikiwa ni pamoja na Katesh.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Flatei kazi ambayo itafanyika sasa ni kukupelekea umeme katika vijiji vyako 78 vilivyobaki pamoja na vitongoji 120 kama ambavyo umeomba. Kwa hiyo, niwahakikishie wananchi wa Mbulu Vijiini kwamba wote watafikiwa na umeme vijiji, vitongojini pamoja na kwenye taasisi zako za umma. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuiliza swali la nyongeza kwenye Wizara ya Nishati na Madini. Wilaya ya Chemba ni mionganini mwa Wilaya mpya na upatikanaji wa huduma ya nishati kwa maana ya umeme ni kwa vijiji 60 tu katika vijiji 112. Nataka kufahamu ni lini sasa kwa *REA* Awamu ya Tatu itakwenda kukamilisha vijiji hivi 52 vilivyobaki ili Wilaya yetu na wananchi wale wawezesha kupata huduma hii ya umeme wa *REA* Awamu ya Tatu? Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa katika Jimbo la Chemba tulipeleka umeme katika vijiji 62 na vikabaki vijiji 52; kwa hiyo viko 124. Niseme tu vijiji 52 vilivyobaki tumeshazindua katika maeneo ya Chemba na Wilaya zote, Mkoa wa Dodoma na tunaelekeea katika Mikoa ya Singida na mingine. Upelekaji wa umeme katika REA Awamu ya Tatu umeanza tangu mwezi Machi na utakamilika kwa nchi nzima ikiwemo pamoja na Jimbo la Chemba mwaka 2020. Mradi huu unakwenda kwa awamu, baadhi ya vijiji na vitongoji vitakamilika mwezi Machi, 2019 na baadhi yake kwenye *densification* ni miezi 15 kuanzia sasa. Kwa hiyo, vijiji vyote 52 kati yake vijiji 12 vitapatiwa umeme 2019 na vilivyobaki nya Chemba mwaka 2020. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na.113

Utafutaji wa Uchimbaji Madini – Kigoma

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Mkoa wa Kigoma una madini ya chokaa, dhahabu, *platinum* na kadhalika:-

Je, Serikali imechukua hatua gani kuendeleza utafutaji na uchimbaji wa madini katika mkoa huo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Mkoa wa Kigoma una madini ya aina mbalimbali yakiwemo madini ya chokaa, chuma, *cobalt*, dhahabu, galena, *nickel*, shaba na *platinum*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuitia Wakala wa Jiolojia Tanzania (*GST*) ilifanya utafiti wa awali wa madini nchi nzima na kuandaa ramani za jiolojia nchini. Utafiti huo utasaidia kutangaza fursa za uwepo wa madini yanayogunduliwa ili wawekezaji wa ndani na nje ya nchi waweze kuwekeza katika tafiti za kina na uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1959 hadi 2010 Wakala wa Jiolojia Tanzania (*GST*) walifanya utafiti wa jiolojia katika Mkoa wa Kigoma na kutengeneza ramani za jiolojia 22 kwa nchi nzima na hasa katika Mkoa wa Kigoma. Kati ya mwaka 2013 hadi 2014, *GST* kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ikiwemo kampuni ya *Beak Consultants GmbH* ya Ujerumani na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walifanya utafiti wa awali kubainisha uwepo wa madini mbalimbali Mkoani Kigoma kama ifuatavyo:-

Madini ya *tin* katika maeneo ya Bwuhinika, Kabogo, Kapalagulu na Lugufu; madini ya shaba katika maeneo ya Gagwe, Kampisa na Nyamori; madini ya *barite* katika eneo la Ilagala; chumvi katika eneo la Uvinza; dhahabu katika maeneo ya Isabika, Lumbwa, Lusahunga pamoja na Mwiruzi; madini ya *agate* katika maeno ya Kabingo, Kasulu, Keza na Nkuba; madini ya *nickel*/katika eneo la Kapalagulu na madini ya chokaa katika maeneo ya Lugufu, Makere, Matiaso pamoja na Kasuku. Utafiti wa kina unahitajika ili kubaini kiasi halisi cha mashapo yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2017, Mkoa wa Kigoma ulikuwa na jumla ya leseni 15 za utafutaji wa madini ya dhahabu, leseni 20 za utafutaji wa madini ya shaba na leseni 2 za utafutaji madini ya *platinum*. Vilevile kuna leseni 25 za uchimbaji mdogo wa madini ya

dhababu na leseni 118 za uchimbaji mdogo wa madini ya chokaa, kadhalika kuna leseni 716 za uchimbaji mdogo wa madini ya shaba katika maeneo mbalimbali Mkoani Kigoma.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swalii la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Swalii la kwanza, katika Wilaya ya Kasulu katika kijiji cha Makere lakini pia katika Wilaya ya Kakonko wananchi wamekuwa wakipata kipato chao kwa kuchimba chokaa, lakini mara nydingi wamekuwa wakizuiliwa kufanya shughuli hiyo. Je, Wizara ya Madini na Wizara ya Maliasili iko tayari kukaa pamoja na wananchi hao ili kuweza kutatua tatizo hilo na kuwawezesha kuwa wachimbaji rasmi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii langu la pili, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inatenga eneo la wachimbaji wadogo ili kuepusha migogoro inayoweza kutokea baadaye? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Genzabuke wakati tunatenga eneo la Kakonko mwaka 2002 alitupa ushirikiano mkubwa sana. Kwa hiyo, nakupongeza sana Mheshimiwa Genzabuke kwa kufuatilia maisha ya watu wa Kigoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusiana na maswali yake mawili, la kwanza alitaka kujua namna sisi pamoja na taasisi ya maliasili tunavyoshirikiana ili kuwawezesha wananchi hawa kupata maeneo na kufanya uchimbaji kwa ajili ya kuongeza pato lao.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge, Sheria ya Madini ya mwaka 2010 katika kifungu cha 95 pamoja na Sheria ya Mazingira zinakubaliana kwamba mtu yejote anaweza akamilikishwa leseni katika eneo lolote ikiwa ni pamoja na maeneo ya *reserve* na hifadhi kinachotakiwa ni kupata kibali cha maandishi. Tumekuwa tukifanya hivyo Mheshimiwa Genzabuke ndiyo maana katika eneo la Makere kuna leseni 15 za uchimbaji wa chokaa, lakini katika maeneo mengine ya Lugufu kuna leseni saba za uchimbaji ambayo pia yako kwenye hifadhi. Kwa hiyo, hilo halina shida, lakini kama ulivyosema tutaendelea kukaa na wenzetu ili wananchi wa Kasulu na maeneo ya jirani waendelee kunufaika na uchimbaji wa madini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na kutenga maeneo. Kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi na ambavyo nimesema katika swali langu la nyongeza la kwanza ni kwamba tunaendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo nchi nzima. Kwa sasa tumeshatenga maeneo saba katika Mkoa wa Geita na katika Mkoa wa Kigoma katika eneo linaloitwa Kinyo na Janda tutatenga maeneo hayo kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa chokaa katika Wilaya ya Kasulu. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kuna baadhi ya maeneo nchini mfano Wilaya za Manyoni na Bahi imebainika kuwa kuna madini ya *uranium* na inasemekana kwamba madini haya yana thamani kubwa sana na yanahitajika maeneo mbalimbali nchini. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuchimba madini hayo ili wananchi wa maeneo yale pamoja na Serikali ifaidike? Ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nilieleza Wakala wa Jiolojia wanafanya utafiti wa kubaini mbale, jiomelia, jiofizikia na jiolojia ili kujiridhisha kama maeneo fulani yana madini ya aina gani. Ni kweli kabisa katika maeneo ya Manyoni, Bahi pamoja na maeneo mengine ya Singida ikiwemo eneo la Sekenke, *GST* wamekuwa wakifanya utafiti. Sasa hivi wanakamilisha shughuli za utafiti kubaini kama hiyo *uranium* ambayo inaonekana inaweza ikatathminiwa ikachimbwa kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika maeneo ya Bahi na maeneo mengine ya Manyoni pamoja na Sekenke yapo madini ya dhahabu na madini megine. Bado *GST* wanajiridhisha lakini mara baada ya kukamilisha maeneo haya yatatengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo ili waweze kuchimba sasa kwa uhakika. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge avute subira, zoezi la ukamilishaji wa utafiti la *GST* likamilike na linatarajija kukamilika mwezi Desemba mwaka huu.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema, Mbunge wa Arusha Mjini, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Mtolea.

Na. 114

Ufufuaji wa Viwanda Nchini

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA (K.n.y. MHE. GODBLESS J. LEMA) aliuliza:-

Agizo la Mheshimiwa Rais la kufufua viwanda ni muhimu na la msingi kwa maendeleo ya Taifa:-

Je, Serikali haioni mradi wa *Kurasini Logistic Centre* unakwenda kinyume na fikra za Mheshimiwa Rais kuhusu viwanda?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI
alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema, Mbunge wa Arusha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mheshimiwa Godbless Lema kwa kutambua na kuthamini fikra za Mheshimiwa Rais juu ya azma ya kujenga Tanzania ya viwanda. Mchango wake na Wabunge wote katika kuhamasisha dhima ya Mpango wa Pili wa Miaka Mitano ni muhimu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Mradi wa *Kurasini Logistic Centre* tunaouhamasisha sasa ni mchango na chachu ya maendeleo ya uchumi wa viwanda. Dhamira yetu ni kuona mradi huo unaendeshwa na sekta binafsi kwa misingi ya kibashara. Serikali imefidia eneo hilo kwa takribani shilingi bilioni 101 hivyo kiasi hicho ni mtaji wa Serikali katika mbia atakayechaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la *Kurasini Logistic Centre* mwekezaji atawajibika kufanya yafuatayo:-

(i) Kujenga miundombinu ya viwanda ikiwemo magodown ya viwanda, barabara, mifumo ya nishati na maji;

(ii) Kutafuta wawekezaji (*operators*) ambao watanunua malighafi kutoka ndani na nje ya nchi na kuzalisha bidhaa katika *industrial shed* nilizozitaja hapo juu;

(iii) Kuwa na mchakato wa kuzalisha bidhaa katika maeneo hayo;

(iv) Kufundisha na kuajiri vijana wa Kitanzania na kutumia *Kurasini* kama kituo cha mauzo ya bidhaa zinazosalishwa viwandani ambapo ni mauzo ya jumla tu yatakayofanyika katika sehemu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu unakwenda sawa na fikra za Mheshimiwa Rais za kujenga viwanda ili kutengeneza ajira kwa vijana na kuzalisha bidhaa zenye ubora wa kukidhi mahitaji ya soko la ndani na soko la nje.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Mtolea, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na heshima kubwa ninayompa Mheshimiwa Mwijage, lakini nasikitika kwa majibu yake mepesi kiasi hiki na hii ndiyo inayothibitisha mawazo ya baadhi ya watu ambao wanafikiria kwamba mradi huu ukitekelezwa basi utakuwa umeathiri zoezi zima la kujenga viwanda katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, fidia ambayo Mheshimiwa Waziri anaizungumza hapa ililipwa zaidi ya miaka saba nyuma na mpaka leo bado eneo hilo liko wazi, hakuna hatua yoyote nyingine iliyopigwa baada ya ulipaji wa fidia.

Sasa swali la kwanza, kwa kuwa bado kuna malalamiko makubwa kwa waliohamishwa katika eneo hilo kwamba hii fedha shilingi bilioni 101 inayotajwa hapa inawezekana kabisa haikuwfikia waliostahili kufikiwa kwa maana ya waliohamishwa katika eneo lile na bado wanalamika mpaka leo, je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari sasa kufungua milango ya majadiliano na wanaodai fedha hizi ili aweze kuona wapi zilipopotelea? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa sababu ni kwa muda mrefu Wizara imeshindwa kumpata mbia wa kuendeleza eneo hilo labda kwa sababu ya urasimu ambaou upo kwenye Wizara, je, atakuwa tayari sasa kuwakabidhi Halmashauri ya Temeke ambayo iko *aggressive* zaidi kuona ule mradi unatekelezwa watafute mbia na waweze kuendeleza eneo hilo? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio fidia imelipwa siku nyingi na watu wote wamelipwa, ambao hawajalipwa ni watu watatu kwa sababu mtathmini hakufanya hakufanya kazi hiyo. Kazi niliyofanya, nimemuagiza *DG* wa *EPZA* aende kwa Mkuu wa Wilaya na Mamlaka ya Kata kusudi wakae na watu wao waweze kufidiwa. Wale watu hawakufidiwa kwa sababu mthamini hakuwathamini. Mimi nimeona busara hiyo na watu wamezungumza na mimi nimeagiza kwamba wafidiwe. Kwa hiyo, eneo lile liko tayari kwa ajilli ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kwamba eneo limekaa siku nyingi, inanirudisha kwenye historia, kazi ninayofanya ndio muhimu kwako kukueleza kwamba sasa kazi ninayofanya, eneo limetangazwa, wawekezaji wako tayari na ili uweze kujenga pale unafuata sheria za manunuzi na ndizo tunazozifuata. Hata Halmashauri yako ikilia kujenga itafuata sheria za manunuzi. Lakini nikupe imani kwamba Kurasini ambalo ni eneo lako la Jimbo itakuwa sehemu nzuri ya viwanda lakini la muhimu kwa wale wenye mashaka na mimi ni kwamba bidhaa zitakazozalishwa pale zitauzwa kwa jumla, hazitauzwa Kariakoo wala Temeke. Lazima eneo lile litoe ajira na mafunzo kwa vijana wako wa Temeke na Tanzania kwa ujumla. Hayo ndio maslahi yako, maslahi yako ya viwanda iwe ajira mengine yatafuata baadaye.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mariam Kisangi, swalii la nyongeza.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swalii la nyongeza. Pamoja na juhudii za Serikali na Wabunge wote tuliokuwepo katika Bunge lililopita katika kuhakikisha mradi huu wa Kurasini unatekelezeka; na kwa kuwa Serikali imetumia gharama kubwa katika kuwekeza mradi wa *Kurasini Logistic Center*; na kwa kuwa wananchi wa Temeke na Dar es Salaam kwa ujumla hususan wanawake na vijana tunataraja kupata fursa kubwa sana za ajira katika eneo hilo la *Kurasini Logistic Center*, na kwa kuwa mimi kama Mjumbe wa *PIC* ...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa naomba uulize swali tafadhali.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Je, ni lini sasa Serikali itaanza kutekeleza mradi ule? Nataka *commitment* ya Serikali. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwijage Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji majibu.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni bora nilieleze, mimi katika ofisi yangu katika Wizara ninayoiongoza, nimeanzisha mkakati unaoitwa *fast-tracking of industrialization in Tanzania*. Kuna mambo yanaendelea mimi sifurahishwi nayo, ukifuata sheria za manunuzi na mchakato wake ambazo Bunge tulipitisha shughuli hili haziwezi kuanza. Mimi ningependa kuanza leo, wawekezaji ninao, nawajua lakini lazima nifuate sheria. Kwa hiyo, nitifuata *fast-tracking* na nimeamua sasa kwenda kwenye Baraza la Mawaziri, wakiniruhusu nianze kesho, nawahakikishia kabla ya mwezi wa tano nitakuwa nimeanza. Kwa hiyo, ni *fast-tracking*, mimi nakwenda kwa wakubwa zangu, Mawaziri wako hapa, waniruhusu naanza. (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, sasa aulize swali lake.

Na. 115

Hitaji la Meli ya Mizigo Dar es Salaam Hadi Mtwara

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM aliuliza:-

Serikali imesema ina mkakati wa kujenga viwanda katika Mkoa wa Mtwara, lakini njia ya usafirishaji wa mizigo inayotumika ni barabara tu hali inayosababisha barabara hiyo kuwa na uwezekano wa kuharibika kwa haraka:-

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha meli ya mizigo itakayotoka Dar es Salaam kwenda Mtwara ili kuinusuru barabara hiyo isiharibike?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa uwepo wa huduma mbadala za meli za mizigo na abiria kati ya Dar es Salaam na Mtwara na maeneo mengine ya mwambao ni jambo muhimu kwa maendeleo na kuzifanya barabara zidumu kwa muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa mahitaji ya huduma za usafiri wa majini katika mwambao wa bahari yetu ni fursa kwa sekta binafsi nchini. Serikali kwa upande wake inaendelea kujenga mazingira wezeshi na kuhamasisha sekta binafsi kutumia fursa hii kutoa huduma za usafiri wa majini katika mwambao kwa kutumia meli za kisasa. Hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa kwa lengo la kuchochea sekta binafsi nchini kufanya uwekezaji katika huduma hii. Moja ya hatua hizo ni kuzuia meli za kigeni kuijingiza katika usafirishaji wa shehena katika maeneo ya mwambao yaani *cabbotage restriction* ambapo lengo la zuio hili ni kuwalinda wawekezaji wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuendelea kutoa wito kwa wawekezaji kuwekeza katika vyombo vyya kisasa vyya usafiri wa majini ili kutoa huduma ya usafiri katika maeneo ya mwambao wa Tanzania ikiwemo Mtwara.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masoud Salim, swali la nyongeza.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imekiri kuwepo kwa mahitaji mbadala ya usafirishaji wa mizigo kutoka Mtwara - Dar es Salaam, Dar es Salaam - Mtwara; na kwa kuwa Kampuni ya Dangote peke yake ina magari 600 ambayo Mheshimiwa Rais aliyazindua na *GSM* ina magari 300 jumla yote ni magari 900 ambayo yanasafirisha saruji kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam; na kwa kuwa barabara hii inaenda kuharibika; Serikali ituambie ina mkakati gani wa dharura na wa makusudi inaopanga kuchukua ili kuinusuru barabara hii isiharibike? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, kwa kuwa inavyooneka mtazamo wa Serikali ni kwamba haitaki kufahamu ukubwa wa tatizo hili. Ikitokea Mheshimiwa Naibu Waziri kwa muda mrefu hamjampata mwekezaji kama mlivyo sema na barabara hii inaenda kuharibika, je, Serikali haioni kwamba mtakuwa mmeanza kutafuta mkandarasi mwininge ambaye atatumia fedha nyngi kujenga barabara hii ya Dar es Salaam - Mtwara, jambo ambalo ni matumizi mabaya ya fedha za umma? Je, uko tayari kuwajibika kwa hili? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliiano, majibu.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu kuwa na usafiri wa baharini hasa ukiangalia kwamba barabara zetu zinaharibika sana. Ukichukua kwa upande wa Bandari ya Mtwara, sasa hivi ipo meli ambayo inasa firisha saruji ya Dangote kutoka Mtwara kwenda Zanzibar. Takribani kila mwezi meli hiyo inasa firisha tani 6,000 sawa na magari 200. Sasa hivi Serikali ikishirikiana na Dangote na watu wengine tunaendelea kuhakikisha kwamba mzigo mkubwa wa saruji kutoka kwa Dangote unasa firishwa kwa meli ili kuhakikisha kwamba barabara yetu ile inadumu kwa muda mrefu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecil Mwambe.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Swali la Mheshimiwa Masoud ambalo kwa masikitiko tu niseme Mheshimiwa Waziri hajalijibu kadri ya mahitaji ya watu wa Mtwara na Kusini kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali letu sisi ni kwamba kwa kipindi cha miaka 50 iliyopita Serikali ilikuwa hajatengeneza barabara inayounganisha Mtwara na Dar es Salaam. Baada ya utengenezaji wa barabara hii na mara Kiwanda cha Dangote kikafunguliwa ambacho kina magari zaidi ya 1,500 yanayosafirisha *cement* kutoka Mtwara na kuzileta Dar es Salaam.

Sasa tunataka kufahamu Serikali kwa nini isizue usafirishaji wa *cement* kwa kutumia magari ambayo yanaleta uharibifu mkubwa sana kwenye barabara za Mtwara, Lindi kufika Dar es Salaam na badala yake wanawaaachia wasafirishaji wale wale wa magari. Kwa nini wasizue na wakapa uwezo watu wa kuleta meli wakasafirisha *cement* hiyo mpaka Dar es Salaam kwa *distributors?* (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyozungumza na Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema kwenye jibu lake la msingi, kwanza barabara ile imekuwa *designed* kuchukua mzigo mkubwa, hilo la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili mzigo wote wa Dangote wa *cement* hauendi Dar es Salaam, unaenda sehemu mbalimbali za Tanzania na tatu, Serikali tunaendelea kufanya utaratibu na kampuni mbalimbali za meli kuhakikisha kwamba mzigo huo unakwenda kupitia vilevile upande wa baharini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Daimu Mpakate, swali la nyongeza.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mazingira ya barabara ya Mtwara yanafanana kabisa na mazingira ya barabara ya kutoka Masasi – Mangaka – Tunduru - Songea - Mbanga kutokana na machimbo yanayoendelea ya makaa ya mawe pale Ngaka, Mbanga. Makaa yale yanasafrishwa kwa malori makubwa yenye zaidi ya tani 30 kupitia barabara ya Tunduru – Mtwara - Lindi - Dar es Salaam. Je, Serikali ina mpango gani wa muda mrefu wa kujenga reli ili makaa yale yaweze kusafirishwa kwa njia ya reli kwa sababu magari yale yanahatarisha usalama wa barabara yetu? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hiyo inasafirisha mzigo mkubwa lakini kila kwenye barabara tumeweka mizani ambayo kazi yake kubwa ni kuhakikisha kwamba magari hayo hayazidishi mzigo ili kuhakikisha kwamba barabara hizo zinadumu kwa muda mrefu. Kwa hiyo, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuitumia barabara hiyo lakini tutahakikisha kwamba magari hayo hayazidishi mzigo ili kulinda barabara yetu.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni, sasa aulize swali lake.

Na. 116

Mnara wa Simu Kuwashwa Katika Kijiji cha Kwamatuku

MHE. OMARI A. KIGODA aliuliza:-

Je, ni lini Kampuni ya Simu iliyofunga mnara wake katika kijiji cha Kwamatuku itauwasha ili wananchi wapate huduma?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote uliikabidhi Kampuni ya Simu ya *MIC* (Tigo) kazi ya kujenga mnara katika kata ya Kwamutuku yenye vijiji vya Komsala, Kwamatuku, Kweingoma na Nkale. Ujenzi huo ulikamilika mwishoni mwa mwaka 2015 na kuanza kutoa huduma katika kata hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa za Kampuni ya Simu ya Tigo, mnara huu wa Kwamatuku uliwashwa na upo hewani ukioa huduma za mawasiliano tangu tarehe 4 Desemba, 2015. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tumetuma wataalamu wetu waende na vifaa vya kupima mawasiliano ili kuhakikisha kwamba taarifa hii ya Tigo iko sahihi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Omari Kigoda, swali la nyongeza.

MHE. OMARI A. KIGODA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa napenda niwashukuru Mawaziri na Wizara yao kwa kutekeleza ahadi hii. Swali langu la nyongeza, kwa kuwa kampuni za simu huwa zinaangia mikataba na Serikali za Vijiji, ni kwa kiasi gani Wizara imefuatilia mikataba hii ukizingatia mingi inakuwa na madalali ambao wanapata hela nydingi kuliko Serikali? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba

nimhakikishie Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda kwamba Serikali za Vijiji chini ya TAMISEMI zinasimamiwa vizuri na sasa wenzetu TAMISEMI wanataka kuweka mpango wa kuhakikisha kwamba mikataba yote inayoingiwa kati ya vijiji na wawekezaji tunakuwa na wataalam wa sheria kutoka Halmashauri wanaohakikisha kwamba maslahi ya wanavijiji yanalindwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge masuala haya na sisi tunayafuatilia kwa sababu yanatuletea picha siyo nzuri sana kwa wawekezaji wetu tunaowapeleka maeneo mbalimbali ya vijiji wanakojenga minara. Tutayafuatilia na baadaye tutakuja kukuletea mrejesho kupitia wenzetu wa TAMISEMI.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa swali hili la mawasiliano linafanana sana na matatizo katika Jimbo la Kilindi katika Kata za Saunyi, Kwekivu na Tunguli. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini kampuni za mawasiliano zitaweza kuweka minara katika Jimbo langu la Wilaya ya Kilindi? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kukutajia ni lini nitakuwa sikutendei haki. Nikuhakikishie tu ombi lako tumelipokea, tutalifanya kazi kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) na hatimaye utapata majibu kwa vitendo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

**Huduma za Benki ya Kilimo kwa Wakulima
Wadogo Wadogo**

MHE. FELISTER A. BURA aliuliza:-

Serikali imeanzisha Benki ya Kilimo kwa lengo la kusaidia wakulima wakubwa na wadogo kupata mikopo ya pembejeo kwa haraka:-

Je, ni lini Benki hiyo itaanza kutoa huduma kwa wakulima wadogo wadogo wa Mkoa wa Dodoma?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilianza rasmi shughuli zake mwishoni mwa mwaka 2015. Hadi kufikia Desemba 2016, Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilikuwa imeshatoa mikopo ya jumla ya Sh. 6,489,521,120/= kwa miradi 20 ya kilimo katika Mikoa ya Iringa, Morogoro na Tanga. Sambamba na utoaji wa mikopo, benki inatoa mafunzo kwa wakulima na hadi sasa imeshafanya mafunzo kwa vikundi 336 vya wakulima wadogo wadogo vyenye jumla ya wanachama 44,400 katika Mikoa ya Iringa, Morogoro na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mkoa wa Dodoma, Benki imepata nafasi kwa ajili ya kufungua ofisi katika jengo jipyaa la PSPF ambapo inasubiri kukabidhiwa ofisi hiyo Julai, 2017, baada ya mkandarasi kukamilisha ujenzi. Aidha, benki imeshaanza kutafuta miradi ya kilimo ya wakulima wadogo wadogo yenye sifa za kukopesheka iliyopo katika Mkoa wa Dodoma na mikoa mingine ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha azma hii, benki imemwandikia barua Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma kumwomba aipatie miradi mizuri ya kilimo ambayo mkoa unapendekeza Benki iifikirie katika zoezi la kutoa mikopo. Pamoja na hayo, benki inaandaa utaratibu wa mafunzo yatakayotolewa kwa wakulima wadogo wadogo nchi nzima ikianzia na Mkoa wa Dodoma. Ni matumaini ya benki kuwa mikopo kwa wakulima wadogo wadogo na wakati kwenye Mkoa wa Dodoma itanza kutolewa mwishoni mwa mwaka 2017. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Felister Bura, swalii la nyongeza.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza nilpongeze Serikali kwa uamuzi wa kufungua Benki ya Maendeleo ya Kilimo Mkoani Dodoma na kukubali kutoa mafunzo kwa wakulima wadogo wadogo Mkoani Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo imeanzishwa kwa malengo ya kuwawezesha wakulima kupata mikopo kwa masharti nafuu na kwa haraka zaidi. Je, Serikali iko tayari kupunguza sasa riba ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili wakulima wengi wapate kufaidika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, kwa kuwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo ni mkombozi kwa wakulima. Je, Serikali iko tayari sasa kuhakikisha kwamba mikoa yote wanapata matawi ya benki hii ili wakulima wasihangaike kwenda Dar es Salaam na Dodoma kufuatilia mikopo? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa

Felister kwa kuwa mbele katika kufuatilia miradi ya maendeleo ndani ya Mkoa wetu wa Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza ameuliza kuhusu kupunguza riba. Kwanza nimkumbushe kwamba Benki hii ya Maendeleo ya Kilimo ilianzishwa kwa malengo makuu mawili. Moja ni kuchangia utoshelezi na usalama endelevu wa chakula nchini na pia kusaidia mapinduzi ya kilimo kutoka katika kilimo cha kujikimu na kwenda kilimo cha kibashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutimiza malengo haya, Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili iweze kufanya kazi hizi ni lazima iwe na mtaji wa kutosha na pia imekuwa iki-lobby katika taasisi nyingine za kifedha ili ziweze kutoa mikopo katika sekta ya kilimo. Benki hii ili iweze kupata mtaji wa kutosha sasa hivi Serikali imeshairuhusu Benki ya Maendeleo ya Kilimo iweze kupata mkopo wa bei nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na iko mbioni kuupata na nina uhakika itaweza kutoa mikopo hii kwa bei nafuu kwa wakulima wetu wadogo wadogo na wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ili kutimiza pia malengo haya Benki yetu ya Kilimo iliandaa mpango wa biashara wa miaka mitano ambao umeanza kutekelezwa kuanzia mwaka 2017 - 2021. Katika kutekeleza mpango huu wa biashara wa Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo imedhamiria kufungua ofisi sita za kikanda ndani ya Tanzania, ambazo ni Kanda ya Kusini, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kati, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Ziwa Viktoria pamoja na Zanzibar. Baada ya kufunguliwa ofisi hizi za kanda nchi nzima ni imani yetu sasa tutaweza kuwafikia wakulima wetu kule walipo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amina Makilagi, swali la nyongeza.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, wanawake wa Tanzania kwa

kiwango kikubwa walio wengi ndiyo wakulima; na kwa kuwa wanawake wa Tanzania hawana fursa za kiuchumi zitakazowafanya wafikie Benki hii ya Wakulima kwa sababu ya kukosa dhamana. Napenda kujua Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wanawake wengi amba ni wakulima waishio vijijini wanafikia fursa hii ya kupata mikopo katika Benki ya Wakulima kwa lengo la kuwakomboa kiuchumi? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wanawake wengi wa Tanzania ndiyo wanaojihusisha katika kilimo hapa nchini. Serikali kwa kutambua hilo imeweka mipango mbalimbali ikiwemo ukopeshaji wa vikundi vya akinamama katika uzalishaji kipitia Halmashauri zao lakini pia tunatoa kipaumbele katika Mfuko wa Pembejeo. Wanawake wanaokwenda kukopa katika Mfuko wa Pembejeo wanapata kipaumbele kwa sababu wao wanafahamika ndiyo wanaoshiriki zaidi katika shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio Benki ya Kilimo tu inayotoa mikopo katika sekta ya kilimo, benki nne hapa nchini kwa sasa zinatoa fedha katika shughuli za kilimo. Utoaji wa fedha hizi hauko katika shughuli yenyewe ya kilimo tu, isipokuwa benki zinatoa fedha katika mnyororo mzima wa thamani katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Benki ya *NMB* mwaka huu pekee wa fedha imetenga shilingi bilioni 500 kwa ajili ya shughuli za kilimo na akinamama wana kipaumbele. Masharti ya mikopo katika benki ambazo tumezungumza nazo za *NMB*, *Commercial Bank of Africa*, *CRDB*, wote wamepunguza masharti katika mikopo ya kilimo ili kuwawezesha Watanzania wengi na hasa wale wasio na dhamana kuweza kupata mikopo hii kwa urahisi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Othman Omar, swali la nyongeza.

MHE. OTHMAN OMAR HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa mujibu wa Msajili wa Hazina, Benki ya Kilimo inawajibika kutoa huduma zake Tanzania nzima. Napenda kumuuliza Naibu Waziri, ni kwa nini benki hii haijafikisha huduma zake kule Visiwani Zanzibar? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyo sema kwenye jibu langu la Msingi, katika utekelezaji wa mpango wa biashara wa Benki hii ya Maendeleo ya Kilimo, imepanga kufungua ofisi sita za kikanda na Zanzibar ikiwemo. Ni imani yangu baada ya kufungua Ofisi ya Kikanda Dodoma, Ofisi ya Kikanda ya pili itakayofunguliwa ni Ofisi yetu ya Visiwani Zanzibar.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 118

Changamoto Zinazowakabili Wakulima wa Kahawa

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA aliuliza:-

Moja kati ya changamoto zinazowakabili wakulima wa kahawa ni kodi na makato mengi:-

Je, ni lini Serikali itazipiga marufuku kodi zote zinazomnyonya mkulima?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto mbalimbali katika uzalishaji wa kahawa nchini ikiwemo kodi na tozo mbalimbali zinazotozwa kwa wakulima na wadau wengine katika tasnia ndogo ya kahawa ambazo zimekuwa na athari katika mapato ya wakulima. Serikali imedhamiria kupunguza na kuondoa kodi na tozo mbalimbali za mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi zisizokuwa na tija ili kupunguza mzigo wa makato kwa wakulima, wafugaji na uvuvi na hivyo kuongeza kipato na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara katika sekta ya kilimo kwa kuititia upya taratibu, vibali, tozo, kodi, ushuru na ada mbalimbali zinazotozwa ili kupunguza gharama za kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mkakati wa kupunguza kodi, tozo na ada mbalimbali kwa wakulima, Serikali katika mwaka 2016/2017, imefuta baadhi ya tozo katika mazao ya kilimo, ikiwemo ada ya leseni ya kusindika kahawa ya Dola za Kimarekani 250. Aidha, katika mwaka 2017/2018, Serikali imepanga kuondoa na kupunguza baadhi ya kodi, tozo na ada katika mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, ikiwemo zao la kahawa ili kuongeza mapato ya wakulima na kuboresha mazingira ya ufanyaji wa biashara katika kilimo, mifugo na uvuvi. Mpango wa muda mrefu wa Serikali ni kuhakikisha kodi, tozo na ada mbalimbali ambazo ni kero kwa wakulima wa kahawa zinafutwa na kubakia na kodi, tozo na ada ambazo zina mahusiano na uendelezaji wa zao husika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sixtus Mapunda, swalii la nyongeza.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri na yenye matumaini kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa muda mrefu unaosemwa na Serikali, umesemwa kwa miaka mingi sana. Hata mwaka 2015, Rais wetu mpendwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli katika kampeni zake alisema hakuna zao lenye tozo na kodi za ajabu ambazo hazi-*exist* duniani kama zao la kahawa, alisema lina kodi 26. Mwaka jana ametoa kodi moja tu ya usindikaji wa kahawa dola 250, bado kuna kodi 25, hatuoni *commitment* ya Serikali kwenye hili. Mbona tumefanikiwa kwenye korosho mwaka jana imefuta kodi zote na wananchi wakulima wa korosho wanaishi vizuri? Naiomba Serikali iji-*commit* kwenye hili mwaka huu iondoshe hizo kodi zote kwa sababu haya matumaini tumeyachoka. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la tozo, kodi, limekuwa likizungumziwa kwa muda mrefu na ni kweli vilevile kwamba Mheshimiwa Rais wakati wa ziara yake ya kampeni ni moja kati ya masuala ambayo aliahidi kwamba atayafanya kazi. Sisi kama Wizara tumeendelea kutekeleza sio katika zao la kahawa tu lakini katika mazao yote ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Sixtus Mapunda kwamba tarehe 22 Mei, tutakuja na mapendelezo ya kufuta tozo mbalimbali katika mazao ya biashara. Katika hili nimuahidi kwamba tutavuka mategemeo yake. Siku hiyo ya tarehe 22 mimi mwenyewe nitahakikisha namwita aje Bungeni kusikiliza. Katika hili tutaleta, sisi tunasema mapinduzi makubwa, tutaondo tozo nyingi sana sio katika kahawa pekee bali katika mazao yote ya biashara.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa John Heche, swali la nyongeza.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Suala la kahawa kule kwetu kuna kata zaidi ya tano zinalima kahawa; Kata ya Mriba, Nyanungu, Itirio na maeneo mengine ya Tarime Mjini pia Kitale wanalamia kahawa. Watu wa maeneo mengine wamefyeka kahawa zao kwa sababu wanaona ni kilimo kisichokuwa na tija. Mwenzangu amelalamikia kodi na tozo, ni kweli zipo, lakini kule kwetu nalalamikia bei. Ukichukua bei za kahawa zinazonunuliwa kwa mfano upande wa Kaskazini, japo bado zipo chini, ni tofauti na za Tarime na maeneo mengine ya kule Mara. Ukichukua bei zilizoko Kenya, sisi tuko mpakani, Kenya bei iko juu...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Heche naomba uulize swali tafadhalii, muda umekwenda kidogo.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kenya mpakani bei inakuwa juu kuliko sisi. Sasa nauliza Serikali ni kwa vipi watu wengine wote bei zao zinakuwa tofauti na sisi? Ni kwa nini wasifanye bei hiyo ipande ili wakulima wale wasifyeke kahawa zao iwe ni katii ya zao ambalo linawapatia faida?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge anavyosema kwamba nchi za jirani bei ya kahawa ni nzuri kuliko bei tuliyonayo nchini. Moja katii ya sababu zinazofanya bei yetu ya kahawa iwe chini ukilinganisha na nchi za jirani ni kwa sababu ya utitiri wa tozo na kodi ambazo zinafanya ile bei anayopata mkulima kuwa ndogo. Ndiyo maana nimesema mwaka huu tutapunguza tozo na kodi kuzidi mategemeo yenu kwa wakati wowote ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kodi hizi sio kwamba zina athari tu kwa bei ya zao hili kwa wakulima lakini zina athari katika mazingira ya ufanyaji biashara. Wawekezaji na wanunuzi wengi wa kahawa hawaji Tanzania kwa sababu kimsingi mazingira ya kufanya biashara ni magumu, ikisababishwa pamoja na mambo mengine na utitiri wa kodi na nyingine zinawagusa wao moja kwa moja. Kwa hiyo, tunapopunguza zitakuwa na faida sio tu ya kuongeza bei anayopata mkulima lakini vilevile kuwavutia wanunuzi wengi zaidi ili ushindani uwe mkubwa na hivyo bei kuongezeka. Naomba naye asubiri tarehe 22 ataona mapinduzi haya ambayo tunayazungumzia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hasunga, swali la nyongeza.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya swali hili yanafanana kabisa na mazingira ya wakulima wa Wilaya ya Mbozi na hasa katika Jimbo la Vwawa. Kwa kuwa, moja ya gharama kubwa ambazo wakulima wa kahawa wanazipata ni pamoja na kusafirisha kahawa yao kupeleka kwenye mnada kule Kilimanjaro. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba Mnada wa Mloo unafunguliwa ili kupunguza ushuru na tozo mbalimbali ambazo zinawakabili wakulima wa zao la kahawa wa Wilaya ya Mbozi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba mnada mkubwa wa zao la kahawa upo Moshi. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika jitihada za Serikali za kuboresha mazingira ya zao la kahawa suala la minada na mahali panapofanyika ni moja kati ya masuala tunayofanyia kazi. Kwa hiyo, avute subira, nina hakika muda sio mrefu tutakuwa na suluhisho katika hili.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Ninayo matangazo kadhaa, tutaanza na tangazo la wageni walio tufikia asubuhi ya leo.

Kundi la kwanza ni Balozi wa Iran nchini Tanzania, Mheshimiwa Balozi Mousa Frahang akiwa ameambatana na Ndugu Maisara Ally ambaye ni Katibu wa Balozi na Ndugu Kisa Mwaseba ambaye ni Afisa, Wizara ya Mambo ya Nje. Karibuni sana. (*Makofi*)

Pia tunao wageni kutoka Chama cha Maskauti Tanzania ambao ni Ndugu Mwantumu Mahiza ambaye ni Skauti Mkuu, Ndugu Abdulkarim Shah ambaye yeye ni Kamishna Mkuu, Balozi Nicholas Kuhanga ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji ya Taifa, Mheshimiwa Eline Kitally ambaye ni Kamishna Mtendaji, Ndugu Florian Mpagale ambaye ni Kamishna wa Skauti wa Wilaya, Dodoma Mjini na Dkt. Japhet Swai ambaye ni Kamishna wa Skauti, Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Profesa Maghembe ambao ni wanafunzi 25 na Walimu watano kutoka Sekondari ya Vudio, Mwanga. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wanafunzi walio tembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Tangazo la pili linatoka kwa Mheshimiwa Spika. Anawatangazia kwamba ametaarifiwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, atakaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni kwa kuwa Waziri Mkuu hayupo, ana shughuli nyiningine. Mpaka atakaporejea Mheshimiwa Mwinyi atakuwa akikaimu nafasi hiyo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu), Mheshimiwa Jenista

Mhagama, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, tarehe Mosi Mei ya kila mwaka ni maadhisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani ambapo wafanyakazi wote nchini wanaungana na wenzao duniani kuadhimisha siku yao ya kimataifa. Kwa mwaka huu maadhisho hayo kitaifa yatafanyika Mjini Moshi, Mkoani Kilimanjaro siku ya Jumatatu, tarehe Mosi Mei, 2017. Kauli Mbiu ya maadhisho ya mwaka huu ni ‘uchumi wa viwanda uzingatie kulinda haki, maslahi na heshima ya wafanyakazi’.

Waheshimiwa Wabunge, mgeni rasmi katika maadhisho hayo atakuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt, John Pombe Joseph Magufuli. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu anawatakia wafanyakazi wote nchini maandalizi mema ya maadhisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani na anawakaribisha Waheshimiwa Wabunge Moshi kwenda kuhudhuria sherehe hizi. (*Makofii*)

Tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (*TWPG*), Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, anawatangazia Wabunge wote wanawake kuwa leo 28 Aprili, 2017 kutakuwa na semina kwa ajili ya Wabunge wote wanawake itakayofanyika katika ukumbi wa zahanati ya zamani ya Bunge mara tu baada ya kuahirisha kikao cha Bunge saa 7.00 mchana. Wanawake wote mnaombwa kuhudhuria. (*Makofii*)

Tangazo lingine linatoka Ofisi ya Utawala (Bunge), wanawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa siku ya kesho Jumamosi tarehe 29 Aprili, 2017 kutakuwa na semina kwa Wabunge wote kuhusu masuala ya UKIMWI. Semina hiyo ambayo itaratibiwa na Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (*NACOPHA*) itafanyika katika ukumbi wa Bunge kuanzia saa 4.00 asubuhi. Waheshimiwa Wabunge, kwa umuhimu wa semina hii wote mnaomba kuhudhuria.

Tangazo lingine linatoka pia Idara ya Utawala (Bunge) linahusu uhakiki wa wanufaika wa mkopo wa masomo ya elimu ya juu. Ofisi ya Bunge kwa nyakati tofauti imepokea

barua kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ambayo imewataka kufanya uhakiki kwa Waheshimiwa Wabunge ambao mionganii mwenu kwa nyakati tofauti mliwahi kunufaika na mkopo wa elimu ya juu iliyo kuwa ikitolewa na Bodi kuanzia mwaka wa masomo 1994/1995. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Katibu ya Bunge inawaomba kujihakiki ikiwa mionganii mwenu wapo ambao walinufaika na mkopo huu lakini hawajaweza kurejesha fedha walizokopeshwa na Bodi. Utaratibu huu wa uhakiki unafanyika kwa kuwa wengi wa Waheshimiwa Wabunge kabla ya Novemba, 2015 mlikuwa kwenye majukumu mengine ya kikazi na kusababisha makato ya mikopo kusimama na kuonekana kama mdaiwa sugu suala ambalo siyo sahihi.

Waheshimiwa Wabunge, umuhimu wa kujihakiki utawasaidia ambao hamjarejesha mikopo ya elimu ya juu kuondokana na usumbufu usio wa lazima ikiwemo kuchukuliwa hatua za kisheria, kudhalilika na kufikishwa Mahakamani. Tafadhali mnaombwa kujihakikiki kwa kujaza fomu zilizoambatanishwa na dokezi hili. Kwa hiyo, wale vijana wetu watapita kuwa letea hii fomu ili mjiandikishe wale ambao bado mnadaiwa. Tafadhali lipeni mkopo hata mimi nilisoma kwa mkopo na nimeshalipa. Kwa hiyo, tangazo hili jamani uhakiki.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Kapteni wa *Volleyball Wanawake*, Mheshimiwa Saumu Sakala, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba wale wanawake wanaopenda kujunga na *volleyball* tafadhali wamuone ili waanze mazoezi na anawakaribisha wanawake wote kwa sababu ana uwezo wa kuwafundisha. Anasema *volleyball* ni akili hakuna nguvu, kwa hiyo, wenye akili wote naamini watajunga na *volleyball*. (*Makofi/Kicheko*)

Tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, anawatangazia kwamba kutakuwa na mechi ya kirafiki itakayochezwa siku ya *May Day*, tarehe 1 Mei, 2017, *Jamhuri*

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Stadiumsaa 10.00 jioni kati ya *Bunge Sport Club Football* dhidi ya *Morogoro Kumba Muslim Club* inayoongozwa na Mheshimiwa Saddiq Suleiman, Mbunge wa Mvomero. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnaombwa mwende kucheza mpira lakini pia mkawashangilie Wabunge wetu wakati wakicheza.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa matangazo tunaendelea.

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kuhusu jambo ambalo limetokea mapema Bungeni leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano akijibu Swali Na. 116 la Mheshimiwa Kigoda, alisema kwamba Halmashauri zetu na Serikali za Mitaa zinasimamiwa vizuri katika suala zima la ukusanyaji wa *service levy* kutoka kwenye mitandao ya simu ya 0.03%. Majibu haya yamekuwa yakijirudia mara kwa mara hata jana yalitolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kumbukumbu zangu, katika Bunge la Kumi liliopita wakati Mheshimiwa Hawa Ghasia akiwa Waziri wa TAMISEMI na mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI chini ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, hili jambo tulilishughulikia kwamba Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Wizara ya Mawasiliano wakae chini waweze kukusanya kodi hii *centrally* kwa sababu Halmashauri zetu hawawezi kujua *exactly* mitandao hii inakusanya kiasi gani na hili lilijibowiwa muda wote wa Bunge liliopita lakini sasa Bunge hili majibu yanayokuja ni kwamba Halmashauri zetu zinakusanya na hizi fedha zinasimamiwa vizuri. Mimi ni Mjumbe katika Baraza la Madiwani, Halmashauri ya Mji wa Babati hili ni tatizo ukiachilia

mbali mikataba ya watu binafsi, lakini Halmashauri na Serikali hatupati makusanyo halisi ya fedha hizi ambazo zingesaidia Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako ni kwa nini Serikali wasikae waka-*reconcile* hili na majibu ya nyuma na hatua ambazo zimechukuliwa badala ya kuturudisha kule kule ambako tulishashindwa na Halmashauri zetu hazipati gawio hilo kiuhalisi na fedha hizi hazikusanyi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kubenea.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7) nataka kupata mwongozo wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa mjadala wa hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, mmoja wa Wabunge mwenzetu Mheshimiwa Lucy Mayenga alisimama Bungeni akasema, "Wabunge wanaozungumza kwa hisia kali juu ya vitendo vya utekaji na utesaji wamehongwa". Nikasimama kwa Kanuni ya 68(1) kuomba utaratibu. Mheshimiwa Mwenyekiti aliyekuwepo kwenye Kiti alisema kwamba suala hilo hakuliskia na kwa hivyo atasoma *Hansard* baadaye atatoa utaratibu. Wakati nilipokaa, Mheshimiwa Lucy Mayenga aliongeza akasema kwamba ana ushahidi na anachokisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi sijahongwa, Mheshimiwa Halima James Mdee hajahongwa, Mheshimiwa Nape Nnauye nimezungumza naye anasema hajahongwa, Mheshimiwa Hussein Bashe anasema hajahongwa na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare hajahongwa. Jambo hili limelichafua Bunge na zimekuwepo juhudzi za makusudi zinazofanywa kuondoa maneno haya ya kuudhi katika Bunge hili.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba mwongozo wako, uamuzi wa Kiti juu ya maneno makali ya Mheshimiwa Lucy Mayenga utatolewa lini? Je, ni halali kwamba Bunge likawa linafanya kazi *double standard* kwa Wabunge wengine kuchukuliwa hatua pale pale wanapofanya makosa na wakati mwingine hata kusingiziwa na Wabunge wengine wakiwa wanalindwa na Kiti cha Spika?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.
(*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru umekuwa na kigugumizi kunipa nafasi lakini nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waitara usipende kujilalamisha, Wabunge mmesimama wengi na mimi naangalia ninayetaka kumsikiliza wakati huo. Siyo kila wakati lazima uone jambo fulani, tafadhali, umepewa nafasi zungumza.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), tulishaomba mwongozo hapa, mimi ni Mbunge wa Dar es Salaam-Ukonga na Mheshimiwa Waziri Mkuu siku anazungumza baada ya kuomba mwongozo alisema Serikali kwa maana Wizara ya Kilimo na Mifugo itatoa tamko juu ya hali ya chakula Tanzania ikiwemo Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza sasa, kiroba cha kilo 25 Dar es Salaam wanauzu Sh. 50,000 wakati huo kilo 50 za *cement* ni Sh.10,000 mpaka Sh.11,000 kiasi kwamba sasa uwezo wa wananchi kula ni mgumu zaidi kuliko kujenga nyumba zao yaani bei ya *cement* ni ndogo

kuliko bei ya chakula. Vilevile kilo moja ya unga wa sembe au dona kwa Dar es Salaam ni Sh. 2,000, Sh. 2,500 mpaka Sh. 3,000...

MHE. MOHAMED A. KEISSY: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. MWITA M. WAITARA: Wakati mafuta ya *petrol* na *diesel* ni shilingi 2,000 na kitu. Maana yake ni rahisi kununua *petrol* au *diesel* kuliko kununua kilo moja ya unga Dar es Salaam.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Keissy naomba ukae.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwamba ni kwa nini Serikali iliahidi hapa itatoa tamko hali ya chakula na namna ya kupunguza makali ya maisha ya watu wa Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla na mpaka leo tamko hilo halijatolewa. Je, maana yake ni kwamba Serikali haiipi uzito maisha ya Watanzania au imepuuza tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 68(7) sambamba na Kanuni ya 46(1) inayolenga maswali kujibiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Swali Na. 115, swali langu la leo mimi kama Mbunge wa Mtambile nilikuwa naulizia hitaji la kununua meli ya mizigo kutoa Mtwara-Dar es Salaam na Dar es Salaam-Mtwara. Jambo lililoniskitisha leo, napenda kupata ufanuzi wa ziada ili kuweka kumbukumbu sahihi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano anasema Serikali inatafuta wawekezaji meli hiyo haipo lakini Waziri wake Mheshimiwa Mbarawa anasema meli hiyo ipo inachukua saruji kutoka Mtwara kupeleka maeneo mengine. Napenda kupata usahihi ili kuweka kumbukumbu vizuri ni nani amesema kweli, ni nani amedanganya Bunge na nani ni mwongo na nani siyo mwongo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ukweli juu ya hilo.
(*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haonga leo hautapata nafasi ya kuomba mwongozo.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa miongozo kadhaa hapa na Wabunge mbalimbali. Nadhani somo la kuhusu Kanuni hii, Katibu wa Bunge aitishe semina ili Wabunge tuwe hatupotezi wakati kwa kuomba miongozo kwa jambo ambalo halihusiani na Kanuni ya 68(7). (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, narudia kila siku, jambo litokee hapa Bungeni na unataka kujua, je, linaloruhusiwa ama haliruhusiwi. Kwa hiyo na wewe unapoomba mwongozo lazima useme mtu huyu ama Mbunge huyu ama Waziri huyu amefanya moja, mbili, tatu, je, inaruhusiwa Waziri huyu kujibu hivi ama inaruhusiwa Waziri huyu kusema hivi? Sasa unapoleta hadithi ndefu halafu unauliza swali sasa unataka Kiti kikuongoze kwenye lipi? Kwa sababu hapo ni lipi sasa linaloruhusiwa ama lisiloruhusiwa? Waheshimiwa Wabunge, tutumie hizi Kanuni vizuri ili tuutumie muda wetu vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa na Mheshimiwa Pauline Gekul kuhusu majibu ya Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano wakati akijibu swali namba 116 akizungumzia ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Gekul anaomba mwongozo wangu kwamba kwa nini Serikali isikusanye hayo mapato kwa sababu ndicho walichokuwa wameshauriwa. Hapa sijaulizwa ni kipi kinachoruhusiwa na kipi kisichoruhusiwa. Kwa hiyo, hakuna mwongozo uliombwa hapa na Mheshimiwa Gekul. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Kubenea akieleza kuhusu uchangiaji wa Mheshimiwa Lucy Mayenga wakati akichangia hotuba ya Waziri Mkuu. Ameeleza kuhusu Wabunge kadhaa amewataja hapo kwamba maelezo ya Mheshimiwa Lucy yalionesha kwamba wamehongwa na pia akasema alimwomba Mwenyekiti kuhusu maneno hayo na Mwenyekiti akamuahidi kwamba atatoa mwongozo na yeye anauliza swali, je, mwongozo huo utaletwa lini?

Waheshimiwa Wabunge, narudia tena, Kanuni yetu inataka uulize mwongozo kuhusu jambo lilitotokea kama linaruhusiwa ama haliruhusiwi. Kama uliambiwa mwongozo utatolewa na haujatolewa siyo lazima usimame hapa kuuombea mwongozo kwa sababu aliyekaa wakati huo hana uwezo wa kutolea mwongozo, atasema linaruhusiwa ama haliruhusiwi lipi wakati yeye mwenyewe hakuwepo.

Ufutiliaji wa Wabunge upo wa namna nyingi na ndio maana siku zote tunasisitiza na wananchi wanajua siyo kila Mbunge anapata nafasi ya kusimama humu ndani kwa hiyo Wabunge wanafutilia kwa namna mbalimbali. Kwenye hili la Kiti kuahidi jambo, kama Kiti hakijafanya niwashauri Waheshimiwa Wabunge msiombee mwongozo, fuatilia jambo hili kiofisi ili urahisishe majibu yake.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa pia mwongozo na Mheshimiwa Waitara akisema kwamba aliahidiwa na Serikali kwamba hapa lingetolewa tamko kuhusu hali ya chakula. Sijui hiyo ahadi ilitolewa lini, lakini mwongozo wake amemalizia na swali kwamba kwa nini tamko hilo halijatolewa. Kama nilivyotoa majibu kuhusu mwongozo uliombwa na Mheshimiwa Gekul, mwongozo ni jambo lilitotokea na unataka kuju linaruhusiwa ama

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

haliruhusiwi. Sasa swali la kwamba Kiti kiliambia Serikali itoe tamko halafu Serikali bado hajatoa tamko, huwezi kukiuliza Kiti kwamba jambo hili linaruhusiwa ama haliruhusiwi. Natoa ushauri tena kama niliompa Mheshimiwa Kubenea, jambo hilo lifuatiliwe kama ambavyo utaratibu upo wa kufuatilia mambo mengine.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Masoud kuhusu tofauti ya majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu swali lake ambalo lilikuwa linahusu meli ya mizigo na usafirishaji wa mizigo kati ya Mtwara na Dar es Salaam. Hili la Mheshimiwa Masoud nitaenda niangalie *Hansard* majibu hayo yanatofautiana vipi leo mchana atajibiwa mwongozo wake alioomba. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2017/2018 -
Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano**

(Majadiliano yanaendelea)

MHE. NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, tutaanza na Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mheshimiwa James Mbatia na Mheshimiwa Joseph Mhagama ajiandae.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii asubuhi hii ya leo ili nichangie hoja iliyoko mbele ya Bunge lako Tukufu. Nianze kwa kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa wasilisho lake zuri. Naelewa nyuma ya wasilisho hilo ni kazi nzuri iliyofanywa na viongozi wa Wizara hiyo pamoja na taasisi ambazo zipo chini ya Wizara hiyo. Hongereni sana kwa kazi nzuri, tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, niungane tu na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa uamuzi wa hekima na busara lakini wa kijasiri sana kuhusiana na reli ya Kati. Uamuzi huu ni wa msingi sana katika kufungua fursa mbalimbali za maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naendelea kuiomba Serikali iendelee kuweka kipaumbele cha juu katika upatikanaji wa fedha za ujenzi wa reli hii kwa sababu wenzetu wa *Northern Corridor* wako mbali sana na shughuli hii. Kwa hiyo, nami naiomba sana Serikali twende nalo lakini naipongeza sana Serikali kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, njielekeze kwenye mambo ya nyumbani, *politics is always local*. Nianze kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 11- 12 Januari, alitembelea Mkoa wa Simiyu hususan Bariadi Makao Makuu ya Mkoa na Maswa. Akiwa Bariadi alifanya mambo makubwa sana na ndiyo maana wananchi wa Mkoa wa Simiyu tunaendelea kumshukuru sana. Moja, Mheshimiwa Rais alizindua barabara iliyokamilika ya kutoka Lamadi mpaka Bariadi yenye kilometra 71.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, akiwa pale pale alitoa tamko kuhusiana na ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Simiyu. Tatu, alimaliza ngebe kuhusiana na mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Viktoria, matenki makubwa yakae wapi. Nne, alitoa maelekezo kuhusu gharama za ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa kwamba waziangalie kwa lengo za kuzipunguza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kwenda Maswa Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo kwamba ujenzi wa barabara ya kutoka Bariadi kwenda Maswa kilometra 49.7 utangazwe; na kweli naona kwenye Bajeti hii Wizara imezingatia hilo. Tukiwa Maswa aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa barabara inayoendelea sasa hivi kutoka Mwigumbi kuja Maswa. Haya ni mambo makubwa sana katika kufungua Ukanda huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Simiyu ni Mkoa mpya, Makao Makuu yake yako Bariadi. Tunahitaji tuunganishwe sisi na Mikoa jirani ya Singida na Arusha. Ndiyo maana Ilani ya Uchaguzi ya CCM inatamka, tufanye Upembizi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya kutoka Bariadi kwenda Kisesa - Mwandoya - Mwanhuzi mpaka Sibiti. Njia tunayoona sisi ni kupitia Mkalama kuja Iguguno. Kwa hiyo, tungependa sana hilli lioneokane. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mimi nimekuwa Mwanasheria Mkuu nikiwa Mbunge. Hii barabara ya kutoka Odeani - Mang'ola - Matala, Sibiti kwenda Mwanhuzi – Lalago – Mhunze – Kolandoto, imekuwa inaongeleta *story, story, story*. Kwa mwaka huu nakubaliana na Serikali kwa hayo waliyosema kwamba wamekamilisha upembizi yakinifu na usanifu wa kina. Mwaka kesho kama ikiendelea hivi mimi nitasema, maneno waache sasa waweke muziki. Hii barabara tunataka ijengwe. Kusema kweli ukishakamilisha usanifu huo, inakuwa sehemu ya kutoka Bariadi mpaka Mwanhuzi kwa sababu sehemu nyingine umeshamaliza. Kwa hiyo, waache maneno, waweke muziki. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukishafungua ukanda huo na kwa mapendekezo mengine ambayo tumeweza, barabara za kufunguliwa Ukanda wa Mkoa wa Simiyu, tutafungua maeneo hayo kiuchumi na kijamii. Sasa nilihangaikia sana hii Sheria ya Barabara kuweka vigezo vya namna ya kupandisha madaraja barabara hizi, basi tupate angalaau maamuzi kwa nchi mzima. Vigezo viro kwenye sheria hiyo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri waliangalie hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema ya nyumbani hayo, lakini nami kama Kiongozi wa Kitaifa niseme. Nchi hii ya Tanzania inafunguka kwa barabara. Angalia hizi barabara za kikanda, maeneo yote kuunganisha Tanzania na nchijirani tumefanya vizuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchijirani sehemu ambayo naiona ni muhimu kwetu sana na nimeiona kwa mbali kwenye hotuba hii ni Kasulu – Kibondo – Manyovu na Burundi. Pia naiona kwa mbali Sumbawanga – Matai – Kisesya – Sanga *Port* ni muhimu sana. Naiona kwa mbali pia, Bagamoyo – Saadani – Tanga – Horohoro – Lungalunga – Mombasa – Nairobi – Isiyolo – Moyale – *South Ethiopia*. Haya ndiyo mawazo tumekuwa nayo, maana upande wa Uganda - Sudan ya Kusini Arua - kuja mpaka Kyaka tayari tunaendelea. Tukikamilisha kazi inayoendelea ya kutoka Nyakanazi – Kakonko – Kasulu mpaka Kigoma na tukashuka sasa kutoka Uvinza tukaelekeea Mpanda - Stalike twende mpaka Kithi – Sumbawanga – Laela – Kikana – Tunduma unaiona nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nimesafiri, namwelewa rafiki yangu Mheshimiwa Zuberi aliyojasema, lakini nimeona humu, kutoka Masasi tukijenga barabara Masasi pale Nachingwea unaenda Nanganga, halafu Nanganga unaweza kushuka hivi kwenda Ruangwa. Haya ndiyo tunataka kuyaona humu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesafiri juzi pia, sikuamini, nimetoka Masasi nikaelekeea Mtambaswala, Mangaka kule nikatoka pale nikarudi kutoka Mangaka nikaelekeea Tunduru, barabara safi. Tukatoka pale tumekwenda mpaka Tunduru mpaka Namtumbo, Songea. Safi! Songea unakwenda mpaka Mbanga, sasa tunabaki sehemu ya Mbanga kwenda Mbamba Bay. Jamani, mambo yanafanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ambayo naitaka sana na nimeona kwa mbali, tukifungua Ukanda wa Kusini kwa chakula, angalieni ukitoka Kidatu uje Ifakara, piga hilo Lupilo uende mpaka Malinyi - Londo unakuja Lumecha,

Songea, unafungua yote. Ni ukanda tajiri sana. Tukiyafanya hayo tutakuwa tumeisaidia sana nchi hii. Naiona Tanzania ikifunguka. Kwa sababu ya muda, siwezi kuyasemea yanayoendelea Ukanda wa juu wa kwetu kule, lakini yamo kwenye taarifa hii. Naishukuru sana Serikali kwa kazi hii wanayoifanya. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa reli ya kat, kwa sababu tunatafuta mzigo utakaoweza kulipa reli hii, nadhani tuje tuiangalie kutoka Isaka kwenda Keza – Kigali - Msongoti. Pia Kaliua – Mpanda – Karema, maana mzigo wa *DRC* kwa Ziwa Tanganyika tungependa sana tuubebe huo. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sipendi kupigiwa kengele, Mheshimiwa Waziri akinisaidia; aah, nimalizie, sehemu moja ambayo nataka tuangalie pia, kutoka Mpemba pale kwenda Isongole upande wa Malawi tutakuwa tumekamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa hayo. (*Makofij*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Chenge. Nimemtaja Mheshimiwa Mbatia, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mhagama na Mheshimiwa Catherine Magige ajiandae.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipatia nafasi hii nami nitoe mchango wangu kwenye Wizara hii au hoja tuliyonayo mezani. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba nilikuwa na afya iliyotetereka kwa takriban miezi sita iliyopita, lakini sasa naendelea vizuri na ndiyo maana nimeweza kusimama kwenye Bunge hili Tukufu. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze moja kwa moja kwenye barabara za Jimbo la Vunjo. Mwaka 2016 Mheshimiwa Waziri aliniahidi kuhusu barabara ya Kawawa - Nduoni mpaka Marangu Mtoni. Barabara hii ina kilometra 29, imeshajengwa zaidi ya nusu kwa upande wa Kawawa –

Nduwoni kuna bado kilometa 4.8 na mwaka 2016 mliahidi kwamba kilometa hizo zitaingizwa kwenye Bajeti ya mwaka huu. Kwa bahati mbaya sana hizo kilometa 4.8 nimejaribu kukagua kila mahali japo sikuwa kwenye Kamati, mpaka sasa hazikuweza kuingizwa kwenye Bajeti ya mwaka huu. Naomba majibu sahihi, ahadi ya Mheshimiwa Waziri hii itatekelezwa vipi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya *Kilema Road* kwenda Hospitali, tunashukuru angalau zile kilometa mbili zimejengwa lakini hazijakamilika vizuri, ambapo zilikuwa ni eneo korofi sana. Ahadi ya Rais wakati wa uchaguzi aliahidi kwamba barabara ya Kilema kilometa 13 itajengwa yote kwa lami na siyo eneo lile ambalo ni korofi tu. Pia barabara ya Mabogini kwenda Kahe mpaka kutokea Chekereni ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Barabara za Himo Mjini ni ahadi za Mheshimiwa Rais, kwamba zote zitajengwa ili Mji Mdogo wa Himo uweze kufanana na maeneo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016 nilishauri, maeneo yenyeye milima au maeneo yenyeye miinuko kwa mfano Mkoa wa Kilimanjaro, barabara zinajengwa lakini sehemu ya kutolea maji (*drainage system*) na maji ni adui mkubwa wa barabara. Namna gani Wizara yake na Serikali za Mitaa wanashirikiana pamoja ili Serikali za Vijiji wawe wanasaafisha hiyo mitaro mara kwa mara? Kwa sababu wasipofanya hivyo, hili jukumu la Serikali Kuu, hawawezi kutekeleza wao wenyewe na mkikaa pamoja, tukishirikiana pamoja na Serikali za Mitaa wakahimiza hasa vijijini ili isafishwe hii mitaro barabara zitadumu zaidi, kwa sababu maji ni adui mkubwa wa barabara na uharibifu huu wa barabara kwa kiasi kikubwa tunazungumzia ujenzi wa barabara kitaalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia vizuri Mbunge aliyemaliza sasa hivi, Mheshimiwa Chenge. Ni namna gani tunafanya *maintenance* ya barabara? Namna gani kwenye mikataba yetu tuna-*include local component capacity basic* ya Wahandisi wetu ili hawa wakubwa wakishaondoka waweze ku-*maintain* barabara hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mikubwa kwa mfano ya reli ya kati ni namna gani tunaweka Wahandisi *local component* tuwanjengee uwezo wale waklondoka waweweze ku-maintain barabara hizo? Namna gani tunaiwezesha TANROADs? Nawapongeza sana TANROADs kwa kazi kubwa wanayofanya na hasa Mkoa wa Kilimanjaro, nawapongeza kweli kweli, wanafanya kazi nzuri ya kitaalam na ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Engineer* wa TANROAD wa Mkoa wa Kilimanjaro na timu yake anafanya kazi nzuri na *Ma-engineer* wote kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Ni namna gani tunawawezesha, tunawapa *capacity* ya kutosha ili waweweze kuhakikisha miundombinu hii inaendelea kuwepo? Ni namna gani sasa hivi tunajenga reli ya *standard gauge*? Ni namna gani tunaandaa wafanyabiashara na namna gani ya kupitisha mizigo kwenye reli ukillinganisha na kwenye barabara, kwa sababu uharibifu wa barabara hizi ambazo zimefunguka karibu nchi nzima, uharibifu wake unakwenda kwa kasi kubwa? Angalia mvua zilivyonyesha sasa hivi barabara zinavyoharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la *environmental impact assessment* ambalo kwa kiasi kikubwa nimeisoma kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri, sioni likiwekewa kipaumbele cha kutosha. Nitatoa Mfano ili nieleweke. Ukiangalia upanuzi wa *Airport* ya Dodoma, suala la *environmental impact assessment* lilizingatiwa kiasi gani? Angalia uharibifu mkubwa uliotokea kwa binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mwengine nieleweke. Barabara inayopita Serengeti iliyokuwa ijengwe, dunia ilipiga kelele kuhusu kusumbua wanyama wa Serengeti. Je, usumbufu wa binadamu ukoje? Miundombinu sawa ijengwe vizuri, lakini suala la kukuza utu na kuzingatia maadili ya uharibifu wa mazingira nao upewe kipaumbele cha kutosha, ambapo nikiangalia kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri, sioni suala la *environmental impact assessment* na *mitigation missions* zake ziko kubwa kiasi gani? Au

utazingatiwa kiasi gani ili miundombinu hii iendane sambamba na *inclusiveness* ya wote ambao ni watumiaji wa barabara hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Taifa letu la Tanzania, zipo kwenye *classification* mbalimbali zikiwepo barabara za Mkoa wa Kilimanjaro. Tusipozingatia kilimo cha matuta katika Mkoa wa Kilimanjaro, uharibifu wa udongo wakati wa mmomonyoko ambao ukija kwenye barabara unaharibu barabara hizo. Sasa ni namna gani sheria zetu, kanuni, tamaduni na mila zetu zinaweza kulinda barabara hizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipoweza kuzingatia tamaduni, tukawa ni *copy and paste* ilimradi tumeona mradi fulani huko Ujerumani au huko Japan tukauleta hapa kwetu, wakati *component* ya *maintenance* na kutunza miundombinu hii hatujaizingatia vya kutosha, tutapata matatizo makubwa sana mbele ya safari. Tutakuwa na miundombinu ambayo iko kwenye *class A*, lakini namna gani ya kui-*maintain* ibaki *class A* itakuwa ni shida ili ile ya *class B* iende kwenye *class A*, *class C* iweze ikafanya hivyo, lakini hapo unaweza kukuta ule uelewa wa ujenzi wa miundombinu tunaendelea kusema, hii ndio *class E* iende *class A*, wakati ya *class A* bado inaendelea kuwa na uharibifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia barabara inayotoka Morogoro kuja Dodoma, barabara zinazotoka Dar es Salaam kuja Dodoma, angalia barabara sasa zinazojengwa za Dar es Salaam ambayo ni maendeleo mazuri tu, lakini ni namna gani ya kuhifadhi barabara hizo, namna gani ya kuzingatia wale wote ambao watatumia barabara hiyo? Ninachozungumzia hapa, narudi kwenye *central education*; elimu kwa matumizi ya barabara, elimu kwa matengenezo ya barabara, elimu kwa ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia uwanja wa *Airport*. Nitatoa mfano nieleweke vizuri. Ukiangalia *Airport* ya *Amsterdam*, ndege zote zinazoruka pale, wakazi wa Aalsmeer wote imebidi wapewe *compensation* ya kutosha na ujenzi

wa nyumba zao za sasa hivi lazima uzingatie masuala ya *sound proof* ili waweze kuishi vizuri katika nyumba hizo. La sivyo, miaka 10 mpaka 20 ijayo, japo tunazingatia kwenye miundombinu, tusipofikiri kwa mapana kitaalam, tutapata shida kwa ajili ya kutokutoa haki kwa uhalsia wa binadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujue leo hii duniani, uharibifu mkubwa zaidi ya asilimia 96 unafanywa na binadamu. Sasa kama unafanywa na binadamu, zile *known-known risk, known-unknown risk and unknown-unknown risk* ambazo ni *act of God*; lakini kuna nyingi hapa ambazo tunasema ni *act of God while is not an act of God!* Ni uzembe wetu tu sisi binadamu, ndiyo tunaosababisha mambo ya mafuriko, hatuna mitaro mizuri na matatizo mengine. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri lakini namwomba, chonde chonde!

Mheshimiwa Naibu Spika, nihitimishe kwa kusema tena kwamba barabara za Bunju ambazo Mheshimiwa Waziri aliahidi mwaka 2016 ahakikishe zinapewa kipaumbele ili tuweze tukazungumza vizuri na ukizingatia kwamba mimi ni *Shadow Minister* wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyezi Mungu akubariki, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Magige na Mheshimiwa George Lubeleje ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi na nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia katika maeneo makubwa mawili na iwapo muda utaniruhusu, nitaongeza sehemu ya tatu. Kwanza kabisa, niungane na Waheshimiwa

Wabunge wote ambao wamempongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya kwa kupitia Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Nisingependa kurudia maneno mazuri ambayo Wabunge wengi wamesema kuhusu kazi nzuri zilizofanyika, Tanzania sasa imeunganishwa kwa barabara nyingi, inaunganishwa kwa reli, lakini inaunganishwa kwa anga. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kutambua mchango mkubwa sana wa Mawaziri kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais na kesho sisi wadau wa Mkoa wa Ruvuma tutakuwa pale Songea tarehe 30 kupokea ndege aina ya *Bombardier* ikitua kwa mara ya kwanza katika Mji wa Songea. Kwa hiyo, ni kazi nzuri ya Wizara hii, nachukua nafasi hii kuipongeza sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo matatu ambayo napenda niishauri Wizara au Serikali katika ujumla wake. Eneo la kwanza, hii miradi tunayowekeza ni mikubwa sana. Wizara ya Nishati inawekeza katika miradi mikubwa sana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano nao wanawekeza katika miradi mikubwa sana. Wizara hizi mbili, ili miradi hii inayowekezwa iweze kuwa na tija, ni muhimu sana hizi Wizara mbili zikafanya kazi kwa ukaribu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua sisi Jimbo la Madaba tunapakana na eneo lenye mradi mkubwa sana, tunaita *Flagship Projects* pale Liganga na Mchuchuma. Huu ni mradi mkubwa sana na ni mradi ambao umezungumziwa kwanza kabisa na Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, baadaye akafuatia Mheshimiwa Waziri Jenister Mhagama. Mimi leo ni Mbunge wa tatu katika Bunge lako kuzungumzia mradi huu kutoka eneo hilo hilo la Jimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu umechukua muda mrefu sana, lakini sasa mradi huu una matumaini makubwa ya kuanza; na taratibu zote za kuanza zimekamilika na tutaisikia kwenye Wizara wa Nishati na Madini watakapowakilisha. Kinachosikitisha ni kwamba hakuna maandalizi ya kutosha kuhakikisha kwamba barabara

zinazokwenda kwenye mradi huu mkubwa zinakamilika. Huwezi kuzungumzia Mradi wa Lingaganga na Mchuchuma bila kuzungumzia barabara inayotoka Madaba kwenda Mkiyu - Linganga. Utawezaje kusafirisha mitambo kwenda katika eneo la mradi? Utawezaje kuvuna makaa na chuma kutoka katika eneo la mradi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, yawezekana Wizara kwa sababu moja au nyngine na yawezekana ni sababu za msingi kwamba hawajaweka bajeti ya kutosha ya kukamilisha barabara hii kwa kiwango cha lami, nawaomba Wizara, kama kweli tupo *serious* na kama kweli Miradi ya Mchuchuma na Linganga inaanza, lazima barabara ya Madaba - Mkiyu ikamilike. La sivyo, tutaiingiza Serikali kwenye hasara kubwa sana. Mradi upo tayari kuanza lakini barabara ya kwenda kwenye mradi haipo. Hatuwezi kufanikiwa tusipoweza kuunganisha haya mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili linahusu Mfuko wa Barabara Vijiini. TAMISEMI wanapata asilimia 30 ya fedha zote zinazokusanya kwa ajili ya Mfuko wa Barabara na asilimia 60 inabaki kwa *TANROADs* kwa ajili ya kushughulikia barabara za mikoa na hii asilimia 30 inakwenda TAMISEMI na inakuwa *translated* kwenye kutekeleza miradi ya barabara ndani ya Halmashauri. TAMISEMI wanakuja na wazo kwamba tuwe na *Rural Road Agency*, hili wazo ukiliangalia kwa haraka, linaonekana kama ni zuri na lenye tija, lakini niliombwa *ni-draw attention* ya TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano. Kwanza lazima tujue kwamba kama kumekuwa na ufanisi katika ngazi za Halmashauri zetu, ni kwa sababu wale wanaofanya kazi katika Halmashauri za Wilaya wapo *accountable* moja kwa moja kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hiyo *sense of accountability* ndio inayofanya Halmashauri zetu ziwe na tija (*efficiency*) kwa sababu anayesimamia miradi katika Halmashauri ni Diwani ambaye yupo karibu na wananchi, anajua matatizo ya wananchi na anawajibika kwa wananchi. *So sense of accountability* imeleta tija sana katika utekelezaji wa miradi katika ngazi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukilinganisha na taasisi au *agency* mbalimbali zinazoundwa zenyé hadhi ya Kitaifa *sense of accountability* haiwezi kuwa sawa. Halmashauri *sense* ya *accountability* ni kubwa zaidi. Naomba sana, *tusi-attempt* kutengeza huu Mfuko wa Barabara Vijijini, isipokuwa fedha hizi zigawanywe kwa uwiano sawa katika Halmashauri na ziendelee kusimamiwa na Halmashauri za Wilaya zetu. Italeta tija zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine najua *TANROADS* hakuna urasimu sana, lakini taasisi yoyote yenye muundo ina urasimu. Halmashauri zina urasimu, *TANROADS* wana urasimu na Taasisi yoyote ina urasimu kwa sababu ya muundo wake. Sasa ukilinganisha *level* ya urasimu katika Taasisi za Kitaifa na Halmashauri, Halmashauri *level* ya urasimu ipo chini sana. Kwa hiyo, tutumie hiyo fursa sasa kupeleka hizi fedha zikafanye kazi kwa tija katika Halmashauri, tukizilacha kwenye ngazi hizo za juu hatutapata ufanisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningeweza kusema, kwangu mimi kufikiria kutengeneza hii tunayoita Mfuko wa Barabara Vijijini kwa maana ya *Rural Road Agency*, katika *context* ile ile na mfananisho ule ule wa *TANROADS* ni jaribio la kudhoofisha dhana ya ugatuvi wa madaraka. Kwa hiyo, naionba sana Serikali ifanye *study* upya ya *efficiency* za Halmashauri zetu ukilinganisha na *efficiency* ya *agency* mbalimbali zenyé hadhi ya Kitaifa ili kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kama muda unaniruhusu, nichangie tu kwamba ukisoma katika hiki kitabu unaona kumekuwa na shida kidogo katika *allocations* za *projects*. Ipo mikoa ambayo imepata miradi mingi zaidi kuliko mingine. Sababu zinaweza zikawa za msingi kwa maana ya mahitaji halisi, lakini ni vizuri sasa niiombe Serikali iangalie *priorities* nyininge pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tumewekeza fedha nydingi sana kujenga Jiji la Dar es Salaam ambalo lina wananchi milioni tatu na zaidi kidogo...

MBUNGE FULANI: Ni zaidi.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Wanakaribia milioni tano, lakini tukumbuke pia mahitaji katika maeneo mengine ni muhimu pia. Naiomba Serikali sasa iangalie, ifanye *rationalization* ya miradi yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile muda hauniruhusu, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Catherine Magige, atafuatiwa na Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Richard Ndasa ajandae.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hili ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mchango wangu nitauelekeza moja kwa moja katika Shirika letu la Ndege la *ATCL*. Katika vipindi viwili vya 2016/2017 na mwaka 2017/2018, tumeona imetengwa karibu shilingi trioni moja kwa ajili ya *ATCL* ambapo kwa kila kipindi itakuwa shilingi bilioni 500. Uwekezaji huu ni mkubwa mno na unahitaji umakini wa hali ya juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili *ATCL* ipate faida, ni lazima twende sambamba na uwekezaji katika mambo makuu mawili. Jambo la kwanza ni uwekezaji wa ndege kama hivi tunavyofanya sasa hivi; jambo la pili ni kuwekeza katika uendeshaji wa *ATCL*, yaani mtaji wa kazi na rasilimali watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ndege, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutuletea ndege za kisasa na ametuhakikishia ni salama kabisa. Itakapofika mwaka 2020 kama siyo 2019 zitakuwa ndege saba. Nampongeza sana Rais wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi mkubwa unakuja kwenye uwekezaji katika uendeshaji wa *ATCL*. Tumezoea

tukinunua tu ndege tunaacha, tunajua tayari tumeshanunua ndege bila kuwekeza. Tunategemea kupata faida, lakini hatuwezi kupata faida tu bila kuiwezesha *ATCL* iweze kuendesha biashara ya ndege. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunajua kuwa *ATCL* ilibaki jina tu, haikuwa inafanya vizuri, ndege zake zilikuwa hazieleweki, lakini sasa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kaanza kururudishia *ATCL* mpya. Vilevile haikuwa na rasilimali watu na mtaji; naongelea kwa upande wa kujidoresha. Kwa hiyo, lazima tuisaidie *ATCL* kujidoresha ili iwe kibiashara zaidi. Tunajua *ATCL* ilikuwa ni jina tu au Kampuni isiyokuwa na rasilimali watu wala chochote; tunajua kwa sasa hivi *ATCL* kitu ambacho inahitaji ni *working capital* na siyo *startup cost*. Ni wazi kwamba bila kuiwezesha *ATCL* haitaweza kujidoresha yewenye na haitaweza kujidoresha kibiashara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji uliofanywa na Serikali ni mkubwa mno, lazima uambatane na uwekezaji wa kujidoresha *ATCL* ili iweze kutoa huduma nzuri. Tumeanza kuona mabadiliko ya *ATCL*, tumeona safari hazikatishwi, tumeona inaenda vizuri sana. Vilevile naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutuletea Mtendaji anayeweza hii nafasi, ana uzoefu. Ni muda mfupi sana naweza nikasema ametuonyesha *wonders*. Naomba sana tum-support Mtendaji huyu Ledislaus Matindi kwa kazi kubwa anayofanya, ana uzoefu na anajua changamoto za *ATCL*. Lazima tuunge juhudhi za Serikali mkono na tuwe wazalendo kwa nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona Mheshimiwa Rais ameteua Bodi nzuri; lazima tuhakikishe Bodi na Menejimenti wamejikita zaidi kuisaidia *ATCL* ijiendeshwe kibiashara na siyo kukaa tu kusema kuwa ni Shirika la Serikali. Hatuna wasiwasi na matumizi ya fedha kwa sababu ya uongozi uliopo sasa hivi tunauamini, tunajua hata tukiwawezesha mapato yataenda vizuri, fedha zitatumika kama zilivyokusudiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tujifunze kwa wenzetu ambao waliweza kuendelea kama Shirika la Ndege la Ethiopia. Serikali yao iliwayezesha Ethiopia na waliendelea vizuri, ilivumilia na walijipanga vizuri. Walianza mambo yao ya ndege mwaka 1945, lakini walikuja kupata faida 1990 walikuwa wavumilivu, waliwekeza katika mishahara, matangazo na hadi sasa hivi inajиndesha kibashara. Tusitegemee ATCL itaanza tu, tayari tupate faida asilimia 100, hapana. Lazima kama sisi Serikali kuiwezesha ili iweze kujиndesha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya Ethiopia yalikuwa na uvumilivu, mkakati na nidhamu. Uvumilivu ulisaidia sana mpaka kufika 1990 ukiangalia ukiangalia kuanzia mwaka 1945, ni kipindi kirefu sana, kwa hiyo, kilihitaji uvumilivu. Nasi tukifanya hivyo, Serikali ikiwawezesha ATCL nina uhakika kabisa tutafika na tutaweza kuendelea vizuri na ATCL. Kwa hiyo, naomba Tanzania tui-support ATCL. Mpaka sasa hivi tumeona inaenda vizuri, ni muda mchache sana lakini imefanya vizuri na wote tumekubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuonyeshe uzalendo kwenye ndege zetu. Tumeona kuna ndege ndogo ambazo zinafanya safari kwenye miji mikubwa, kwenye barabara kuu ambazo zingeweza kufanya ndege zetu. Naomba pia Serikali iliangalie hili tumetumia kodi za wananchi. Ndege ndogo zinaweza kupewa *trip* nyinye kwenda sehemu ambazo hizi ndege zetu za ATCL haziwezi zikafika. Zenyewe zikaenda zikawaachia njia ATCL.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumeona kuna tabia moja kuwa ndege inapokuwa na nguvu kuna baadhi ya ndege zinakuja zinawakwamisha, zinaua kabisa. Tumeona ndege tayari ambazo tayari zilikuwa zinafanya vizuri zimekufa, lakini tusikubali hili kwa ndege zetu ambazo zimenunuliwa kwa kodi ya wananchi. Tumeona ATCL inaweza ikaenda Mwanza labda kwa kiasi fulani lakini ndege nyinye ikaenda ikashusha kabisa. Hao ndio wauaji wakuu wa soko letu, Watanzania tusikubali, tuwe wazalendo wa nchi yetu. Mheshimiwa Waziri

naomba uje unijibu wakati unajibu hili la ndege nyingine kuja kutuharibia biashara huku tukijua tunatumia kodi za wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tusipokuwa makini tunaweza tukajikuta *ATCL* inakufa, tukaishia kwenye madeni yasiyolipika. Kwa hiyo, tuunge mkono juhudzi za Mheshimiwa Rais na nia yake nzuri ya kufufua Shirika letu la ndege ili lije kufanya vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie na uwanja wangu wa Ndege wa *Arusha Airport*. Kiwanja cha Ndege cha *Arusha Airport*, njia ya kurukia ni fupi, hali inayopelekea ndege za kati na kubwa kushindwa kutua, ikiwemo *ATCL*, inashindwa kuruka. Kwa hiyo, inabidi wakatize *trip* za kwenda Arusha. Ukizingatia Arusha ni Jiji lenye biashara, Jiji la utalii, ni kitovu cha utalii ambapo tungeweza kuiingizia Serikali mapato mengi sana kutokana na utalii. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wakati ananijibu, naomba aniambie ana mpango gani na Kiwanja cha Ndege cha Kisongo cha Arusha ili nasi wana-Arusha tuweze kupata hizo ndege tuweze kuiingizia Serikali mapato. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naomba Waziri aniambie ameandardaa kiasi gani cha uwekezaji kama mtaji na rasilimali watu kuwekeza kwa ajili ya *ATCL* iweze kujlendesha yenyewe kibashara? Siyo kuwekeza tu kwenye ndege tukasahau kuwa inahitaji na yenyewe kujwekeza? Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa George Lubeleje, atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Mussa Zungu ajiandae.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie Wizara hii. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *EngineerMfugale* ambaye ni *CEO* wa *TANROADS* na vilevile nimpongeze *Manager* wa *TANROAD* wa Mkoa wangu kwa kazi nzuri wanazofanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitazungumzia barabara moja tu; na hii barabara ni ya kutoka Mbande - Kongwa kwenda Mpwapwa kujengwa kwa kiwango cha lami. Nimeanza kudai barabara hii tangu mwaka 1984. Nimekuwa Diwani miaka 15; Mwenyekiti wa Halmashauri Wilaya ya Mpwapwa miaka 15, nadai barabara hii. Nimeanza Ubunge mwaka 1990 nikiwa kijana, wakati huo nachana *afro*; ukienda Ofisi ya Makumbusho Dar es Salaam, utakuta pitcha yangu pale. Sasa mpaka nafika umri huu, nadai barabara. Sasa umri wangu ni mkubwa, tangu kijana nadai barabara hii, lakini Serikali hawanionei huruma, kwa nini? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa Mbunge miaka 20; 2010 - 2015, nikaenda likizo miaka mitano; sasa nimerejea tena kwa matumaini kwamba wananchi wa Mpwapwa sasa hii barabara itatengenezwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakuomba sana ndugu yangu, kijana wangu, sikiliza kilio cha wananchi wa Mpwapwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpwapwa ni Wilaya ya zamani, tangu mwaka 1905. Sasa umri wake ni miaka 100. Kwa hiyo, Mpwapwa ina sifa zote za kupata barabara ya lami. Ni kilomita 50 zimebak; Mbande - Kongwa *Junction*; Kongwa *Junction* mpaka Kongwa, kilomita tano mmeshajenga tayari, bado kilomita 50. Mbande *junction* ya Kongwa na *junction* Kongwa kwenda Mpwapwa kilomita 46. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, Eng. Mfugale unanisikia, wewe ndio *CEO* wa *TANROADs*, mnisaidie ndugu zangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpwapwa kuna uchumi. Hii barabara ndio inayounganisha Majimbo matatu; Jimbo la Mheshimiwa Simbachawene, Waziri wa TAMISEMI. Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Jimbo la Kongwa na Mheshimiwa Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa. Hii barabara ina umuhimu kwa uchumi na maendeleo ya Wilaya ya Mpwapwa. Hii barabara Mheshimiwa Waziri inapitisha magari zaidi ya 150 kutoka Mbande kwenda Mpwapwa; magari makubwa ya mizigo pamoja na magari madogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana ndugu yangu, leo nilitamani nilie, lakini namsamehe kwa leo, maana mtu mzima kulia siyo jambo jema. Leo itakuwa ni mara yangu ya mwisho kuomba barabara. Nitakuwa nakaa kimya tu naisikiliza Serikali yangu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpwapwa kuna taasisi zaidi ya nane; kuna taasisi ya utafiti wa Mifugo ya Kitaifa, kuna Chuo cha Mifugo Mpwapwa, Chuo cha Maafisa wa Afya na Chuo cha Ualimu Mpwapwa. Mpwapwa pia kuna mabonde mazuri sana ya kilimo; Bonde la Malolo, Lumuma, Matomondo na Bonde la Chamkoroma. Mpwapwa vile vile ina madini aina ya *ruby* katika Kijiji cha Uinza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *CEO* Mfugale, mnisikilizze kilio changu. Wananchi wa Mpwapwa wananipenda na ndiyo maana wananiresha Bungeni. Sasa nitakuja kuwaachia kumbukumbu gani jamani ndugu zangu?

MBUNGE FULANI: Lia!

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Wamenirejesha kwa matumaini kwamba safari hii Serikali yangu sikivu itasikia kilio changu, watapata barabara ya lami. Kwa hiyo, nawaomba sana ndugu zangu, viongozi wakubwa watatu; Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa TAMISEMI; hivi Mheshimiwa Waziri huwezi kuwaonea huruma hata wakubwa wenzako hawa kweli! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nimesema nazungumzia hii barabara, Mheshimiwa Waziri amenisikia kilio changu, Serikali yangu ni sikivu, najua wananchi wa Mpwapwa wanansikiliza na safari hii kwa kweli nina matumaini makubwa kabisa kwa baraka za Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, namshukuru sana Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri na *CEO*

Engineer Mfugale, Katibu Mkuu na Viongozi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri. Ahsanteni sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje. Naomba uzime *microphone* yako. Mheshimiwa Richard Ndassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani na Mheshimiwa Ester Bulaya ajienda.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nianze kwa kukushukuru wewe kwa nafasi hii, lakini namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote pamoja na taasisi chini ya Wizara kwa kweli kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Kuna msemo mmoja wa Kiswahili unasema ukiona adui yako anakupongeza kwa jambo lako, achana nalo; lakini ukiona adui yako kwa jambo lako anakupigia makofi, jitazame mara mbili. Kwa hiyo, wenzetu kila jambo jema linalofanywa wao hawakubali. Namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa yale mazuri ambayo mnayafanya na ni mengi tu, kazeni buti, endeleeni, wala msitishwe na hizo kelele ambazo zinatokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri, najua amevaa kiatu cha Mheshimiwa Rais kwa sababu Mheshimiwa Rais ndiye alikuwa Waziri wa Ujenzi; na kiatu hicho naona kinakufaa sana. Naomba, ipo barabara ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kutoka Isandula - Magu inakwenda Bukwimba - Ngudu kwenda Hungumarwa. Ni ahadi! Mwaka 2016 mlisema kwamba mmetenga pesa kwa ajili ya usanifu, sasa leo sijaona humu, nami kama *Senator* hatupendi sana kupiga makelele na hasa ukizingatia kwamba Mheshimiwa Waziri wa Wizara ni mtu msikivu na mwelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne akiwa na Rais wa Awamu ya Tano, walikuja kufungua Daraja la Mto Simiyu, Maligisu. Vingunge wote wa Wizara walifika pale Maligisu na Mheshimiwa Rais aliahidi

kwamba ile *approach* ya mita 50 upande huu na mita 50 upande huu itajengwa kwa kiwango cha lami. Tena kama natania, ili na fisi nao waje wapite kwenye lami. Hyo ilikuwa mwaka 2015. Mheshimiwa Waziri, maagizo ya Mheshimiwa Rais, mita hamsini hamsini, hebu tusimwangushe Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kubwa, Mheshimiwa Waziri, anazo taasisi zaidi ya 30 zilizo chini yake. Taasisi hizi ni kioo kwa nchi yetu na Taasisi hizi ni uchumi kwa nchi yetu. Nawaomba kwa sababu bahati nzuri ma-*CEO* wapo hapa, Wakurugenzi wapo kwa maana ya Wenye viti. Kwa taasisi hizi, kila *CEO*, Mwenyekiti kwenye eneo lake kwa ajili ya kuisaidia Serikali na kwa sababu tunaomba pesa nydingi, pesa hizi tunazitegemea kutoka kwenye hizi taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana viongozi hawa, yale makubaliano ambayo inawezekana Mheshimiwa Waziri tutaweka na utaratibu mmoja mzuri, nafikiri wa kupimana, kwa sababu ile *business as usual*, tukienda na utaratibu huo kwa taasisi zetu hizi, tunaweza tukafika mahali tukashindwa kufikia yale malengo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na viongozi wa taasisi zilizo chini yako, zifanye kazi ili kusudi matokeo makubwa tuyaone kwa kuisaidia nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, namwomba Mheshimiwa Waziri upande wa Wakala kwa Mama Kijazi pale, *TMA*. Eneo hili ni eneo zuri sana kama watapatiwa vifaa na wataalam wa kutosha. *TMA* hii igawanyike kikanda; Kanda ya Ziwa, (mimi nazungumzia Kanda ya Ziwa, huku kwinge baadaye) ili kusudi waweze kutambua na kuwashauri wakulima, maana yake sasa hivi kuna ubashiri, lakini tutoke kwenye ubashiri tusogee kwenye uhalisia kwamba mvua zitanyesha kesho saa fulani. Jamani wale wavuvi kesho kutwa msiende ziwani kwa sababu kuna

upepo mkali. Sasa ili wafanye hivyo ni lazima wawe na vifaa vya kutosha vinavyoweza kuhimili badala ya kwenda kupiga ramli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, barabara ya Nyanguge - Musoma, Mwanza -Shinyanga *Boardertumekuwa tukizitengea pesa nyingi kila mwaka*. Hivi hakuna utaratibu mzuri wa kuzifumua hizo barabara zikajengwa upya? Maana yake kila mwaka fedha inatengwa. Namshauri Mheshimiwa Waziri, hebu walitazame hili kusudi barabara zetu hizi ambazo kiuchumi na kijamii zina faida kubwa sana kwa Kanda ya Ziwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, nashukuru tunatengeneza hii reli ya kati. Sasa nasikia na namwomba *CEO* wa *TRL*, kama treni itatoka Dar es Salaam lakini inakuja Shinyanga, inafika Malampaka, halafu haisimami katikati hapa pote inakwenda kusimama Mwanza; nashauri treni hii isimame Bukwimba Stesheni, panajulikana! Panaeleweka! Kadogosa; siwezi kusema Kisukuma lakini nakuomba treni isimame Bukwimba Stesheni, miundombinu ipo ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kumekuwa na malalamiko mengi sana kuhusu upoteaji wa makontena. Hebu wataalam wako wakae waangalie namna nzuri zaidi; hivi *NASACO*, Wakala wa Meli, nasema mkae mwangalie; Wakala wa Meli wa wakati ule *NASACO*, tulikosea wapi? Kwa nini tuliwaondoa? Kwa sababu haiwezekani mizigo ikawa inapotea, makontena hayajulikani, yanaingia makontena na taarifa hatuna. Naomba kama inawezekana *NASACO* iangaliwe upya ili kusudi tuweze kurejesha heshima ya nchi yetu hasa upande wa mizigo inayokwenda nje na ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena lakini naomba kusitiza, taasisi hizi ni kioo cha nchi yetu; *TPA* ni kioo na uchumi, *ATCL*, *TRL* na mengine, ni kioo kwa uchumi wa nchi yetu. Toeni huduma, fanyeni biashara lakini kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii na naunga mkono hoja. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa David Ernest Silinde ajiandae.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwiningi wa Rehema na mwiningi wa Utukufu aliyenijalia kusimama hapa siku hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii nami kuchangia Wizara ya Miundombinu. Nianze na usafiri wa anga. Nachukua nafasi hii kumpongeza sana Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ya kusimamia kikamilifu utekelezaji wa ilani, lakini pia kuwezesha ndege hizi sasa kuweza kufanya usafiri ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa leo nikiwa nina furaha sana na niwashirikishe Wabunge wenzangu kwamba keshokutwa tarehe 30 ni siku maalum kabisa ambapo ndege aina ya *bombardier* itaanza safari zake kutoka Dar es Salaam kuelekea Songea. Naishukuru sana Serikali yangu, kitu kama hiki kilikuwa ni ndoto, lakini kwa kudra za Mwenyezi Mungu na kwa jitihada za Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli imewezekana kwa kipindi kifupi cha mwaka mmoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye barabara. Kuna barabara ambayo ina changamoto kubwa sana. Barabara hii ni barabara yenye urefu wa kilometra 66 inayotoka Mbanga kwenda *Mbamba Bay*. Naomba barabara hii sasa ianze kutengenezwa kwa sababu ina muda mrefu, imekuwa katika mpango lakini pia tayari upembuzi yakinifu umeshafanyika, ianze kutengenezwa sasa kwa kipindi hiki cha mwaka 2017/2018 ili kuweza kuunganisha mkoa mzima na hata kufikia kule katika Ziwa letu la Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo sasa tutakuwa tumeshawezesha ile *Mtwara Corridor* kuwa tayari imeungwa kutoka Mtwara mpaka kufika *Mbamba Bay* ambapo sasa tunaweza tukasafirisha bidhaa mbalimbali kwa kutumia usafiri wa maji kutoka Mtwara na hata kupeleka mpaka Malawi. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niende kwenye barabara ya Likuyufusi. Barabara ya Likuyufusi – Mkenda ni barabara yenye urefu wa kilometra 24 na ni barabara ambayo inaunganisha Mkoa wa Ruvuma na nchi yetu ya Msumbiji; kwa maana ya nchi ya Msumbiji na nchi yetu ya Tanzania. Ni barabara ambayo ikishajengwa kwa kiwango cha lami, itainua uchumi wetu wa Tanzania kwa kuunganisha mipaka hii miwili na kufanya biashara kama nchi marafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende pia kwenye barabara ya Kitahi – Lituhi – *Mbamba Bay*. Hii barabara imekuwa ikipigiwa kelele sana, lakini kwa masikitiko makubwa, sijaona ikitengewa pesa kwa kipindi cha mwaka huu 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inasikitisha sana na hii ni barabara muhimu ambayo kimsingi kama mnasikia makaa ya mawe yanayochimbwa katika Mkoa wa Ruvuma, basi barabara hii ni ile inayotoka Kitahi kwenda mpaka kwenye yale machimbo na kufikia Lituhi na hatimaye kwenda kuunganisha mpaka *Mbamba Bay*; inapita kwenye uwanda pembezoni mwa Ziwa Nyasa mpaka kufika *Mbamba Bay*. *Mbamba Bay* ni mahali ambapo tayari sasa hivi kumeshakuwa na uwekezaji mkubwa wa mambo ya utalii, lakini nashangaa hii barabara haiunganishwi hata kuweza kuwezesha watalii kuweza kufika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ina umuhimu mkubwa na ukizingatia kwamba magari makubwa yanayokwenda kuchukua makaa ya mawe kule katika eneo lile linalochimbwa makaa ya mawe; ni magari ambayo yanatimua vumbi kiasi ambacho wananchi wanaoishi pembezoni mwa zile barabara tayari asilimia kubwa

wanaathirika kutokana na zile vumbi, wanapata maradhi ya aina mbalimbali, lakini pia inachelewesha hata namna ya kutoa makaa ya mawe na kupeleka labda Mtwara kule ambako huyu mwekezaji ambaye anazalisha *cement* kwa wingi anachukua makaa ya mawe kule. Siyo huko tu, viwanda vyetu vingi sasa hivi vinatumia makaa ya mawe. Kwa hiyo, barabara ile ni muhimu ili kuweza kurahisisha uchumi wetu tunaoutarajia; uchumi wa kati kufikia mwaka 2025. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara nyininge ya Lumecha – Londo. Barabara hii inaunganisha Mkoa wa Ruvuma na Morogoro. Barabara hii toka tumeanza kuiimba, ni muda mrefu na sijaona kama imetengewa pesa. Namwomba Mheshimiwa Waziri, tafadhali sana naomba atenge pesa kwa ajili ya kuunganisha hii barabara inayotoka Lumecha hatimaye kwenda Londo, Mkoa wa Morogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ambayo inatoka Mtwara Pachani kuelekea Narasi. Barabara hii kwa kweli wanasema hivi, mtu naweza akasahau kwake, akapata sungura wa kugawa, akagawia maeneo mengine akasahau kwake. Namwona kabisa kaka yangu Mheshimiwa Ngonyani Naibu Waziri wa Miundombinu amesahau; na leo nimeona nisimame hapa niisemee. Barabara hii iko katika Jimbo lake lakini naona kama ameisahau. Naomba Mheshimiwa Waziri tafadhali juu ya tafadhali, naomba utusaidie hii barabara ili iweze kutengenezwa kwa kiwango cha lami iweze kusaidia wananchi wa Namtumbo lakini pia na wananchi wa Tunduru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii imeweka changamoto nyangi sana kiasi ambacho akinamama wengi wanaopata shida za namna ya kujifungua kwa kweli siku ya uwasilishi hapa wa Wizara ya Afya, jamani nitawaletea na picha ili mwone wanawake wa Namtumbo wanavyopata shida hasa maeneo ya kule pembezoni kuelekea Namtumbo

na kuunganisha na Tunduru. Wanapata shida kubwa sana kiasi ambacho wanabebwa mpaka kwenye matenga, barabara ni shida, magari hayawezi kwenda huko. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri barabara hii. Naomba sana Mheshimiwa Waziri amsaidie ndugu yake huyo Naibu Waziri aliyeko hapo ili aweze kupata hii barabara. Barabara hii ina changamoto kubwa sana; akina mama wanapoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hebu siku moja hawa wanaume na wenyewe wangeonjeshwa wakaona uchungu wa kuzaa, ndiyo pale wangeweza kujali na kuthamini hata wakaona umuhimu kwa barabara ambazo tunaziomba kwa machungu waweze kutuunganishia. Akinamama wanapoteza maisha! Nasikia uchungu sana, natamani kulia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ambayo inatoka Lingusenguse kuelekea Tunduru, nayo ni ya Mheshimiwa Naibu Waziri katika Jimbo lake. Anashindwa kusema, mimi naona nimsemee hapa kwa sababu yeye yuko hapo. Naomba umsaidle hii barabara pia ina changamoto kubwa. Tafadhalii juu ya tafadhalii, tusaidieni, wanawake wa Namtumbo wanapoteza maisha, wanawake wa Tunduru wanapoteza maisha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niende kwenye barabara ya Nangombo – Chiwindi yenye urefu wa kilometra 19. Barabara hii ni barabara ambayo iko kwa dada yangu Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya*, anaafuatilia pole pole, lakini mimi leo nimesimama hapa kindakindaki nimsaidie kumsemea mwanamke mwenzangu. Barabara hii nayo ina changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba barabara hizi nilizotitaja hapa zilizopo ndani ya Mkoa wa Ruvuma, endapo zitatengewa fedha, katu hutaniona nikisimama hapa nikiongelea barabara tena katika Mkoa wa Ruvuma. Kwa

maana moja ama nyingine, tutakuwa tumemaliza matatizo ya barabara katika Mkoa wa Ruvuma. Naomba tafadhalii sana mwaka huu wa fedha muweze kutenga fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia barabara hii niliyosema ya Kitahi – Lituhi, Mheshimiwa Waziri kama hataitengea fedha atakapokuja ku-*wind up* hapa, haki ya Mungu nitashika shilingi. Nimhakikishie kabisa nitashika shilingi kwa sababu ni barabara ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa David Ernest Silinde na Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela ajiandae.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami kwa moyo mkunjufu, napongeza kwanza hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa yale mambo mazuri ambayo yameandikwa na tumeendelea kuyasisitiza, Serikali myachukue myafanyie kazi maana kazi yetu ni kuwashauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napongeza Majiji yote na Halmashauri zote zinazoongozwa na Upinzani. Mbali ya ufinyu wa fedha lakini wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana na hiyo inaonesha ni namna gani Watanzania hawakukosea kutupa kura na tunawahakikishia wakiendelea kutupa kura, haya mambo ya kuwaza mawasiliano ya simu, hakuna. Sisi tutawaza *flyovers* zenye nafasi na *underground*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, sasa naomba niende katika Jimbo langu la Bunda. Kwanza, natambua kazi nzuri ambayo inafanywa na TANROADs Mkoa wa Mara, lakini pia nashukuru kwa baadhi ya barabara kwenye Jimbo langu ambalo tayari zimeshapandishwa hadhi, ila tu Mheshimiwa Waziri najua yeye ni mchapakazi na alikuja Bunda. Kuna barabara ambazo hazijapandishwa hadhi katika mwaka huu wa fedha, *please*, naomba

mwakani ziangaliwe ziweze kupandishwa hadhi. Naomba sana, kwa sababu bado Halmashauri yetu ni changa, inahitaji kulelewa na inahitaji *support* yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hiyo ni Sazira – Misisi – Kitaramanka, barabara ya Bitaraguru – Kiwasi na barabara nyingine zote hizo tunahitaji zipandishwe hadhi ili ziweze kuitika ili akinamama wanapokwenda kujifungua waweze kuita katika miundombinu iliyo salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie Mfuko wa Barabara. Katika Mamlaka ya Mji wa Bunda, mwaka 2016 tulitengewa shilingi milioni 710 mpaka sasa hivi zilizofika ni shilingi milioni 73 tu. Shilingi milioni 700 ndizo zilizokuwa zimetengwa, zilizofika ni shilingi milioni 73, tutazifanyia nini jamanii?

MBUNGE FULANI: *Very bad!*

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni asilimia ngapi hiyo? Kumi kati ya 100! *Please!* Halmashauri yetu ya Bunda ni changa; na ukizingatia kwenye hizi Halmashauri, vyanzo vya mapato Serikali Kuu mmevichukua ambavyo vingesaidia hizi Halmashauri changa kujitahidi angalau basi kukarabati hizi barabara. Hamkleta pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANROADs* Mkao wa Mara na wenyewe ni Killio. Mkao wa Mara barabara zinazokarabatiwa sasa hivi ni vyanzo vya ndani. Kwenye RCC iliypita, mpaka tuliunda Kamati ndogo kuja Wizarani kudai pesa. Miaka mitatu mfululizo mnachelewa kutupa pesa, Mkao wa Mara tumewakosea nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nazungumzia Majimbo yote; na huu mkao una historia katika kutafuta uhuru wa nchi yetu. Mara unazungumzia Baba wa Taifa, lakini leo hii Mkao wa Mara, Makao Makuu ya Mkao tukizungumza Uwanja wa Ndege, mara mnauweka katika ujenzi wa kiwango cha lami, mara mnautoa. Tatizo liko wapi? *Please,* tunaomba Uwanja wa Ndege wa Musoma ujengwe kwa

kiwango cha lami, biashara ya kuuweka na kuutoa na kuanza kuukarabati kwa kiwango cha changarawe tumechoka. Mara ndege zinakuja, mara zinasimamishwa kwa sababu ya uwanja mbovu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa alianza kuusema *Veda one*, *Veda two* karudi. Sasa akaja tena *Nyerere One*; sasa sijui akirudi tena *Nyerere two*, ataendelea kuongelea huu uwanja! (*Kicheko/Makof!*)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine...

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Taarifa.

MBUNGE FULANI: Uwanja jamanil! *Chief Whip!*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya, subiri Taarifa.
Mheshimiwa *Chief Whip*.

TAARIFA

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
(KAIMU MNADHIMU MKUU WA SERIKALI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nimpe Taarifa mzungumzaji ambaye sasa hivi umemwambia aketi kwamba mikakati yote na mipango yote ya Serikali inavyotekelvezwa ikiwemo ujenzi wa *flyovers* hautegemei ni Jimbo la Mpinzani au siyo la mpinzani. Kwa hiyo, naomba asipotoshe umma. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya, unapokea hiyo Taarifa?

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, sina haja ya kujibu taarifa yake. Naendelea na mchango wangu. (*Kicheko/Makof!*)

MBUNGE FULANI: Anapoteza muda.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunazungumzia barabara ya Kisolya – Bunda – Nyamswa; barabara ya Nata ambayo inatokea Musoma Vijiji kwenda Serengeti, barabara ya Tarime – Mtomara mpaka Ngorongoro; lakini pia tunataka hizi barabara ambazo zinaenda katika mbuga zetu, kama kweli utalii ndiyo unaongoza katika pato la Taifa, kwa nini sasa tusitengeneza barabara ambazo zinaenda katika hizi mbuga zetu ili watalii waongezeke, Serikali iendelee kupata mapato tuweze kufanya mambo mengine? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa pia nimeona kwenye kitabu chako, nakupa hongera, barabara ya Tanga – Saadani – Bagamoyo, isishie kutengewa fedha, zijengwe kwa kiwango cha lami. Barabara ya kutoka Iringa kwenda *Ruaha National Park*, kutoka pale Tarangire, zote hizo ziwekwe lami ili utalii wetu ukue.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nizungumzie tu barabara ya Iringa kwenda Ruaha, zaidi ya kilometra 120, leo hii watu wanashindwa kwenda kule. Mvua ikinyesha wanatumia zaidi ya saa manne na hii Mbuga ya Ruaha ndiyo mbuga ya kwanza Afrika Mashariki kwa ukubwa na ina wanyama wengi. Kwa Afrika ni mbuga ya pili kwa ukubwa, lakini ni mionganoni mwa mbuga tano zinazochangia mapato ya Serikali. Sasa kwa nini tunashindwa kuweka lami kwenye hizi barabara ambazo zinaenda katika mbuga zetu ili kukuza utalii wetu? Hilo pia ni jambo la msingi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie fidia ya barabara ya kutoka Mwanza kwenda Musoma. Katika kipande cha Jimbo langu wananchi wamedai fidia kwa muda mrefu katika kupisha ule ujenzi na tena barabara ndiyo ilifuata nyumba za wananchi, siyo wananchi walifuata barabara, watalipwa lini? Hapa pia nimetumwa na mpiga kura *senior*, baba yangu Mzee Wasira, ana nyumba yake pale Manyamanyama, mlipeni. Lini sasa mtawalipa hawa watu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ukarabati wa hii barabara unaendelea, imekwisha, haijakamilika, tayari barabara zimeanza kuharibika. Hivi hawa Wakandarasi mnaowapa *tender mnatumia vigezo gani?* Kabla tu barabara haijakabidhiwa, tayari kuna mashimo kama mahandaki. Juzi niliuliza swali, hii barabara ya Dodoma, hapa Dodoma Waheshimiwa Wabunge wenyewe mnajua katika maeneo yetu, kila siku zinakarabatiwa. Kule Ununio, barabara ile ya Mbagala kule Dar es Salaam na yenyewe hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuone ni namna gani hawa Wakandarasi wetu wanajenga barabara zenye viwango! Hilo ni jambo la msingi sana Mheshimiwa Waziri. Kama wanashindwa kazi, washughulikieni. Siyo kwamba Wakandarasi wanachezea tu Serikali; mmewapa *tender*, hawafanyi kazi kama vile ambavyo inatakiwa na fedha za Serikali zinaenda bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni madeni ya Wakandarasi. Barabara nyangi zimesimama kwa sababu Serikali hamjalipa Wakandarasi fedha. Naomba sana... (*Makofii*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, na yule wa mwongozo, sijui taarifa, sijui kitu gani, umehesabia hapo?

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri achukue, alikuja Bunda, tunahitaji Mkoa wa Mara tupate fedha za kutosha... barabara zetu. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa David Ernest Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, ajiandae.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hususan katika mpango wake wa Makadirio ya Mapato na Matumizi wa mwaka unaofuatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo napenda kuanza nalo, maana nina mambo kama sita hivi ya kuzungumza kwa haraka haraka. Jambo la kwanza ni utekelezaji wa miradi ya barabara. Hii imekuwa ni kilio kwa Wabunge wote ndani ya Bunge, nami kama Mbunge wa Jimbo la Mombasa nimekuwa nikilalamikia hivi kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali ya kawaida tu ambayo hata Waheshimiwa Mawaziri wanasema, tumekuwa tukilalamikia juu ya ahadi wanazotoa Viongozi wetu Wakuu hususan Marais, zinachukua muda mrefu sana kukamilika. Nimezungumzia barabara ya kutoka Kamsamba, yaani Kibaoni – Kilyamatundu – Kamsamba unakwenda mpaka Mlowo zaidi ya kilometra 200. Aliahidi Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete mwaka 2009, lakini barabara ile mpaka leo imekuwa ni *story* ambayo haibadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia kitabu cha Mheshimiwa Waziri hapa, ukiangalia kwenye ukurasa wa 269, fedha iliyotengwa mle ndani, unakuta tu ni *rehabilitation, sijui feasibility study*, yaani shilingi milioni 120, shilingi milioni 200; kwenye zaidi ya kilometra 200, ni sawa na kazi bure. Kwa hiyo, tunataka Serikali iwe na mpango maalum kukamilisha hizi ahadi za Waheshimiwa Marais wanazozitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuendana na barabara hiyo msisahau lile Daraja la Mombasa. Mmelitengea shilingi bilioni tatu, wananchi sasa tumeshachoka kusikia zile *story* za kila mwaka; fedha inatengwa, *feasibility study*, tuko *site*; tunataka daraja, hatutaki *story* hizo ambazo zimekuwa zikijirudia kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu kwa haraka haraka ni usimamizi wa huduma za usafiri na uchukuzi hususan

majini na kwenye maziwa. Sana sana mnachokuwa mnazungumzia kila mara, Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa; lakini kuna maziwa madogo madogo yallyoko kule kwetu, kwa mfano Ziwa Rukwa liko mpaka kule Momba; kuna Ziwa Manyara, watu wanakuwa kule kila siku, maboti yanaua watu, lakini taarifa zake huku huwezi kuzikuta na hakuna hatua yoyote ambayo inakuwa ikichukuliwa na Wizara yako. Kwa hiyo, tungependa mnapotoa ufanuzi muyajadili pamoja na maziwa haya madogo likiwemo Ziwa Rukwa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya kuyajadili hayo machache ya Jimbo langu, nizungumze sasa masuala ya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia Shirika la Ndege (*ATCL*) ni kama vile hatujawahi kuwa na shirika nchi hii. Yaani ni kama vile ndiyo limeanza mwaka 2016, lakini ukweli ni kwamba Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wakati anaondoka madarakani aliacha ndege 11. Hii kila mtu anajua kwamba ziliachwa ndege 11 ambazo zilipotea katika mazingira ambayo hayaeleweki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nia njema inaonekana kwamba tunahitaji kufufua shirika letu la ndege na kuna sababu za msingi zimeelezwa, hakuna mtu anayebishana nayo; lakini kuna mambo tunahitaji kuwashauri kama wachumi. Kununua ndege *cash* kwa kulipa asilimia 100 siyo sifa nzuri sana kiuchumi tofauti na utaratibu ambao duniani watu wote wanatumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nimeona kwenye bajeti mmetenga shilingi bilioni 500 kwa ajili ya ununuzi wa ndege, ni jambo jema hakuna mtu anayekataa. Nunueni ndege kama utaratibu wa watu wengine wanavyofanya. Lipa *ten percent*, ndege inakuja nchini inafanya kazi. Kwenye hiyo fedha mnaweza kununua zaidi ya ndege kumi tofauti na sasa hivi mnavyotaka kwenda kulipa *cash*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa sisi hatukatai, lakini tunachojaribu kuwashauri, jaribuni kufanya mambo kwa utaratibu wa kawaida wa kichumi ambapo fedha moja inaweza ikasaidia mambo mengine wakati jambo lingine na lenyewe linafanyika. Kwa hiyo, hicho ni kitu ambachoh nasema ni muhimu tukawa tunakizungumzia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tuelezeni kuhusu deni ambalo lilikuwa linaikumba *ATCL*, kwamba mnasema ndege zitakuja, hofu yetu ni kwamba kwa mfano hiyo ndege ambayo itakuwa inakwenda mpaka huko Uchina sijui wapi; tunafahamu kuna kesi Mahakamani kuhusu Shirika la *ATCL*, madeni yanayodaiwa; ikitokea sasa ndege ikaenda kule, ikakamatwa ikazuiwa kule, maana yake hasara kwa Taifa itaendelea kubaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunataka tuje kwa nini Serikali imechukua hatua ya namna hii kwa sababu mpaka sasa hivi hizi ndege zimekuwa zikinunuliwa kwa utaratibu mmoja tu; wa Mheshimiwa Rais kununua na kuzileta ndani ya nchi, lakini ule utaratibu wa kishirika wa kiuendeshaji ambao unaweza kuwaathiri huko nje kutokana na deni ambalo shirika lilikuwa nalo tangu awali utatupeleka wapi? Kwa hiyo, tungependa tupate ufanuzi juu ya hili jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumza jambo la tatu kwa haraka haraka kuhusu Shirika la *TAZARA*. Kila mwaka tumekuwa tukilalamika kuhusu *TAZARA*, kwamba *TAZARA* haifanyi kazi vizuri, sasa hivi ukiangalia kwenye rekodi zao wanasema mwaka huu angalau umebeba mizigo tani laki moja. Wakati Shirika la *TAZARA* linaanza lilikuwa linabebe mizigo tani milioni moja kwa mwaka, sijui kama umenielewa, lakini leo tunajisifu kwa tani laki moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jibu ni moja tu, kwamba nchi mbili wanachama, zinategeana juu ya hili shirika, ndio maana hili shirika haliwezi kuendelea. Kila siku mgogoro kwenye hili shirika umekuwa ukisemekana ni *management*, lakini ukweli ni kwamba hapa kuna kutegeana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama mnashindwa, kuna *plan B* vilevile. Mnaweza mkazungumza na Zambia pamoja na Tanzania mkakubaliana kwamba sisi tunafikiri hii reli kutokea Tunduma mpaka Dar es Salaam, sisi watu wa Tanzania tuwe tunaihudumia wakati huu kuna matatizo. Watu wa kutokea Tunduma mpaka kwenda *New Kapiri Mposhi* kule wahudumie watu wa Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu mizigo siyo tu ile inayotoka Kongo, kuna mizigo ambayo inatoka Mbeya pale kuja Dar es Salaam; kuna mizigo inayopitia Iringa na maeneo mengine; tunaweza tukaitumia hii kama sehemu mojawapo ya reli ya kat, yaani mkavunja mkataba, kila mmoja wa kipande chake akatumia huku na wao watu wa Zambia wakatumie kule. *You can go on that way*, inaweza kusaidia kuliko sasa hivi mnatumia fedha nydingi na shirika halione kani liklenda mahali popote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nataka nzungumzie hapa, nimeona kwenye hotuba, Serikali inataka kufufua Shirika la *TTCL*. Shirika hili lilikuwepo tangu mwaka 1993, lakini kwenye *records* hapa wanasema tunataka tutoke wateja laki mbili mpaka kufika milioni moja; mpaka mwaka 2020 wanahitaji kufikisha wateja milioni nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *Master plan* ya *investment* yao, fedha wanazohitaji ni Dola 663,000 kwa miaka hiyo mitano ili wafikie wateja milioni nne lakini ukiangalia Kampuni dogo kabisa la *Halotelambalo* limeanza Oktoba, 2015 wenyewe *within* mwaka mmoja na kidogo wame-invest dola bilioni moja, wana wateja *2.7 million*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *mindset* ya Watanzania bado imekaa ile ile kwamba sisi ni Serikali, tutaliendesha Shirika Kiserikali; sasa imegeuka mashirika yote Serikali ihudumie; haiwezekani! Kwa hiyo, lazima tu-change mtazamo huu ambao umeenda; na ndiyo maana unakuta hata Shirika la *ATC* sasa hivi linakwenda katika huo mtazamo wa Kiserikali Serikali, siyo mtazamo wa Kikampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi biashara ni ushindani! Sasa huwezi kwenda kwenye ushindani wa kimawasiliano unaona kuna *Vodacom* pale, kuna *Tigo*, kuna *Airtel* halafu na wewe unakuja *TTCL* kwanza una-invest kidogo, pili hamna *marketing strategies* ambazo unaweza uka-penetrate kwenye *market*, lakini mtu atakuja atasema hawa *Hallotel* wanatumia mkongo wetu. Yes, wanatumia minara ya *TTCL*, lakini *at the end of the day* gharama yao wao *Hallotel* iko chini kuliko gharama ya wao wanaomiliki huo mtambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapo unakuwa unajiuila, hapa utakuwa unafanya nini katika hili Taifa? Yaani *we don't think big!* Bado mitazamo yetu kufikiri juu ya biashara ni mitazamo ya kijima. Tunafikiri bado kule nyuma kwamba Serikali inaweza kufanya kila kitu, lakini sasa hivi dunia inaendeshwa na *market forces*; soko huru ndiyo linaloamua juu ya uendeshaji wa uchumi wa nchi husika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda haya mashirika na hizi taasisi ndogo ambazo tunataka Taifa lifanye biashara, zisibaki na huu mtazamo; hii *mindset* ya sasa kwamba kila kitu Serikali ita-*injectfedha* pale, kwamba Serikali ndiyo itaendesha hiyo kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Shirika la *ATC*, Serikali ikitoa mconi maana yake na Shirika lenyewe linakufa kwa sababu mtazamo wetu si ule ambao kwamba tunaweza kujiendesha wenyewe tukafika kule tunapotakiwa, kwa sababu sasa hivi kila kitu tunataka *investment* ya Serikali. Kwa, kwa hiyo, ni lazima tubadilishe mtazamo wetu dhidi ya haya mashirika ambayo Serikali inahitaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, nashukuru na naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ajiandae.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami nataka kuchangia kidogo kuhusiana na miundombinu katika Mkoa wa Katavi. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai. Pia naunga mkono asilimia 100 hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nataka nijikite zaidi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Kwanza kabla sijaenda mbali zaidi, ukisoma katika ukurasa wa 22 na 19, nataka nimwulize Mheshimiwa Waziri; barabara ya kutoka Mpanda - Stalike, barabara ile imekwisha, lakini ukisoma kwenye hotuba ya Waziri ametenga shilingi bilioni 4.1. Sasa pesa hizi ametenga kwa ajili ya ujenzi wa kitu gani? Ukisoma, mradi umekamilika. Nadhani atakapokuja kuhitimisha anieleze hii shilingi bilioni 4.1 ni ya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna madaraja mengi katika Mkoa wa Katavi ambayo yamekuwa yanasuasua kwisha na watu wa Katavi wanaendelea kupata shida, hawana mawasiliano kutoka kwenye Wilaya moja kwenda kwenye Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna daraja la lteka ambalo liko katika Halmashauri ya Nsimbo, daraja hili karibu kila mwaka limekuwa likiua watu, magari yanakwama, watu wanalala njiani, lakini katika bajeti hii sijaona popote daraja hili limetajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya kutoka Kibaoni – Mpanda; barabara hii imechukua muda mrefu sana. Watu wa Katavi wanahangaika, lakini muda mwingine wanasaafiri zaidi ya masaa 12 kutoka Mpanda mpaka Sumbawanga, lakini katika bajeti hii sijaona kokote ambako Mheshimiwa Waziri ametenga bajeti kwa ajili ya kumaliza hizi barabara. Sasa sielewi ni nini mkakati wa Serikali; ni aidha kuendelea kuwatesa na kuwanyanyasa watu wa Katavi? Kwa sababu ukiangalia kwenye mikoa mingine, kwa mfano, Mkoa wa Bukoba pamoja na Pwani wametengewa zaidi ya

shilingi bilioni mbili kwa ajili ya matengenezo tu ya kawaida; lakini Mkoa wa Katavi leo hii tunaongea mnatutengea shilingi milioni 27! Za nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nijikite katika suala la mawasiliano. Wakazi wa Katavi ni watu ambao wanatangatanga, wanapata shida. Mawasiliano ni ya hovsky, barabara ni mbovu, sasa Mheshimiwa Waziri, kuna wakazi wa Kata ya Ilunde iko katika Jimbo la Mheshimiwa *Engineer Waziri wa Maji*; Kata ile watu wanasafiri kilometa 10 mpaka 15 kwenda kutafuta *network* ili awasiliane na mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Serikali gani hii ambayo mpaka leo mtu anasafiri, anatembea kilometra 10, anatembea kilometra 15 kwenda kutafuta *network*na *network* yenye inakuwa ni mbovu, mtu mpaka apande kwenye mti ndiyo awasiliane! Hatutakubali watu wa Katavi. Kwanza nashangaa kwa nini watu wa Katavi bado wanaendelea kuwa na imani na Chama cha Mapinduzi! (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya kutoka Tabora - Sikunge kwenda mpaka Katavi. Barabara hii imechukua muda mrefu sana, mpaka sasa Wakandarasi haijulikani, kila siku wanaweka tu changarawe, wanarekebisha na ma-grader, ukipita, watu wanalala njiani lakini pia kuna Mto Koga ambao miaka mwili iliyopita kuna zaidi ya watu 30 walikufa katika mto ule, lakini ile barabara mnayotuletea ni marekebisho tu. Kimsingi, hamko *serious* na Mkoa wa Katavi. Naomba majibu ya Mheshimiwa Waziri, ni kwa nini hawakutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa Mkoa wa Katavi? Wanayotuletea ni marekebisho tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la kushangaza, ukisoma kwenye ukurasa wa 285 anasema; barabara hizi zitatumia kwa ajili ya marekebisho shilingi milioni 846 kwa kilometra 695.5. Ukitawanya shilingi milioni 846 kwa kilometra 695.5, katika hizi barabara zaidi ya saba zilizotengewa kwa ajili ya marekebisho, kila barabara yenye urefu wa kilometra 112, barabara ya kutoka Mamba -

Kasansa; barabara ya kutoka Mpanda – Ugala; barabara ya kutoka Mnyamasu kwenda Ugala; zina zaidi ya kilometa 111; na nyingine, hii barabara ya kutoka Kagwira kwenda mpaka Karema ni kilometa 250.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu nadhani ni utani, unawezaje kufanya marekebisho kwa barabara yenye urefu wa kilometa 250 kwa shilingi milioni moja? Huu ni utani na hatuwezi kukubali kwa sababu kuna mikoa ambayo inapewa vipaumbele na Mkoa wa Katavi ukiendelea kuwekwa nyuma wakati ndiyo mkoa ambao unaongoza kwa kuzalisha mazao ya chakula ambayo Waheshimiwa humu ndani wanatumia vyakula hivyo. Sasa hatuwezi kuendelea kukaa kimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie pia kidogo kuhusiana na ujenzi wa uwanja wa ndege. Mwaka 2010, Serikali ilitenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege katika Mkoa wa Katavi, katika Manispaa ya Mpanda, lakini mpaka hivi tunavyoongea, wakazi wale hawajalipwa na wengine wakati wanalipwa zile pesa kwa jili ya kupisha ujenzi wa ule uwanja, watu walilipwa sh. 75,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu ambaye alikuwa ana nyumba, ana kiwanja unaenda kumlipa sh. 75,000/=! Mpaka leo ninavyoongea kuna wananchi ambao wanalala kwenye mahema na wako mjini katika Kata ya llembu; pia kuna Kata ya *Airtel* ambayo wakazi wake wengi walitolewa kwenye lile eneo ambalo uwanja ulijengwa. Sasa watu hawa hawawezi kuendelea kusubiri huruma ya Serikali. Viwanja vilikuwa ni vya kwao na walikuwa wamejenga nyumba, sasa walihamua tu kupisha ujenzi huo.

MHeshimiwa Naibu Spika, pia wakazi wa Mpanda hawakuwa tayari kwa ajili ya matumizi ya Uwanja wa Ndege, kwa sababu *majority* ya watu wa Katavi wanatumia usafiri wa reli ambapo usafiri wa reli wenyewe ni wa hovyo, barabara ni mbovu, mnaenda kuwapelekea Uwanja wa Ndege ambao mpaka sasa wanapanda watu wawili, watatu kwenye vindege vile vidogo vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka kufahamu, hii *TTCL* ina faida gani? Sioni faida ya *TTCL* kwa sababu ukiangalia *Hallotel* wamekuja juzi tu, lakini leo wanafanya vizuri. Sasa labda Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha, atueleze faida ya *TTCL* ni nini? Kuna haja gani ya kuendelea kuitengeta bajeti *TTCL*?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kufahamu sasa, Wizara ina mkakati gani wa kuongeza pesa katika Mfuko wa Barabara kwa Mkoa wa Katavi? Kwa sababu hakuna kitu chochote kinachoendelea hapa. Ukitisoma kwenye ukurasa wa 287, hakuna bajeti yoyote iliyotengwa kwa ajili ya Mkoa wa Katavi. Sasa wakazi wa Katavi wataendelea kusubiri miradi ambayo haikamiliki kwa wakati, lakini ni miradi ambayo inawafanya watu wa Katavi waendelee kudanganywa kwamba mtaletewa barabara, mtatengenezewa *standard gauge* kwa ajilli ya watu ambao wanasafiri kwa njia ya reli, hakuna chochote! Mtaendelea kuwadanganya mpaka lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nahitaji majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni lini sasa wakazi wa Mkoa wa Katavi wataacha kusafiri siku mbili mpaka tatu kulala njiani? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka kufahamu, ni kigezo gani ambacho kinatumika kwa ajili ya kuwapata wakandarasi... (*Makof*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa na Mheshimiwa Ali Salim Khamis ajiandae.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kukutana hapa kutimiza wajibu wetu wa Kikatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara, vile vile nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jambo moja kubwa sana. Kwa muda mrefu tulikuwa tuna kilio cha reli ya kati. Tulipokuja kwenye Bajeti ya mwaka 2016/2017, Waheshimiwa Wabunge wengi sana tulijadili reli ya kati ya kutoka Dar es Salaam - Kigoma - Mwanza kwenda Mpanda kwa maana ya reli ya kati yenye tafsiri ya Kitanzania. Kwa hiyo, tumeona jiwe la msingi limeshawekwa na vile vile mkandarasi anaanza kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa naibu Spika, nianze kuishauri Serikali kwenye hii *project*. Tunatumia zaidi ya shilingi trilioni mbili kwa ajili ya Mradi wa Reli (*Phase I*). Ukitazama, kuna *lot* ya Morogoro mpaka Makutupora, halafu *lot* ya Makutupora mpaka Tabora. Ninachotaka kuishauri Serikali, kuwa na *lot* zenye masafa mafupi, *cost per unit* inakuwa kubwa. Ni vizuri kwa sababu kuna *fixed cost whether* ni kilometa 100, kilometa 200, kilometa 300, kilometa 600 *mobilization cost* unaweza ukakuta ni *almost the same*. Ni vizuri tukaangalia namna gani tunatoa huko mbele *lot* zinakuwa ni za kilometa ndefu ili angalau gharama iweze kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tunatumia fedha za ndani; tunachukua shilingi zetu *converting into dollar* kumlipa Mkandarasi. Nawaomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Wizara ya Ujenzi na watu wa *TANROADs* wapo hapa, waambieni hao Wakandarasi *strictly sub-contracting jobs* zote zifanywe na *local* kwa sababu zitasaidia fedha yetu tunayoitoa kubaki ndani. Tusipokuwa makini, tunaweza tukajikuta fedha nyingi zinakwenda nje badala ya kubaki ndani ya uchumi wetu. Hili ni muhimu sana kuliangalia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza watu wa Wizara ya Nishati (*REA*). *REA* mkiangalia ilivyoanza, ilianza na *foreigners* lakini baadaye wali-up grade kuhakikisha *sub-contracting jobs* zote zinafanywa na *local*. *Lotszilizotoka* sasa hivi asilimia kubwa inafanywa na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali, huu ni mradi mkubwa sana, mkitusaidia kuweka hii *condition* kwenye kazi na hata tulivyokuwa tunazindua mradi wa maji ya Ziwa Victoria, tumemwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji kwamba *600 billions* ya mradi wa maji ya Ziwa Victoria, hawa Wakandarasi waliopewa wa kutoka India wahakikishe kazi zote za *sub-contracting* zinafanywa na Watanzania ili tubaki na fedha ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili katika hili, nataka niishauri Wizara kwamba, mpango wetu ni reli ambayo itatumia umeme na hii ni miezi kama 36. Nawaombeni Serikali, hakikisheni suala la *TANESCO* na *TRL* kufikia muafaka namna gani umeme utapatikana. Itakuwa ni hatari sana kwamba tumefika mwisho, mradi umejamiliwa wa *phase* ya Morogoro suala la umeme likaanza ku-*drag*. Kwa hiyo, ni vizuri hivi vitu vyote vikienda vinafuatana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne katika hili la mradi wa reli; leteni Sheria ya *RAHCO* Mheshimiwa Waziri tuifute hapa ndani, haraka sana, ili tuweze kumpa mamlaka *TRL*. Halafu chagueni *financial institutions* moja, *TIB* atafute *financial advisor* wazunguke duniani kutafuta fedha. Hatuwezi kumaliza huu mradi kwa fedha zetu za ndani tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nina hofu, hata hii *phase II* anaweza akaomba Mturuki tu peke yake. Kwa hiyo, mtafunga milango ya *competition*. Watabaki wao kwa sababu wanatu-*finance* wao, wanaleta mkopo wao kwa kilometra hizo 400 zilizobaki, zitatu-*restrict competition*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukichukua Benki kama *TIB* ikatafuta *financial advisor* mwingine ambaye ni *recognised internationally*, wakazunguka kutafuta fedha, mtampunguzia kazi Mheshimiwa Dkt. Mpango kutafuta fedha kwenye Mfuko wa Hazina ku-*finance* hii miradi mikubwa, kwa sababu tuna miradi mikubwa sana ambayo iko katika Wizara yenu, miradi ya ndege na miradi hii ya reli. Tukiamua kuwa *strategic* miradi hii itatusaidia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwenu ni *transfer of knowledge*. Nawaomba, hawa Wakandarasi wanaotujengea reli, *componentya transfer of knowledge* ni muhimu mno. Tutakapokwenda kwenye *phase* inayofuata kwa sababu tutahitaji kuwa na mabehewa na vichwa vyatreni, lazima kuwe na makubaliano kwamba atakayeenda kutengeneza vichwa vyatreni na mabehewa, ahakikishe anachukua watu wetu wakati wa kutengeneza ili watakaporudi hapa ndani, hizi kazi za kutengeneza vipuri, *assembling* zote zifanyikie nyumbani kuliko kufanyika nje. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawapongeza, mnafanya kazi kubwa sana ya kuifungua nchi na Mheshimiwa Rais ameamua, *vision* yake *it is very costfull*. Matokeo ya *vision* ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli inaweza ikatuchukua muda mrefu sana kuona matunda yake, lakini *I believe* baada ya miaka mitano, miaka kumi kazi hizi zinazofanyika sasa hivi matunda yake yataonekana wazi kwenye uchumi wa nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, mwezi Septemba tarehe 14 Mheshimiwa Rais alituahidi Nzega ujenzi wa kilometra 10. Ahadi hii ilitokea wakati yeye akiwa Waziri wa Ujenzi na Rais Kikwete juu ya ujenzi wa kilometra 10 ndani ya Mji wa Nzega.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia kitabu cha Mheshimiwa Waziri hapa hakuna *any shillings* ambayo imekuwa *allocated* kwa ajili ya hizi kilometa 10, na ukitazama kwenye bajeti ya 2016/2017, *road fund* fedha zilizokuwa *allocated* kwa ajili ya Halmashauri ya Nzega ilikuwa ni milioni 707 lakini tulichopokea ni milioni 190.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Waziri, na wewe kwenye mwezi Desemba, wakati Rais anaenda Chato, niliongea na wewe kwa simu ukaniambia Hussein sema mbele ya wananchi na Mheshimiwa Rais kwamba daraja la Nhobola na daraja la Butandula tunajenga mwaka huu wa fedha. Shekhe mwaka unaisha, Mheshimiwa Waziri na mwaka huu tumepoteza watu watatu katika mto ule. Mheshimiwa Waziri naomba sana hili jambo lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, zimekuwepo hoja nyngi sana juu ya *priority*, na mimi nataka niiombe Serikali, tunapojenga hii reli tufanye *cost benefit analysis* kwa sababu tunawekeza fedha, ni wapi *return on investimate* itakuwa rahisi. Mzee Chenge ameongelea *northen corridor* kwamba wanakwenda *speed* sana, lakini wanakimbilia wapi? Wanakimbilia wafike Kigali ili waweze ku-*benefit* na Msongati. Tujiulize kipi kiwe mwanzo? Tufike Mwanza ama twende Kigoma ndio iwe *priority*? Wizara lazima ifanye hii *analysis* ili iweze kutuambia Watanzania kwamba tunakwenda Mwanza kwa sababu *tuta-benefit* mizigo ama tunakwenda Kigoma kwa sababu *tuta-benefit* mizigo na fedha tulizowekeza kama nchi zitarudi haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa ni jambo la upotезаји wa fedha za Watanzania kama tutakwenda Mwanza wakati kuna biashara kubwa Kigoma, Kalemii ama Msongati. Mzigo ulioko Msongati kama tutawahi kufika Msongati kabla ya *northern corridor*, sisi ndio tutakuwa na *competitive advantage* kuliko watu wengine. Ni vizuri sana mkafanya maamuzi haya kwa mtazamo wa kibashara zaidi. Reli si kubeba abiria, abiria ni *subsidiary, fundamental* ni mzigo unaobebwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie, Mheshimiwa Waziri, kwa heshima kabisa nitakuomba unapokuja kufanya *wind up* hapa uniambie daraja la Nhobola ambalo imekuwa ni ahadi ya muda mrefu ni namna gani linajengwa. Halmashauri ya Mji wa Nzega na TAMISEMI haziwezi kujenga daraja la Nhobola.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tunaweka fedha kwenye *Rural Road Agency* inayotaka kuanzishwa. Mimi ningeshauri tulitazame sana, *TANROADS* imekuwa *good performer*. Kurundika shughuli kwenye TAMISEMI wote tunalalamika, TAMISEMI Elimu malalamiko, TAMISEMI Afya tunalalamika, kila kitu TAMISEMI, ni afadhali tuangalie namna gani *Rural Road Agency* ni *unit* ndani ya *TANROADS*. Kwa sababu safari hii mmeiwekea bilioni 80 hamna kitu haiwezi, lakini *TANROADS* ina sheria ina vyanzo vyake mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *Rural Road Agency* haina vyanzo vyake mapato inapewa kwa hisani, haiwezi kuwa *sustainable unless* mtuletee sheria hapa. Lakini mimi nadhani kwa *technical no how* kwa *infrastructure* iliyopo ni vizuri tukaangalia hii wakala wa ujenzi wa barabara vijijini ikiwa ni *sub unit* ndani ya *TANROADS* ambayo inatengewa fedha kwenye bajeti ya *TANROADS* na *TANROADS* waisimamie. Kwa sababu *TANROADS* wana watu, tayari wana ofisi kwenye mikoa na wana kila kitu. Tukianzisha hii *agency* tutaanza kujenga miundombinu mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru, naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ally Salim Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratius Ngala wa, Mheshimiwa Lucy Magereli ajiandae.

MHE. ALI SALIM KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa katika hali ya afya njema. Na mimi naomba nitumie fursa hii kuchangia katika Wizara hii ya Mawasiliano na Uchukuzi. Kwanza ningependa

ninukuu Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano katika nyongeza ya kwanza katika masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Katiba yetu kwenye mambo ya Muungano mojawapo ni bandari. Sasa, bandari ni uchumi wa nchi, na mpaka leo hii toka Muungano huu tulipoungana miaka 53 bado suala hili liko katika masuala ya Muungano ambayo Zanzibar wameonesha wazi kuwa wanao uwezo wa kuisimamia bandari na kuweza kujitegemea kupitia bandari yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hadi leo hii bado suala hili limewekwa katika masuala ya Muungano na inapelekea kuizua Zanzibar kuwa na ile *free port* kujenga *port* kubwa pale ambayo iweze kusaidia kupokea mizigo inayotoka Kusini kufika Zanzibar na ile ya Kaskazini kufika Zanzibar wakagawana mizigo ile badala ya kusafiri umbali mrefu katika kusambaza mizigo katika hili eneo la Afrika Mashariki. Sasa nimuombe Waziri, iko haja sasa wakatafakari kutumia ile Ibara ya 98(b) kuletwa mswada hapa ili suala la bandari hili lisiwe tena la Muungano na liachiwe Zanzibar iweze kujitegemea ili kuendesha bandari yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni suala la Posta na Simu, hili pia ni jambo la Muungano. Tangu ilipovunjika Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1979 lilianzishwa hili shirika, lakini mpaka sasa hivi Zanzibar hatujaona faida yake ni ipi. Kwa hiyo, namuomba Waziri atakapokuja hapa kuhitimisha hoja hii basi atuambie, *at least* hii miaka kumi ya Rais aliystaafu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuambiwa *TTCL* imetengeneza kiasi gani na mgao wa Zanzibar ni kiasi gani, wametupa kiasi gani na bado kiasi gani tunawadai ili tujue, kwa sababu hii ni kama mali ambayo tumempa mtu anatukamatia, lakini hatujui hesabu, hatujui kitu chochote. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atupe ufanuzi wa jambo hili la Posta na Simu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni suala la anga. Taasisi hii inakusanya makusanyo mbalimbali kwa ajili

ya nchi yetu. Lakini bado mpaka sasa hivi masuala hayo hayapo wazi, namuomba Waziri atakapokuja hapa atuambie miaka hii kumi ya Rais Mstaafu, Idara hii imekusanya kiasi gani na imetoa mgao wake kwa Zanzibar kiasi gani, na kiasi gani tunawadai kwa sasa ambacho hawajalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne ni suala la ndege. Mwaka wa jana hapa nilitoa ushauri katika Wizara hii, kwamba ni kweli tunahitaji Shirika la Ndege na hili wala hakuna mtu analipinga, lakini nikatoa ushauri kwamba tutafute mtaalamu wa masuala ya ndege, biashara za ndege ili huyu atuongoze kuonesha tuanzishe shirika kwa namna gani. Mfano, leo Shirika la *ATCL* tulipotoa ushauri Serikali imekimbilia kwenda kununua ndege haraka haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake tumenunua ndege ya *Bombardier* ambayo hii ni Kampuni ya Canada, lazima wa Canada walete *base* yao hapa kwa ajili ya kuzifanya *mantainance* hizi ndege. Lakini miezi saba baadaye tumeingia mkataba na *Boeing* ambaao nao inabidi walete *base* yao kwa ajili ya kufanya *mantainance* ndege hizi za *Boeing* ambazo zitakuwepo hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shirika kubwa kama hili *Ethiopian Airline* kwa miaka sabini zimekuwa zikifanya kazi ya biashara ya ndege kwa kutumia kampuni moja tu ya *Boeing*, kuanzia sasa hivi sasa baada ya kuona kwamba wameshakuwa *sustain* ndipo wameanza kuingia mkataba na kampuni ya *Air Bus* kwa ajili ya kuongeza huduma zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa lengo la kuanzisha *Air Tanzania* ni biashara, lakini mpaka leo biashara hii ipo Serikalini haiwezi kuendelea. Biashara ukiichanganya kwenye Serikali haiwezi kuendelea. Lazima Shirika la Ndege la *Air Tanzania* liwe *independent* ndipo liweze kuendeshwa kwa faida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano; leo kuna Shirika hapa la *TPDC*. *TPDC* inafanya kazi sasa hivi lakini hili Shirika linaendeshwa kwa hasara, kwa sababu ina fedha na kodi

ambazo Serikali imeziweka inalipwa na *TPDC* ambazo ukiuliza hizi pesa zinalipwa kwa sababu zipi hajjulikani. Mwisho wa siku ikija kuombwa bajeti zao hapa ile bajeti ambayo wameomba wao kufanya kazi zao za kawaida tu hawapati, lakini wao wameshazalisha fedha na fedha zimepelekwa Serikalini, halafu Serikali inawarudia *TPDC* wanaambiwa kwamba waweze kuijendesha wao wenyewe. Hatuwezi kuendesha biashara namna hii.

Mhsimiwa Naibu Spika, sasa inaonekana kwamba wataalam wetu ambao wanatushauri, wanatushauri ambavyo visivyo. Sasa Mheshimiwa, Shirika hili la *Air Tanzania* toka liliyvoanzishwa, amesema hapa Mheshimiwa Silinde kwamba Mwalimu Nyerere alituachia ndege 11 lakini leo inaonekana ndege hizi sita imekuwa jambo la ajabu. Ndege 11 zilikuwa zinafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa shirika hili toka liliopoanzishwa linatua katika viwanja vyetu kule Zanzibar, lakini halilipi kodi hili shirika, sasa kwa nini lisilipe kodi mpaka leo hii, hapa mwaka wa jana nilimuuliza Mheshimiwa Waziri hapa akajibu swalilangu akasema kwamba kuna deni la milioni 230 linahakikiwa na *CAG* halafu tutalipa. Juzi ninamuuliza hapa anasema hata hajui kama zimelipwa. Sasa sijui huyo *CAG* mpaka leo hajamaliza wakati *CAG* ameshawasilisha ripoti zake mara mbili hapa Bungeni hakuna hili jambo. Sasa tuambiwe kwamba ni lini *Air Tanzania (ATCL)* italipa deni lake la *landing fees* kwa Mamlaka ya Viwanda vya Ndege ya Zanzibar na tupewe deni lile halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana alisema Bhagwanji hapa sisi sote ni ndugu moja, sasa kwa nini mnatzamisha sisi tusipate kuendelea na hili jambo mmelfanya kama liwe la Muungano? Sisi hatujakataa kwamba liwe la Muungano lakini sasa hivi imeonyesha kamba mashirika haya kwamba sisi tunachangia lakini hatufaidiki nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba Wizara ya Muungano ilivyokuja hapa imetoa *ratio* ya asilimia 21 kwa 79. Nimuombe Mheshimiwa Waziri sasa, shirika limeanza

kufanya kazi naomba sasa kila baada ya muda patolewe takwimu kuhusu Shirika hili kama tumepata faida au tumekula hasara ili tujue Zanzibar mgao wao ukoje. Kama mgao wetu ni hasara tushajua hasara, lakini kama kuna faida basi tushee faida kupitia Shirika la Ndege la ATCL.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo biashara ya Ndege imekuwa ni ya ushindani mkubwa. Shirika letu hili tulilibinafsisha kwa Shirika la Ndege la *South African Airways*. Na tulipowapa *South Africa* tumewapa na zile *route* zetu ambazo sisi tulikuwa tunakwenda. Leo tumeshanunua ndege ya 787 *Dreamliner* kwa ajili ya kwenda nchi za mbali. Lakini namuomba Waziri atuambie hizi *route* ambao itakwenda hii ndege atakapokuja hapa atuambie kwamba ndege yetu tulionunua mpya kubwa itakwenda kwenye *route* hizi huko Ulaya na Marekani anaposema. Kwa sababu ninavyofahamu kupata *route* kwenda Ulaya na Marekani si jambo rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano tu *Kenya Airways* leo wana *route* mbili kutoka Nairobi kwenda London, lakini kwa sasa hivi kwa Shirika lao ilimetetereka kidogo katika maswala ya kiuendeshaji na *Oman Air* wao wana *route* moja kutoka Muscat kwenda London, matokeo yake sasa *Oman Air* wametafuta hii *route* kwa muda mrefu ili wawe na *route* mbili kutoka Muscat kwenda Heathrow lakini wamekosa, wamerudi kwa *Kenya Airways* wamekwenda kununua ile *route*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *route* hii wamenunua kwa *20 million USD*, tena kwa masharti ambayo *Kenya Airways* imewambia kwamba tunakupeni hii *route* tunakuuzieni lakini pia ndege yetu moja kubwa lazima muitumie kwa ajili ya kufanya kazi, yaani waikodi *Oman Air*; na wamekubali kulipa *20 million USD* kwa sababu ya *route* moja tu kutua Heathrow. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri atuambie kwamba ni *route* zipo ambazo ndege hii itakwenda ambazo zipo *available*, kwa sababu tayari *route* tulishamuuzia *South African Airline* akaua Shirika

letu ye ye wakaendelea na shirika lao na sasa hivi wanapata maendeleo makubwa kuititia *ATCL* ambayo ilikuwepo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli wa mambo ni kwamba kama Serikali haitotafakari basi tunaweza tukajikuta kwamba lengo la kuanzisha hii ndege kwamba itupe faida matokeo yake ikawa ni mzigo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani *British Airways* ilikuwa inakuja hapa Tanzania, Dar es Salaam lakini imesitisha safari za kuja Dar es Salaam, kwa nini, kwa sababu ya ushindani wa kibashara na kwamba leo *Emirates* ana ndege nne ambazo zinakwenda Uingereza kila siku, kwa hiyo *route* ile ndiyo ambayo abiria wanaitumia na *British Airways* imejikuta kwamba imekosa abiria wa kutosha kuweza kuitoa ndege Londan kuleta hapa. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilli sana kwa sababu hapa lengo na madhumuni ni kwa ajili ya kuijendesha kiuchumi ili Taifa letu liweze kufunguka na kutoka kwenye umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Deogratius Ngalawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, Mheshimiwa Victor Mwambaliaswa ajiandae.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza kabla ya yote nipende tu kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nipende kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, pia na watendaji wote na viongozi wakuu wa taasisi ambazo zipo chini ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha kwanza ambacho pengine ningependa kuchangia leo ni juu ya mtandao wa mawasiliano ya simu. Ikumbukwe kando kando ya Ziwa Nyasa yaani Ziwa Nyasa liliyvo eneo kubwa ni eneo la Ludewa. Upande wa Nyasa kama Wilaya lina urefu wa kilometra 112 na upande wa Kyela lina urefu kama kilometra

10; lakini sisi Wana-Ludewa tuna kilometra zipatazo kama 220, cha kushangaza na cha kusikitisha, mpaka hivi ninavyoongea kando kando mwa Ziwa Nyasa tuna tarafa moja na tuna kata sita, hakuna kijiji wala Kata ambako kuna mawasiliano ya simu. Ikumbukwe kwamba eneo lile la ziwa lipo mpakani mwa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, enzi zile sisi tukiwa watoto, yule bwana mkubwa akija unakuta kuna *Sub Marine* imesimama juu, wazee wetu walikuwa wanakimbia wanajifungia kwenye mahandaki, lakini mahandaki hayo sasa hivi hayapo. Kwa hiyo, eneo hili hata kama ni kutoa taarifa za kiulinzi na kiusalama tunashindwa. Kwa hiyo, nipende tu kumuomba Mheshimiwa Waziri alipe kipaumbele cha juu lile eneo kwa sababu ni eneo kubwa, kwa sababu ukiangalia ni kama vile tumetengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyasa yenye kilometra 112 vijiji vyake vyote vinamtandao wa mawasiliano, Kyela yenye kilometra kama 10 vijiji vyake vyote vina mtandao wa mawasiliano. Lakini unapoanza mipaka, *beacons* za Ludewa hakuna kijiji hata kimoja; vijiji 15, tukiweka kata sita vinakuwa vijiji 18 kata sita hakuna kijiji wala kata ambayo ina mawasiliano ya simu. Kwenye hili tunajiona kama ni wakiwa na kama vile tumetengwa. Ukiwa pia kwenye eneo hilo hilo la barabara yaani barabara zimeishia Nyasa na Kyela. Eneo la Ludewa halina kabisa. Tuna vijiji 15 ambavyo havijawahi kufika hata baiskeli, wananchi wameamua kuchimba wenyewe kwa mkono. Kwa hiyo, tunaiomba sasa Serikali ije iwaunge mkono wananchi wale ili waweze kupata barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii hata nikizungumzia suala la *road upgrading* Ludewa imeachwa kabisa. Kuna *upgrading* Makete kama mkoa, kuna *upgrading* Makambako, Wanging'ombe na Njombe lakini Ludewa imeachwa. Sasa huwa tunashindwa kujua Ludewa ina matatizo gani mpaka tusi-*upgrade* barabara hata moja? Mimi nipende kutoa masikitiko ya Wana-Ludewa kwa sababu inakuwa sio jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ndani ya mkoa yanafanya *road opening, paving way*, lakini eneo la Ziwa Nyasa ambalo lipo mpakani mwa nchi; hata kipindi kile wakati wale jamaa wanakuja kuja na ule mtafaruku tukawa tunashindwa wapi pa kwenda, barabara sehemu ya kukimbilia hatuna, mawasiliano kusema kwamba tutatoa taarifa kwenye vyombo vya usalama hakuna. Sasa nipende tu kujua labla pengine Mheshimiwa Waziri utakapokuja kuhitimisha utatuambia inawezekana Ludewa ina makosa ambayo imeifanya ndani ya Serikali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuja upande wa bandari. Tunaishukuru Serikali kwa zile meli tatu, meli mbili za mizigo na meli moja ya abiria. Vilevile kuna ujenzi wa gati ndani ya Ziwa Nyasa bado tunakuja kuona hapo hapo, upande wa Wilaya ya Nyasa kuna gati zinajengwa na kwenye bajeti mmeweka, upande wa Kyela kuna gati zinajengwa lakini ni upande wa Ludewa tu pekee yake ndiko hakuna gati.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunakuja tunajiuliza maswali mengi sana, Ludewa ina tatizo gani na nchi hii? Kyela wanawekewa gati, Nyasa inawekewa gati. Halafu mahali huku ndiko ambako tunasema leo tuna uchumi wa viwanda. Tunapozungumzia uchumi wa viwanda huwezi ukaisahau Liganga na Mchuchuma. Liganga na Mchuchuma inakuja lakini miundombinu hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu angalia upande wa barabara; tunashukuru barabara ya Itoni - Njombe - Manda - Ludewa, mkandarasi yupo, ipo kwenye *mobilization finalization*, lakini kuna zile barabara ambazo ndio zinakwenda kwenye ile miradi, kuna barabara ya Mkia kuelekea Madaba.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunaambiya inafanya *rehabilitation*, lakini mimi nilikuwa najua tungeweke sasa kwenye upembuzi yakinifu baadae iende kwenye usanifu wa kina ili twende kwenye lami, kwa sababu barabara hii ndiyo inayoelekea kwenye mradi mkubwa wa Liganga. Kwa

sababu utakuta sasa miundombinu Ludewa ni miundombinu ya kizamani na hakuna *consideration* ambayo inafanyika kwa ujio wa miradi mikubwa kama ya Liganga na Mchuchuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unaponiambia kwamba kuna *flagship project* za Liganga na Mchuchuma; na ndiyo maana huwa tunauliza, hii Liganga na Mchuchuma itaanza lini? Maana tungeweza kupewa *schedule* kwamba mwaka huu mpaka mwaka huu kuna hiki kuna fidia inafanyika, mwaka huu mpaka mwaka huu kuna hiki kinafanyika *then* baada ya hapo tunajua sasa mradi *unatakeoff*. Kwa inawezekana tunaona kwamba hata hii miundombinu inakuwa haiwekwi kwa sababu hata huo mradi wenyewe haufahamiki utaanza lini? Kama ungekuwa unafahamika utaanza lini mimi ni naamini kwamba hizi barabara zinganzwa kutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababau Nchi inavyoolekea kwenye viwanda mnakitegema chuma cha Liganga, Nchi inavyoolekea kwenye viwanda mnakitegemea umeme utakaozalishwa Mchuchuma, megawati 600; lakini kwa nini leo hatuweki hiyo miundombinu?. Wenzetu wote ambao wako ndani ya Mkoa kuna *activities* zinafanyika lakini ni Ludewa tu. Ukija gati inafanyika Nyasa na Kyela; Ludewa inaacha, ukija mawasiliano ya simu kuna Nyasa na Kyela; Ludewa inaachwa. Ukija barabara zinaishia kwenye *beacon* ya Kyela na huku inaishia kwenye *beacon* ya Nyasa lakini Ludewa inaachwa. Sasa lazima tuijulize panashida gani na Ludewa?

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deo Ngalawa taarifa.

TAARIFA

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba mchangiaji anayechangia yeye ajikite

kwenye kuomba fursa hiyo, iende kwake asilalamikie huku analalamika tu aombe moja kwa moja kwamba na taka gati, nataka nini badala ya kulalamikia maeneo mengine ambayo wamepata fursa, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deo Ngalawa unaipokea hiyo taarifa?

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Hiyo taarifa siipokei, kwa sababu haiwezekani watu wengine wanapewa fursa wengine hawapewi halafu uniambie kwamba... tena unanifundisha hata namna ya kusema, haiwezekani, tunazungumza vitu vilivyo-/ive. Mimi bajeti ninayo kila kitu kipo humu wakati mwingine mnaaweza mkaenda mbali labda kwagine labda pengine huku kwa sababu kuna Mawaziri na Ludewa hayupo Waziri, ndiyo mnataka kuniambia hicho, kwa nini Ludewa isipewe? Hiyo ndio hoja yangu mimi ya msingi

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa wa Stella Manyanya, *Chief Whip.*

TAARIFA

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kwanza niseme kwamba eneo linalozungumzwa lina nihusu, lakini nilipenda tu kumfahamisha nikirejea kwa kifungu cha 68(8) na (9). Ninatoa taarifa kwamba Mheshimiwa Deo kama ambavyo Mheshimiwa Msongozi alijaribu kukushauri, ni kwamba haya Majimbo au Wilaya tunapewa fursa za aina tofauti. Kwa mfano kwenye Jimbo lake kuna chuo kikubwa cha VETA kinajengwa ambacho kipo kwenye jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni kwamba fursa zipo na hata hizo barabara au gati anazozingumzia kwa jimbo la Nyasa kwa kweli ni aibu kabisa ye ye kuzungumzia

kwa sababu hawa wote ni ndugu zake na zinaenda pamoja, na kimsingi mimi ningemshauri ajielekeze kwenye kuomba mahitaji kwenye eneo lake. Lakini akisema nazungumzia Nyasa haitendei haki kwa sababu kuna tatizo kubwa la miundombinu ukilinganisha na maeneo mengine. Nasikitika kuzungumza jambo hili ila tu namuomba ni vema akafanya hivyo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deo Ngalawa unaipokea hiyo taarifa?

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo taarifa siipokei. Mimi naongea kwa niaba ya wananchi wa Ludewa na wananchi wa hii. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama sehemu kipo na wakati huo mahitaji yetu yanalingana naona ni kama tunabaguliwa. Kwa sababu katika eneo la Ziwa Nyasa sisi ndio wenyenye eneo kubwa kuliko Nyasa, kuliko Kyela, sasa kule kuna kitu gani kikubwa ambacho hiyo miundombinu inapewa kipaumbele kuliko huku kwingine, kwa nini? Maana ukiniambia unajenga chuo lakini barabara hamna chuo hicho kitakuwa hakina maana yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo lazima ifike mahali kwamba hizi fursa lazima tupewe wote sawa. Kama ni chuo hata Nyasa kinajengwa, kipo kwenye programu, kwa hiyo, maana yake utakuwa una barabara, una gati na hicho chuo kitakuja. Ndiyo maana tunazungumza hapa Ludewa ina tatizo gani? Kama ni uvuvi, uvuvi mkubwa unafanyika Ludewa kuliko Nyasa na Kyela, wao wanajua, sisi ndio mabingwa wa kuvua, mabingwa wakuvua ni Wakisi kuliko Wamatengo, kuliko Wanyakuysa, sisi ndio tunaowafundisha, tumeenea kwenye mabwawa yote ya Tanzania. Ndiyo maana tunazungumza, kwa nini hatupewi kipaumbele? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Marehemu Deo Filikunjombe, Mungu amuweke mahali pema, amekuja hapa, amezungumza sana juu ya haya mambo;

kapita kaenda. Ndiyo kwa maana sisi tunasema kwamba tunakosa gani? Licha ya kwamba tumekuwa tukiwasiliana na Waheshimiwa Mawaziri juu ya masuala haya. Si kwamba ni mara yangu ya kwanza mimi kuzungumza hapa Bungeni, nimezungumza sana na Mheshimiwa Mbarawa, ni mezungumza sana tu na Mheshimiwa Ngonyani, na inafikia kipindi hata Katibu Mkuu nimejaribu kuwa nampigia simu amekuwa hapokei, na mpaka nikajitambulisha naitwa Deo Ngalawa, Mbunge wa Ludewa *still yet hapokei!* Inawezekana Ludewa kuna matatizo. Ndiyo maana tunazungumza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama ni suala la fursa basi tupewe fursa sawa. Leo hii Ludewa barabara hazipitiki, hii barabara tunayozungumza ya Mkiu – Madaba imekata, watu wanakaa siku mbili njiani *why*, wakati wenzetu wanapeta? Vijiji havijawahi kufika baiskeli hata siku moja, pikipiki haljawahi kufika vijiji 15. Wananchi wameamua wenyewe kuchimba, kwa nini Serikali isije? (*Makofi*)

Tumeamua wenyewe *clips* za wananchi kuchimba Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri niliwaonesha kwamba tumeamua kuchimba wenyewe kwa majembe kwa nyundo kwa mitalimbo. Leo hii tunapokua kuzungumza unasema tusilinganishe, tusilinganishe kwa *base ipi*? Ifike mahali fursa lazima tupewe sawa, mimi langu ilikuwa ni...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA ...kufikisha ujumbe huo na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Asante sana, Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimetaja Wabunge wawili kuchangia, kwa muda uliobaki na dhani taarifa zilikuwa nyingi zimechukua muda kwa hiyo na dhani tutamalizia na mchangiaji mmoja Mheshimiwa Lucy Magereli.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Naibu Spika, na kushukuru sana kwa kunipa fursa nichangie na mimi Bajeti ya hii Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na nianze kwa kueleza na kukubaliana kwamba ninaunga mkono hoja zote katika ripoti ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye hoja ya suala la Daraja la Kigamboni. Hili mimi nitaendelea tu kulisemea tu sana kwa sababu imekuwa ni changamoto kubwa. Tozo katika Daraja la Kigamboni zimekuwa kero kuliko msaada, gharama zinazotozwa pale kwenye lile daraja ni kubwa kuliko hali halisi ya wananchi wa Kigamboni. Tulitarajia kama ambavyo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati anazindua lile daraja alivyosema, kwamba daraja lile lifungue fursa za kuwasaidia Watanzania, wananchi wakazi wa Kigamboni kubadili mfumo wa maisha yao lakini pia kujipatia fursa za maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wakazi wa Kigamboni bado ni aina ya wananchi ambao wanawaza watoto wao watakula nini, watapata wapi ada ya shule, lakini pia wanawaza hata namna ya kugharamia mavazi ukilinganisha na hali halisi ya uchumi ilivyo leo na ukiangalia hali halisi ya uchumi wa Tanzania, mimi nafikiri bado hatujafikia mahali pa kulipia tozo za huduma muhimu na nyeti kama barabara na madaraja.

Mheshimiwa NAibU Spika, kwa hili naomba kabisa Mheshimiwa Waziri litazamwe upya, ikiwezekana kama iko lazima sana kwa sababu daraja hili limejengwa kwa ubia wa NSSF na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania basi lile eneo la NSSF lifanyiwe utaratibu fedha zile ambazo zilitolewa kama mchango wa NSSF kwenye ujenzi wa lile daraja zilipwe, kwa sababu daraja hili kulingana na jinsi ambavyo nimesoma kwenye hotuba yako itakuwa ni *connection* ya *interchange* ile barabara ya haraka ya Chalinze, sasa kama ndivyo je, ni eneo lile tu la kuvuka pale kwenye daraja litakuwa linalipiwa ama na barabara zote za *interchange* zitakazo unganisha na daraja la Kigamboni zitakuwa zitalipiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama zote zitalipiwa bado tufahamu kabisa kwamba ni changamoto kubwa kwa Watanzania wa sasa hivi na hali ya uchumi ilivyo jamani hatujafika huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichangie baadhi ya vipaumbele ambavyo vimeoneshwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusu eneo la Kigamboni nikianzia na barabara ya Kongowe – Mjimwema – Kivukoni ambayo kulingana na taarifa zilizopo katika kitabu cha Waziri ni ya kilomita 25 na imepangiwa shilingi bilioni 1.290. Mheshimiwa Waziri niombe sana kwamba barabara hii ni muhimu sana kwetu na tangu mwaka jana ilikuwa katika bajeti yako, lakini kwa bahati mbaya nadhani ilipata fedha kidogo mno ambapo utaratibu wa upanuzi ulianzia tu eneo la pale kwa Mwingira mpaka kufika Mji Mwema na imeishia hapo.

Kwa hiyo, nikuombe sana katika bajeti yako ya utusaidie kutengwa fedha za upanuzi wa hiyo barabara kwa sababu ndicho kiunganishi kikubwa cha kutoka eneo la Kivukoni mpaka kwenda kuunganisha na Kongowe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimeona Mheshimiwa Waziri amelitaja daraja la Mzinga, nikuombe sana lile daraja msimu wa mvua tunapata matatizo makubwa sana, na mwaka juzi daraja lile lilikatika kabisa tulishi kwa msaada wa ujenzi ulifanywa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Kwa hiyo, nimeona umetenga fedha pia kwa ajili ya daraja hilo, tunaomba pesa hizo zipatikane na hilo daraja lijengwe ili kuweze kuwa na *connection* baina ya wakazi wa Kigamboni na eneo la Temeke; lakini ukizingatia na hiyo *express way* ambayo nimeona mnaijenga, nimeona inakwenda mpaka eneo la Mbagala ambayo na amini ile barabara ya Kongowe itakuwa ni *feeder road* kwenda kwenye hiyo *interchange* ambayo umeizumzumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye barabara ya Tungi – Kiswani – Kibada. Mheshimiwa Waziri wakati wa hotuba yako wakati wa uzinduzi wa daraja la Kigamboni

kwa maneno yako mwenyewe kabisa ulisema umejipanga na utakwenda kumalizia lile eneo la kilomita 1.5 lilitobaki baada ya daraja kwenda mpaka pale kwa Msomali, na ulisema fedha zipo na ujenzi ungekamilika mapema iwezekanavyo. Hata hivyo lile eneo limebaki na sura kama alivyosema Mheshimiwa Shabiby jana, kwamba umevaa koti zuri safi na tai lakini chini umevaa kaptula na makobazi.

Mheshimia Naibu Spika, ukubwa wa barabara inayotoka darajani ni kubwa mno ya njia tatu pande zote mbili lakini inakwenda kuingia katika barabara ndogo halafu mbaya na chafu sana, tena wakati huu wa mvua ukifika eneo lile hata kupita na gari ndogo ni shughuli kubwa na pevu. Kwa hiyo tunaomba kipande hicho cha kilometra 1.5 kimaliziwe kama ambavyo uliahidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba hiyo hiyo ya Mheshimiwa Waziri ya siku ya uzinduzi wa daraja la Kigamboni alisema lile eneo la darajani, mpaka pale kwa Msomali kwa maana ya kuunganisha barabara ya Kivukoni kupitia Tungi, Vijibweni mpaka Kibada usanifu umeshakamilika na barabara ile ilipaswa kuanza, ujenzi ungeanza Mei 2016 lakini mpaka ninavyozungumza leo hakuna kinachoendelea eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sielewi kilichotokea yawezekana ni ufinyu wa bajeti lakini tunaomba sasa msimu huu kwa maana bajeti hii inayokuja mtusaidie eneo lile liweze kukamilika na barabara ile ikamiliike kwa sababu ndio barabaara ambayo ina wasaidia wananchi wengi wa kazi ya maeneo ya Kisarawe II, kata za Kibada, Mji Mwema kupita kwa ajili ya kuja kikutana na eneo la daraja la kuvuka kuja mjini. Barabara ile ya sehemu ile ni mbaya sana na kisehemu cha lami kilichojengwa kuanzia Tungi mpaka Vijibweni karibu kuelekea hospitali eneo limesaharibika kabisa lina hali mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe pia nizungumzie au ni muulize Mheshimiwa Waziri atusaidie. Katika bajeti iliyopita ulitupangia fedha kwa ajili ya barabara ya Kibada -

Mwasonga kuelekea Tundwi Songani. Najua unaufahamu umuhimu wa barabara hii, ndiyo barabara ambayo magari makubwa sana ya yanayotoka Kimbiji kuelekea Kiwanda cha Saruji cha Nyati yanakopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ile kwa kweli imepata uharibifu mkubwa sana kutokana na matumizi makubwa ya yale maroli na kwa hiyo wananchi wa kawaida na usafirishaji wa kawaida unashindwa kuendelea kabisa katika eneo lile kwa sababu mara nyingi yale magari yanapoharibika au yanapokwama katika barabara ile wakazi wanashindwa kuendelea na maisha yao ya kawaida. Kwa hiyo, sasa sielewi imekuaje kwamba barabara hii ya Kibada – Mwasonga – Tundwi kuelekea Kimbiji hajatengewa fedha msimu huu wala haujaizungumzia wakati 2016/2017 ilikuwepo kwenye bajeti yako Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe pia nizungumzia barabara ambayo nimeona umezungumzia katika kitabu chako ukurasa wa 35, barabara ya bandari ambyayo ni ya kilomita 1.2 lakini barabara ya Minjeni kilometra moja na *Dock Yard* kilometra 0.7. Barabara ile Mheshimiwa Waziri nikusihii sana kwamba tungependa itengewe fedha lakini itanuliwe kiasi cha kutosha, kwa sababu msongamano wa yale maroli pale bandarini unatupashida shida sana.

Mheshimiwa Naibu Soika, kweli unafiri ni haraka sana kutoka Kigamboni kwa kuvukwa kwa daraja na kuondoka haraka kufika mjini lakini ukishaondoka darajani tu unakutana na hii barabara ya bandari imejaa foleni ndefu, unakutana na barabara ya Mandela imejaa foleni ndefu, kwa hiyo, shughuli ile inabaki kuendelea kuwa shughuli vilevile. Hata kama kungekuwa na nafuu barabara ya bandari bado utaratibu wa kuegesha magari yale makubwa ni mgumu mno na barabara hii inashindwa kuitikika. Kwa hiyo, tunaomba mtusaidie utaratibu wa kutengeneza *parking* maalum ya yale magari ili barabara zibaki huru zitembee kwenda na kurudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nikushukuru sana, nimeona umetenga bajeti yako pia ukurasa

wa 214 umetenga fedha kwa ajili ya upanuzi wa gati ya pale Kivukoni, Kigamboni. Eneo lile nalo ni shida kubwa sana, vivuko vile tunashukuru vinafanya kazi na vinatusaidia sana kwa sababu sisi kwa bahati mbaya tumejikuta na hilo janga la kujikuta barabara kwa maana ya daraja tunalipia na kivuko tunalipia, hewala kama ndivyo ilivyowapendeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikuombe basi mtusaidie sana Bajeti hii fedha za utanuzi wa gati pale zipatikane kwa sababu hata kama pantoni imefika imetia dock pale utaratibu wa utokaji wa magari unakuwa taratibu mno kwa sababu eneo ni finyu mno. Kwa hiyo, pantoni kupakia rutu nyingine iende inachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru kwa haya ya leo, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa uchangiaji wa kipindi chetu cha kwanza kwa siku ya leo. Nitayasoma majina ya wachangiaji wetu wa mchana; lakini kwa sababu vi-note huwa vinakuja hapa mbele wanaosomwa mwanzo sio lazima wawe wa kwanza kuchangia.

Nasoma majina ya wachangiaji wa mchana. Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Aysharose Matembe, Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mheshimiwa Augustine Holle, Mheshimiwa Susan Limbweni, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Omar Kigua, Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, Mheshimiwa Moshi Kakoso na Mheshimiwa Stephen Ngonyani.

Wengine ni Mheshimiwa Omary Mgumba, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mheshimiwa Quambalo Willy Qulwi, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Martin Msuaha, Mheshimiwa Saul Henry Amon, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Kiswaga Destery na Mheshimiwa Abdallah Chikota.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutangaza majina hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

(Saa 6:59 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11: 00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Tukae. Katibu.

NDG. LINA KITOSI - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 – Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, tutaanza na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa atafuatiwa na Mheshimiwa Augustine Holle, Mheshimiwa Susan Limbweni ajiandae.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuniwezesha na mimi kuweza kutoa mchango wangu kwenye hoja iliyo mbele yetu. Naomba nichukue nafasi hii vilevile kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, kwa mawasilisho yake mazuri sana aliyoafanya kwenye hotuba yake. *(Makof)*

Vilevile kuwasilisha hotuba nzuri ina maana hotuba hii ilitayarishwa na timu ya wataalam wenyewe weredi mkubwa sana, napenda nichukue nafasi hii, kumpongeza Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na wataalam wote kwenye Wizara hii kubwa ambao wamewezesha kutengeneza hotuba nzuri kama hii. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuipongeza na kuishukuru Serikali hii ya awamu ya tano ambayo kwa makusudi mazima imeamua kuwekeza karibuni asilimia 40 ya bajeti yetu kwenye miundombinu. Ukiwekeza kwenye miundombinu sawasawa na kuweka akiba kwa ajili ya vizazi vijavyo, kwa sababu miundombinu inachochea maendeleo na uchumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naomba nije kwenye barabara yangu ya Mbeya - Chunya - Makongorosi. Napenda nifahamishe Mheshimiwa Waziri kwa sababu ye ye anaifahamu sana hii barabara. Kwanza ninamsifu sana ametoka Mbeya mpaka Itigi anaikagua barabara. Hii barabara zamani ndiyo ilikuwa njia ya *The Great North Road* inayotoka Cape kwenda Cairo, ilipita Chunya, Itigi ikaja Manyoni kwenda Arusha - Nairobi mpaka Cairo. Serikali kwenye mlaka ya 1960, 1961, 1962 ndio waliibadilisha route hiyo ya *Great North Road* kwa kutumia GV kwa kuifanya itoke Mbeya - Iringa - Dodoma - Babati kwenda Cairo, lakini originally ilikuwa ni hiyo ya Chunya, Itigi, ndiyo hii *The Great North Road* kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nakusifu sana umeikagua unaifahamu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali imejenga barabara hii kwa kiwango cha lami kutoka Mbeya mpaka Chunya, kilometra 72 tunawashukuru sana wananchi wa Chunya, mmetupunguzia sana matatizo. Sasa hivi kutoka Mbeya kwenda Chunya ni shilingi 3,500 au 4,000 ambapo ilikuwa shilingi 10,000 au shilingi 12,000 sasa hivi mazao tunayolima Chunya yanafika haraka kwenye masoko, kwa hiyo mimi napenda kuishukuru sana Serikali kwa jambo hili kubwa ambalo wamelifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mwaka huu Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 22 barabara hii kujengwa kwa lami kutoka Chunya kwenda Makongorosi hadi Mkola kilometra kama 42. Kwenye kitabu chake nimeionna na ninajua kwa sababu niko karibu sana na Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, *tender* imetangazwa sasa hivi wako kwenye *evaluation*, najua ujenzi utanza siku za karibuni,

ninawawashukuru sana. Naomba barabara hii ambayo ni ya muhimu sana tuiendeleze mpaka ifike huko inakohitajika kufika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona vilevile kwenye kitabu kwamba, barabara hii hii kwa mwaka huu inaanza kujengwa kutoka Mkiwa kwenda Itigi ili mwaka ujao itoke Itigi kuja tukutane katikati na Mheshimiwa Massare, kwa hiyo naishukuru sana Serikali kwa niaba ya wananchi wa Chunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niongelee barabara ndogo ambayo inatoka kijiji cha Kiwanja inakwenda kwenye kijiji cha Mjele kwenye Mkoa mpya wa Songwe, Wilaya mpya ya Songwe Barabara hii inashughulikiwa na Halmashauri ya Chunya, lakini kwa kuwa sasa hivi Mkoa wa Songwe ni Mkoa mpya na Chunya iko Mkoa wa Mbeya kwa hiyo hii barabara inaunganisha mikoa miwilli, inaunganisha Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Songwe. Kwa hiyo, naomba Serikali na Wizara muichukue barabara hii iweze kushughulikiwa na *TANROADS* badala ya kushughulikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kidogo kwenye hii hii barabara ya Mbeya - Chunya - Makongorosi. Barabara hii ina matatizo makubwa mawili, naleta killio kwako Mheshimiwa Waziri. Tatizo la kwanza barabara hii baada ya kujengwa kilometra 72 ukipita sasa hivi kama ulivyoona ulivyopita kumeanza kuonekana matobo mawili, matatu, manne; kwa barabara ambayo haijamaliza hata miaka mitano siyo vizuri, haina afya hii. Kwa hiyo, naomba sasa hivi mnavyofanya *evaluation* kwa kuiendeleza barabara hii kutoka Chunya kwenda Makongorosi na Mkola, kandarasi ambaye alijenga huku nyuma ambaye hata miaka mitano haijapita mashimo yanaonekana asipewe kazi tena. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili hili labda tungechukua mfano wa barabara ambayo inajengwa na Serikali kutoka Ruaha ambayo sasa hivi imefika mpaka Mafinga imekwenda Igawa, barabara imejengwa kwa kiwango cha juu sana. Labda wakandarasi wengine wa

barabara hapa nchini wangekewenda kujifunza kwa mkandarasi huyu anayejenga barabara kutoka Ruaha kwenda mpaka Igawa kwenda mpaka Tunduma. Kwa hiyo hilo ni tatizo la kwanza, kwamba kumeanza kujitokeza mashimo madogo madogo, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri na viongozi wako mlielewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la pili, Chunya tunalima tumbaku, sasa wasafirishaji wa tumbaku wanaobeba tumbaku kutoka Chunya kuleta Morogoro kutoka Chunya kuja Mbeya wanapakia malori ya rumbesa kwa sababu wanajua kwamba kule sijui hakuna mizani; wanapakia malori ya rumbesa ili akifika Mbeya ndipo anagawa hilo lori yanakuwa malori mawili. Sasa hiyo rumbesa inaumiza sana barabara ya lami ambayo mmetujengea inaumizwa vibaya sana. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri ni pewe hata *weighbridge* moja au mbili hata *mobile weighbridges* ili tuweze kuilinda hii barabara, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri katika hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niongee kidogo kuhusu uwanja wa Songwe. Naishukuru Serikali kwa awamu zilizopita na awamu hii, mmejenga uwanja wa ndege wa Songwe ambao unainua sana uchumi wa Mikoa ya nyanda za juu Kusini; Mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma, Katavi, Rukwa, majirani wa Zambia wa Congo tunatumia uwanja wa Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumeona hapa karibuni wakati wa masika huu, ndege zinatoka Dar es Salaam kufika Songwe kama kuna ukungu zinashindwa kutua, kwa hiyo naomba katika hii bajeti tunayoimalizia mwaka huu, Serikali iweke taa kwenye uwanja huo ili madhumuni ya Serikali ambayo ilikuwa imepanga kwa ajili ya uwanja huu yaweze kutimia. Vilevile naomba Serikali imalizie jengo la abiria kwenye uwanja wa Songwe, naomba tafadhalii sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niongelee reli ya *TAZARA*, reli ya Uhuru ambayo walijenga Waasisi wa Taifa

hili. Serikali inafanya jambo jema sana kuwekeza kwenye miundombinu, kutengeneza bandari, kujenga reli ya kati kwa *standard gauge*, bandari za Mtwara, Dar es Salaam, Tanga Serikali inawekeza ili iweze kuvuna kwenye uchumi wa jiografia wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hatuwezi kukamilisha jambo hili kama tutaelekeza tu kwenye reli ya kati na bandari zile basi bila kuingalia reli ya uhuru. Reli ya uhuru yenewe haihitaji kujengwa, reli ya uhuru inahitaji kukarabatiwa kidogo ifanye kazi, nadhani ni sheria ambazo zimeiweka reli ya uhuru. Naomba Serikali ishirikiane na Serikali ya Zambia tuangalie sheria hizo ni sheria gani ambazo zinaikwamisha reli hii bila sababu, ili bandari zikikamilika, reli ya kati ikikamilika na reli ya uhuru ikikamilika nchi iweze kuvuna kutumia uchumi wa jiografia ambao Mungu ametuwezesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye reli ya kati zimeanza *block trains* ambazo zinabeba mizigo inayokwenda Isaka au inayokwenda Burundi au Rwanda na reli ya *TAZARA* nayo ingeweza kufanya hivyo, tungeweza kufanya bandari kavu ikawa Mbeya au Makambako au Tunduma tukawa tunatoa *block trains* kwenda Dar es Salaam, Tunduma, Mbeya au Makambako. Naomba sana, tunapotaka kuboresha miundombinu ya kutumia uchumi wa Jiografia wa nchi hii basi tuiangalie na reli ya *TAZARA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa barabara ya mchepuko (*bypass*), Mheshimiwa Mwanjelwa aliongelea jana; ya kutoka Uyole kwenda Mbalizi. Sasa hivi *congestion* ni kubwa mno kutoka Uyole kwenda Mbeya Mjini na kuelekea Mbalizi. Barabara ni ndogo, ni ya siku nydingi, biashara ni kubwa mno, fursa ziko nydingi sana za biashara kwenye Mkoa wa Mbeya. Kwa hiyo, hii hadithi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina kila mwaka, naomba barabara hii ya *bypass* iweze kujengwa ili tuweze kuuokoa Mkoa wa Mbeya kwa uchumi ambao unaweza kudidimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Augustine Holle, Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Zungu.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie kwenye Wizara hii ya Miundombinu. Naibu Waziri anajua lakini bahati mbaya sana alifika wakati wa kiangazi. Hapa ninaposema, ninaposimama, naogopa hata kwenda Jimboni kwa sababu kuna vilio, kuna vifo, Mheshimiwa Naibu Waziri ile barabara imekatika kabisa. Hata kama ulimuagizia *engineer* siku ile kwamba ile barabara ipitike mwaka mzima ukimuuliza sasa hivi; kwanza namshukuru Meneja wa Mkoa, yule mama anafanya kazi kubwa sana lakini hela hana. Makandarasi wako kule, lakini kama unavyojuwa ile barabara ya Jimbo la Mlimba ina mito mingi sana, kwa hiyo kuanzia pale Idete Kalia Gogo mpaka ukifika Taweta, kule karibu na Madeke, Njombe barabara yote inakatika, mkandarasi anahangaika, leo akiziba hapa kesho imekatika hapa mito kila kona. Kwa hiyo, Jimbo la Mlimba linatakiwa litazamwe kipekee kuhusu masuala ya barabara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninaposema, sisemi tu kwa kujifurahisha lakini nimeona kwenye kitabu chenu kwamba mnaboresha barabara ya mpaka Madeke - Njombe, mnaposema Madeke, Njombe ndiyo inapakana na Mlimba, na watu wa Njombe wanataka ile barabara iboreshwe na mnajenga kwa kiwango cha lami ili watu wa Njombe wapite Mkoa wa Morogoro waje Dodoma, sasa mtapoboresha kule barabara ya Njombe mpaka Madeke mkiilacha kutoka Madeke - Tanganyika - Taweta hadi Mlimba (Ifakara) mtakuwa hamjaitendea haki thamani ya ile barabara ya Madeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninachoomba mnasema iko kwenye upembuzi yakinifu na kweli kabisa lakini kwenye vitabu vyenu hajazungumziwa kabisa hiyo barabara, huo upembuzi yakinifu na wa kina umeisha au vipi? Mnataraja kujenga kwa kiwango gani? Mnasema kiwango cha lami kuanzia Ifakara mpaka Mlimba, lakini mjue kwamba

ili tulinganishe Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Njombe inatakiwa barabara ifike Madeke kule Taweta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi naomba, tumeteseka kiasi cha kutosha miaka mingi tangu uhuru sasa na sisi angalau tufaidi matunda ya uhuru. Tunashangaa tu barabara za wenzetu lami, *flyover*, ndege, sisi hatutaki hata kuzungumzia ndege, tunataka barabara. *TAZARA* ipo inapita kule hivi wananchi wa kule wanaponea *ki-peace* cha kutoka Makambako mpaka Kilombero lakini *ki-peace* kinapita kwa wiki mara mbili au tatu.

Leo mama mjamzito anayetokea kule Masagati, Taweta, Njombe moyo unaniuma mimi, moyo unalia machozi akina mama wanakufa katika Jimbo la Mlimba, wanataka kujifungua hakuna hospitali ya uhakika, hospitali mpaka iwe Ifakara kilometra 230 hivi huyu mama mjamzito anafikaje kwenye hiyo hospitali? Wote mmezaliwa na wanawake, hebu muwaonee huruma wanawake wanaotokea katika Jimbo la Mlimba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanakufa kule jamani, kwa vile hakuna vyombo vya habari wangekuwa wanaripoti kila siku, lakini tunahangaika tu, hakuna *tv* nani apeleke *tv* yake kule sehemu ambayo haina barabara? Kwa hiyo, mimi naomba suala la barabara Mlimba ni kipaumbele. Naomba barabara, Mheshimiwa Naibu Waziri umefika Wananchi wamekushangilia ukamuagiza *engineer* lakini nakuambia leo hii hata hawa ma- *engineer* hawana bajeti ya kutosha, kinachotakiwa ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme sasa, kinachotakiwa ni kwamba barabara hii ya kilomita 230 kutoka Ifakara mpaka Madeke, mpakani na Njombe imekatika haina uwezo tena wa kupitika na hajapangiwaa pesa za kutosha. Hata kama tunasubiri lami, basi tunaomba ipitike kwa mwaka mzima na nimeongea na wataalam, *engineer* anasema kwamba ili hii barabara ipitike kwa mwaka mzima inahitaji inyanyuliwe kwa kiwango cha juu sehemu zile korofii kilometra zisizopungua 50 angalau, lakini

hela mliyoitenga kwa kukarabati hiyo barabara haisaidii, tutaendelea kuteseka wananchi wa Mlimba. Naomba mtuokoe tumo kwenye shimo, tunaonekana kama hatujapata uhuru ndani ya nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kuna akina mama, kuna vijana na wazee wanahitaji huduma. Kwa hiyo basi maeneo ambayo barabara imekatika, ukianzia Jimbo la Mlimba utaanza katika kata ya Idete Kalia Gogo. Vilevile kuna maeneo mbalimbali ambayo hii barabara haipitiki, utaenda Idete, Kalia Gogo, Kiogosi, Kisegese, Tandale, Mbingu, Ngajengwa, Njage, Udagaji, Mgugwe, Mlimba Mpanga mpaka Madeke - Njombe, hili eneo lote ninalosema ni barabara ambayo ni ya *TANROADS*, mnatusaidiaje wananchi wa Mlimba? Hali ni mbaya tunateseka. Kwa hiyo, ni muhimu wakaliangalia kwa jicho la karibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, ni Waziri wa kwanza uliyefika kuitembelea ile barabara, basi naomba uitendee haki, naomba tafadhalii uitendee haki ile barabara ungepita wakati huu kwanza usingefika ingebidi urudi Ifakara, Mkuu wa Wilaya alikuwa anaenda Mlimba akashindwa akabakia pale Mgugwe maji yamejaa yanakatiza barabara akarudi Ifakara. Ndiyo maana nilikuwa nalalamika haiwezekani Mkurugenzi tumemnunulia *V8* halafu gari mnamuachia Mkuu wa Mkoa, hivi huyu Mkurugenzi akitaka kuwahudumia wananchi wa Mlimba ataenda na usafiri gani? (*Makofii*)

Kwa hiyo tuna umuhimu wa vitu vyetu vibaki Kilombero. Yaani mimi hapa leo nalia na barabara, hela mlizotenga hazitoshi hata kwa haya matengenezo yanatakiwa linyanyuliwe matuta katika eneo korofi ya kilometra 50. Naomba mtutengee hela za kutosha. Ongeeni na wataalam wenu wanajua, na mimi haya nimeyapata kwa wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeomba barabara ya kutoka Mlimba, tuna Kata moja ya Uchindile ina mto mkubwa sana, huu Kilombero unaanzia kule, tunaomba ile barabara

ichukuliwe na *TANROADS* sisi hatuna uwezo wa kuunganisha hiyo barabara kama Halmashari kutoka Mlimba mpaka Uchindile. Vilevile kutoka kijiji cha Tanganyika tumeomba mpaka mkoani ile barabara muichukue *TANROADS*, kuanzia Taweta mpaka Tanganyika kuna mto mkubwa wa Kilombero unakatisha. Kwa hiyo, wananchi wametengwa na kata zao, jimbo la na Mkoa wao. Chonde chonde nawaomba sana mtuangalie na mtupe haya maeneo tuhakikishe kwamba barabara inapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo hivyo tu kuna suala la *TAZARA*. *TAZARA* mmeandika kidogo sana. Jimbo langu limepitwa na *TAZARA*, makao makuu ya *TAZARA* kiwilaya yako Mlimba, lakini *TAZARA* hiyo kuna wastaaafu wanadai miaka kenda rudi, wengine mpaka wanakufa watoto wameshindwa kusoma, ninyi katika kitabu chenu sijaona mahali popote. Namna gani mnasema tu sasa hivi sijui ngapi, naomba kauli ya Mheshimiwa Waziri wale wastaaafu wa *TAZARA* waliotumikia reli kwa muda mrefu, na watoto wao sasa hivi wanateseka na wenyewe wanateseka ni nini hatima yao nchi hii jamanii? Watu waliotumikia kwa moyo mkubwa kwa imani bila wizi kwa nini mnawafanya hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba muwaokoe wastaaafu wa *TAZARA*. Mheshimiwa Waziri ukija hapa useme kidogo kuhusu wastaaafu wa *TAZARA*, kama ndio wamesahaulika hawawezi kulipwa tena, basi mtuambie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mawasiliano, barabara hakuna simu wengine mpaka wapande juu ya miti, sasa haya mambo gani? Kuna maeneo ambayo huwezi ukapata simu, mimi mwenyewe nikienda Jimboni kipindi fulani utanitafuta hunipati, hakuna mawasiliano ya simu, naomba mtuangalie kwa karibu watu ambaa tupo *remote area*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mjini mnajenga mpaka *flyover* nyie nini? Kwa nini wenzeni mmetusahau huko?

Mnazungumzia tu viwanja vya ndege sisi havitusaidii. Hivi leo usafiri wa kule ni trekta, namshukuru kijana mmoja analitwa Muddy Kindindindi wa Ifakara alinunua mabasi yake yanaitwa Mukti yakawa yanaenda mpaka Mpanda lakini kutokana na barabara mbovu sasa hivi hayaendi tena, wanatasafiri na trekta. Jamani, hivi bado tupo dunia hii ya leo? Mimi naomba Waziri kama ikiwezekana Naibu Waziri umruhusu akimaliza kupitisha hii bajeti twende mimi na yeze tuongozane mpaka kulekule alikofika mwanzoni aone hiyo barabara ndipo atapata uchungu akija ataona kwamba hii hela mliyotenga hapa sio lolote sio chochote. (*Makofi*)

Mheshimia Naibu Spika, naomba tafadhali, hata kama huna mafuta mimi ntawaambia wananchi wa Mlimba wajichangishe tukuletee mafuta twende ukaikague hiyo barabara sasa hivi na watafurahi sana wakikuona. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio changu ni barabara...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda umekwisha Mheshimiwa, ahsante sana.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, barabara, Mlimba. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mussa Zungu atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Stanslaus Mabula ajiandae.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, na momi nachukua nafasi hii kukushukuru kunipa nafasi, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwanza nitoe pongezi za dhati kwa Serikali, Mheshimia Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Waziri mwenye Wizara hii kwa

kazi nzuri ambayo wanaifanya. Lazima tuwapongeze sababu Wizara hii imeshika mambo mengi kwenye nchi lakini bado inafanya kazi vizuri sana, lazima tuwape pongezi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko makubwa sana yamepatikana kwa kipindi kifupi sana toka Mheshimiwa Rais aingie madarakani na hasa alivyompa Wizara hizi tatu Mheshimiwa Mbarawa. *The Country is progressing sasa.* (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajikita kwenye maeneo yale ya siku zote, yapo mabadiliko kidogo tumeyaona, lakini Mheshimiwa Waziri nilitaka nikwambie sijui kama ulishawahi kuona kiti kinawahi kukamata mshahara wa Waziri; na Kiti kikikamata mshahara wa Waziri ujue kura ikipigwa ujue Kiti kitasema nini. Haya mambo tunayasema; kuna mtu juzi nimekutana naye anasema wanashukuru Ethiopia imewafungua macho kwenye mambo ya simu. Tumeyasema haya miaka mitano hamjafungua macho? (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi na kuomba Mheshimiwa Waziri ni mchapakazi vizuri sana, *cash cow* ya Tanzania sasa hivi ni Shirika la Simu la *TTCL*. Kama tumeweza kununua ndege zetu, ni hatua nzuri sana ambayo Serikali imeifanya, ni lazima *tui-bail out TTCL* ili nayo iweze kutoa mchango mkubwa sana wa *GDP* kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wana utawala mpya, kuna *CEO* mpya kijana, kabobeaa, taaluma zake anafanya kazi vizuri, *Chairman* mpya kachaguliwa mzuri, wanachohitaji ni *affirmative action* ya Serikali katika kuwasaidia. Sasa mimi nakuomba Mheshimiwa Waziri tupate majibu mazuri kuhakikisha *TTCL* kweli inasaidiwa na Waheshimiwa Wabunge tuwe mabalози wa *TTCL* ili tuweze kusaidia Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TTCL* ni shirika la umma, *its high time* Serikali ikaipa *exclusive rights* za *TTCL* ku-handle

masuala yote ya *IT* Nchi nzima badala ya kutegemea wakandarasi binafsi. Leo Serikali ina-share asilimia 39 mpaka 40 *Airtel*. Toka Serikali iweke pesa zake *Airtel* hakuna faida yoyote ambayo imekuwa *decreared* na Kampuni hii. Kwa nini sasa Serikali isitoe pesa zake ikaziingiza *TTCL* ili Shirika hili liweze kuboea? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitoa ushauri hapa kuhusu *TCRA* sasa wazibane kampuni za simu kwenye *correction* za kodi za Serikali kwenye *VAT* na *excise-duty* ziwe *displayed* kwenye simu kuonesha kweli kodi ya Serikali inapatikana. Lakini bado napata kigugumizi, hizi *display* kwenye simu zetu hazina *feed* kwenda *TRA*. Kwa hiyo, *TRA* hawana taarifa ya kodi inayokusanywa, huyu mkandarasi ambaye aliyepewa kazi hii ya *TTMS there is something wrong with this thing.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtambo huu ni mali ya Serikali kwa asilimia mia moja, umenunuliwa zaidi ya miaka mitatu/minne iliyopita, leo mkandarasi anauendesha kwa kulipwa *four percent* kwa mwaka. Mikataba mingi kwenye mtambo huu bado inatia mashaka Serikali kukusanya mapato yake. Sasa Mheshimiwa Waziri ndiyo nakwambia Kiti kikikamata mshahara wako usilalamike. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napata taabu, unapoona mtambo wa *TTMSambao* umenunuliwa na Serikali unaendeshwa na mkandarasi *for all this time, why?* Hivi hatuna *local staff?* Kwenye mikataba hakukuwa na *package* ya ku-*train* Watanzania wakauendesha mtambo huu? Na *TCRA* wameonyesha udhaifu mkubwa sana wa kuweza kuingia kwenye *Network Operating Centre* za *operators*. Na kwa vile hawaingii kwenye *NOC* za ma-*operator* hawawezi wakakamata *line* zote na miamala yote ya simu inayopita kwenye mtambo huu. Hamuoni haya Mheshimiwa Waziri tunasema haya miaka mitano? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna teknolojia mpya kila siku zinazaliwa, sasa imekuja *IOT (Internet On things)*, nafikiri unajua. Ni makampuni machache sana wanajua na wanafanya na wame-*introduce software* hii kwenye soko.

Software hii wapewe *ITCL* ili waweze kushirikiana na maeneo ya kukusanya kodi kama vile *TRA*, waingie kwenye mitambo kwenye *operating centres* za makampuni ya simu. Sababu *IOT* ni mtandao maalum ambao mashine hizi zinazungumza wenyewe kwa wenyewe bila binadamu kuingia ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mashine hii ita-sense kuna *transaction* inafanyika hapa itabidi itume ile *message* ipeleke *TRA*. Kwa hiyo, mimi nakuomba Mheshimiwa Waziri kama mnataka mfano wa Ethiopia ambayo ndio juzi mnaambiwa wamefanikiwa, reli ile imejengwa kwa kusimamiwa na Kampuni ya simu ya Ethiopia. Leo Ethiopia inatengeneza vifaa vyya Jeshi vyya kisasa vyenye *standard* ya *NATO*, pesa zinatoka kampuni ya simu. Hivi tunangoja nini na leo Mheshimiwa Rais amezungumza asubuhi? Hivi kwa nini Serikali Mawaziri msimsaidie Rais ambaye ana uchungu wa mapato nchi hii? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mikataba hii ya simu bado tuna-*weakness* kubwa sana. Makampuni haya yamepewa *ten percent deduction* ambayo wana *redeem* kwenye *gross turnover* yao kwenye masuala ya matangazo. Hii lazima ipitiwe upya ipunguzwe. Makampuni ya simu haya yamepewa *three percent* kwenye *management fee*. Mheshimiwa Waziri wewe unajua mambo ya simu, *management fee three percent* ya *turnover* ya kampuni ya simu ni pesa nyingi sana, ndio maana utasikia unaambiwa sasa hivi *your call is not reachable*, yule mtu anayezungumza anazungumza nchi nyingine. Hela inatoka hapa analipwa mtu inakuwa *recorded* kwenye eneo lingine, hebu pitieni tena haya mambo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imenunua ndege, ndege nzuri, mimi ni mtaalamu wa masuala ya ndege. Ndege hizi zina *STOL* (*Short Take off and Landing*) zinaweza zikatua kwenye kiwanja cha mpira. Kwa abiria haiwezekani lakini kwenye dharura kwenye mambo muhimu zinatua na zina-*take off* kwenye kiwanja cha mpira kwa kuweka *flats forty degrees down*. Lakini zina *advantage* vile vile zinabeba

abiria wengi, sabini na sita, *nautical mile* moja kwa gharama ya mafuta kwa kiti inalipa vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *management* mpya, bado kuna tatizo la Serikali kuboresha baadhi ya viwanja vyatia. Ndege hizi zina uwezo wa kuruka *twenty four seven* Mheshimiwa Waziri. *Service* ya ndege ni *hourly bases, item* za ndege zinakwenda kwa masaa, kama ndege hairuki kile kifaa hakitumiki. Sasa kwenye viwanja vyetu vyatia ndege vingi, *unless unambie mmeshafanya maana Bunge liliopita* nililisema hili wakati huo *I think* Naibu Waziri alikuwa Tizeba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kinaitwa *PAPI* (*Precision Approach Path Indicator*) ambayo inamsaidia rubani kutua. Tumenunua ndege za gharama kubwa sana ni lazima tuwe na usalama wa ndege na abiria. (*Makofii*)

(*Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

MHE. MUSSA . ZUNGU: ...Dakika kumi tayari?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Moshi Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko ajiandae.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niwe sehemu ya mchangiaji kwenye Wizara hii. Awali ya yote nitoe pongezi kwa Serikali kwa kazi kubwa sana ambayo inafanyika hasa kwenye suala la miundombinu. Wapo watu ambaao hawaoni kile ambacho kinafanywa na Serikali, lakini tunaipongeza Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ambayo yamefanyika na yanaonekana ni mapinduzi makubwa ya haraka. Tuna upanuzi wa uwanja wa ndege wa kimataifa

pale Dar es salaam. Kwa wale ambao hawajafika wanaona mabadiliko ambayo yapo, ni kazi ambayo inafanywa na Serikali. Kuna ununuzi wa ndege mpya ambazo zinatengeneza sura mpya na historia ya nchi yetu. Ndani ya kipindi kifupi tumepeata ndege ambazo zimeanza kutoa huduma kwa wananchi, lakini baadhi ya watu hawaoni yale ambayo yanafanywa na Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yapo ambayo yamefanywa makubwa, ni ujenzi wa reli ya kati, tayari Mheshimiwa Rais alishaweka jiwe la msingi ambalo linaashiria kuanza kwa ujenzi ambao utatoa unafuu wa maisha ya Watanzania hasa wale ambao ni maskini wa kipato cha chini. Zipo jitihada ambazo Serikali imefanya kama ujenzi wa barabara ambapo karibu kila kona kuna ujenzi wa barabara. Hizi ni shughuli ambazo zimefanywa na Serikali, tuna haki ya kuipongeza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu kutoa shukrani za dhati kwa Mkoa wetu wa Katavi japo yupo Mbunge mwenzangu ambaye amesema hakuna lolote liliofanywa, nasikitika sana. Tuna uwaja wa ndege ambao umejengwa, lengo la kujenga uwanja wa ndege pale Mpanda ni kuweza kukuza utalii ukanda wa Magharibi, kwa maana ya Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanapojenga ule uwanja wanahitaji sasa kui-*promote* mbuga ya Katavi pamoja Mbuga ya Mahale ambayo ipo Mkoa wa Kigoma; ndiyo malengo makubwa ya Serikali. Kwa taarifa tu, ni juzi juzi Watalii kutoka nchi ya Israel wamefika, wana *interest* kubwa sana ya kwenda Mkoa wa Katavi na kufanya utalii wa Ziwa Tanganyika. Sasa kwa wale ambao hawana uelewa hawajui. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Serikali kwa kutengeneza miundombinu, tunayo barabara ya kutoka Sumbawanga kuja Mpanda tayari iliishaanza kujengwa. Tunachokiomba Serikalini ni kuimaliza ile barabara japo mwenzangu aliyetangulia amefika na kuponda na anasema

zile fedha zilizotengwa hajui kazi yake kwa sababu barabara imekamilika. Lakini kwa taarifa tu ni kwamba ile barabara inahitaji mifereji na vitu vingine ambayo vinahitajika kukamilika kwa barabara ndio maana asilimia 80 imekamilika lakini bado asilimia 20. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la bandari. Bandari ni nguzo kubwa sana ya kiuchumi na ni lango kuu la mapato ya Serikali kwa nchi yetu hasa Bandari ya Dar es Salaam. Tunaishauri Serikali ihakikishe inaandaa matengezo ya haraka kuhakikisha upanuzi wa ile bandari unafanywa kwa wakati. Bandari ile ikikamilika itaruhusu kuletwta kwa meli kubwa ambazo ni za kimataifa ambazo zinashindwa kwa sasa kufika kuweka gati pale Dar es Salaam kwa sababu bado miundombinu haijakamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana Serikali ishughulikie ujenzi wa bandari sambamba na bandari zingine, Bandari ya Tanga, Bagamoyo na Mtwara ziweze kujengwa. Vilevile bado zipo bandari muhimu sana za Maziwa makuu. Tuna Bandari ya Mwanza inahitaji iboreshwe, tuna bandari ya Kigoma tunahitaji ifanyiwe maboresho makubwa, tuna bandari ya Karema ambayo Serikali illazimia kwa nia njema kufungua mawasiliano katika nchi ya *DRC* na nchi yetu ili kuweza kujenga bandari ambayo itafanya shughuli za kibashara katika bandari ya Kalemie na bandari ya Karema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba sana Serikali ielekeze nguvu, hii bandari ya Karema imekuwa kila Bunge linalopita inazungumzia ujenzi wa bandari, lakini leo hii tunaiomba sasa Serikali ipeleke nguvu ikamilishe ujenzi wa bandari hii ili iweze kutumika na kuwasaidia wananchi sambamba na ujenzi wa reli ule unaojengwa kutoka Mpanda kwenda Karema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie reli. Reli ni kiungo muhimu sana kwa wananchi, hasa ujenzi wa reli ya katika. Serikali imeazimia na tumeona dhamira kubwa ya Serikali ya kujenga miundombinu ya reli, lakini reli ya katika

maana yake ni reli inayotoka Dar es Salaam kwenda Kigoma. Tunaomba sana Serikali ijielekeze kuhakikisha inakamilisha ujenzi kwa uelekeo wa kwenda Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na matawi yale ambayo yapo katikati kwa maana tawi la kutoka Tabora kwenda Mwanza, tawi la kutoka Kaliua kwenda Mpanda mpaka Karema na tawi jipya ambalo litajengwa kuanzia Uvinza kwenda Msongati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa reli hii malengo yake ni kuchukua mzigo wa nchi ya Congo kwa maana tuchukue mzigo wa Congo upande wa Kusini na upande wa Mashariki ni sambamba na uboreshaji wa bandari ya Kigoma ili iweze kutumika vizuri. Tunaomba sana Serikali iangalie *route* itakayoanza ianzie Tabora kwenda Kigoma, ianzie Kaliua kwenda Mpanda ili kuweza ku-cover kwenye maeneo ambayo kiuchumi ndiyo yana nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la barabara. Tunaishukuru Serikali, barabara sasa hivi zinaanza kujengwa, kutoka Mpanda kwenda Kigoma ilikuwa ni hadithi kwamba huwezi ukaona basi linalotoka Mikoa wa Kigoma likaenda Mpanda au Mbeya, lakini leo hii barabara zinapitika, tunaomba sasa zifanyiwe maboresho. Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutoka Mpanda kwenda Kigoma kwa kuanzia tuna kilometra 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sasa Serikali kama ilivyokuwa imeahidi iandae utaratibu wa barabara itakayoanza Uvinza kuja Mishamo, na hii inayoanza kutoka Mpanda kwenda Mishamo iende sambamba na ujenzi ambaeo upo kwa sasa. Tukifanya hivi tutakuwa tumesaidia wanachi wa Mikoa hii ya Kanda ya Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado tuna barabara ya kutoka Mpanda kwenda Tabora, tunaomba sana Serikali ianzie haraka ujenzi wa barabara hii. Kukamilika kwa barabara hii kutakuwa kumekamilisha mawasiliano ya Mikoa ya Tabora, Kigoma, Katavi na Rukwa, hii ni Mikoa ambayo

kimsingi ilisahafulika sana kwa kipindi kirefu, tunaomba barabara hizi ziwekewe kipaumbele kikubwa kama ahadi ya Mheshimiwa Rais alivyokuwa ameahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mawasiliano, yapo maeneo ambayo mawasiliano nchini bado ni duni hasa Mikoa yetu ya Ukanda wa Magharibi. Nizungumzie suala la Jimbo langu, kuna baadhi ya kata hazina mawasiliano. Tunaomba Serikali ipeleke mawasiliano kwenye kata ya Kabungu, Mpanda Ndogo, kata ya Tongwe ambako kuna makao makuu ya Wilaya ya Tanganyika pamoja baadhi ya maeneo ya Mkoa kama kata ya Ilunde; tunaomba mawasiliano yapelekwe ili wananchi waepuke adha ambayo ipo kwa kupata mawasiliano ambayo ni duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lipo jambo mahsusimba ambalo kimsingi kwa Mbunge ambaye analitakia mema nchi yetu amelizungumzia sana Mheshimiwa Zungu. Suala la kuipa nafasi *TTCI* iweze kumiliki na ikiwezekana Serikali inunue *shares* zile za Airtel ili imiliki yenye, iendeshe na kulisimamia hili Shirika, litaenda vizuri sana na litatoa tija na faida kubwa kwa nchi yetu; tukitengeneza mazingira haya tutakuwa tumewasaidia sana wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho nisisitize kwenye suala la reli Wilaya ya Mpanda na Mkoa wa Katavi kwa ujumla bado kuna wasafiri wengi. Tunamuomba Mkurugenzi mhusika wa Shirika hili aongeze mabehewa ili kuwasaidia wananchi wanaopata shida kubwa sana kwa ajili ya usafiri. Mabehewa yanayohitajika yaende yote, yale ya daraja la tatu, la pili na la kwanza yanahitajika. Kwa hiyo, tunaomba wananchi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda umekwisha Mheshimiwa.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Mabula atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko. Mheshimiwa Kuchauka ajlandae.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie walau maneno machache katika hii Wizara muhimu kabisa juu ya masuala mazima ya miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa maneno machache ya shukrani nikimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara husika juu ya kazi njema na nzuri wanazoendelea kuzifanya katika kuhakikisha suala zima la miundombinu ya barabara, usafiri wa maji na nchi kavu unafanyiwa kazi na unakamilika kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani hizi nafahamu uko upanuzi wa uwanja wa ndege, tumeziona fedha pale Mwanza na niwapongeze sana kwa kutumia zaidi ya shilingi bilioni 18 kwa fedha za ndani na shilingi bilioni tano peke yake fedha za nje. Hii tafsiri yake ni kwamba zoezi hili linaweza kukamilika kwa wakati kama tulivyokusudia tofauti na tungetazamia sana kutumia fedha za nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili niwashukuru kwa upanuzi wa barabaraya kutoka Furahisha kwenda Kiwanja cha Ndege, kwa barabara nne. Ni kitendo kizuri ambacho kitaendelea kuujenga Mji wa Mwanza uendelee kubaki kuwa mji bora na mji wa pili kwa ukubwa Tanzania katika kuhakikisha shughuli zote za maendeleo na uzalishaji mali za kiuchumi zinazoifanya Mwanza kuwa mji wa pili katika kuchangia pato la taifa iendelee kuongeza zaidi ya pale ilipo leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kufikia malengo haya tunayoyafikiria liko suala la barabara za kupunguza msongamano. Mara kadhaa nimekuwa nikisema, lakini nasikitika sana kwa sababu hata vikao vya RCC Mwanza mara kadhaa vimeshafanya mapendekezo zaidi ya vikao

miaka mitatu mfululizo. Vinafikiri kupandisha barabara ya kutoka Buhongwa kupita Lwanima, Sawa, Kanindo kutokea Kishiri – Igoma na Fumagira kama itajengwa kwa kiwango cha lami, barabara yenye urefu wa zaidi ya kilometra 11.8 inaweza kusaidia sana Mji wa Mwanza kufunguka na tukaendelea zaidi kuwa kwenye hali nzuri ya kiusafiri. Lakini hii ni pamoja na barabara kutoka Mkuyuni kupita Igelegele - Tambukareli - Mahina na kwenda kutokea Buzuruga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kwamba mji wa Mwanza unakua, na kama mji wa Mwanza unakua na tunatambua ndiyo mji ambaao uko kwenye kasi ya kuchangia pato la Taifa, sioni tunapata kigugumizi gani kuhakikisha kwamba barabara hizi zinafunguka kwa urahisi ili unapokuza uchumi wa Mwanza unaendelea kuchangia/ kuongeza pato la Taifa kutokea kwenye Mkoa huu ambaao ni Mkoa wa pili kwenye kuchangia pato la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimesema hapa ni ukweli usiofichika kwamba Mwanza ndiyo Mji pekee unaokua kwa kasi zaidi katika *East Africa*. Ukichukua Afrika ni mji wa tano katika Majiji kumi yanayokuwa kwa kasi. Leo hatuangalii kama kuna umuhimu wa kuendelea kuitengeneza Mwanza iendelee kuwa mji wa tofauti na mji ambaao utakuwa unaendelea kutoa matunda bora zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unapoongelea kukua kwa mji unaongezea pia kuongezeka kwa watu. Sasa hivi tunazo barabara mbili peke yake, iko barabara ya Kenyatta na barabara ya Nyerere, hizi ndizo barabara peke yake unazoweza kujivunia leo Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee tu kusema, naamini Mheshimiwa Waziri analitambua hili na tusifikiri hata siku moja kwa fedha za Mfuko wa Barabara hizi zinazokuja kwenye Majimbo na Halmashauri zetu, shilingi bilioni mbili au tatu zinaweza zikasaidia kupunguza msongamano. Fedha hizi ni kidogo, kama zinaweza kufanikiwa sana zitatusaidia tu kutengeneza barabara za kilometra 0.5, 0.2 au 0.3 na kadhalika, hatutawea kufikia malengo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo barabara ya kutoka Mwanza Mjini, nazungumzia barabara ya Kenyatta, kuja kutokea Usagara ambako unakwenda kupakana na Misungwi barabara hii ni finyu sana, lakini yako maeneo upanuzi wake unahitaji gharama kubwa sana. Kwa hiyo, kama hatuwezi kuitengeneza kwa maeneo kadhaa na yenye we ikawa kwa njia nne hatutakuwa tumesaidia sana. Kwa hiyo, niendelee kumuomba Mheshimiwa Waziri, wakati wanakamilisha ujenzi wa njia nne kutoka Furahisha kwenda *Airport* tuifikirie kwa namna nyingine barabara ya Kenyatta, nazungumzia kutoka mjini kati kwenda Mkuyuni - Butimba, Nyegezi - Mkolani - Buhongwa na hatimaye kukutana na Misungwi ili tuweze kuwa kwenye mazingira ambayo yanafanana sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze habari ya bandari. Imesemwa hapa, katika bandari hizi zinazojengwa, Bandari za Mwanza zimesahakuwa ni za kizamani sana. Lakini tukiboresha Bandari hizi za Mwanza, naongelea *South Port* na *Mwanza Port*, tutakuwa tumesaidia kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu mizigo mingi inayotoka Kenya, Uganda wamekuwa wakitumia bandari hizi, lakini hata kukamilika kwa reli ya kutoka Dar es Salaam itakapokuwa imekamilika vizuri bandari hizi bado ni chanzo kikubwa sana. Juzi tumemsikia Mheshimiwa Rais wakati anazungumza na Rais wa Uganda, amezungumzia juu ya bandari ya nchi kavu iliyoko kwenye Kata ya Lwanima.

Mimi nioneshe masikitiko yangu makubwa sana kwa Mheshimiwa Waziri, bandari hii ambayo tayari miaka minne iliyopita toka mwaka 2012/2013 mpaka leo 2017 wananchi kutoka kwenye mitaa minne, nazungumzia wananchi wa Kata ya Lwanima kutoka kwenye mitaa ya Ihushi, Isebanda na Nyabahegi wameshafanyiwa uthamini miaka minne leo lakini bado hawajalipwa hata shilingi moja, Wameendelea kulalamika juu ya bandari ya nchi kavu na mbaya zaidi, hivi ninavyozungumza ziko taarifa kwamba ujenzi wa bandari hii unataka kuhamia Misungwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naomba nimpe taarifa kabisa hapa Mheshimiwa Waziri, wananchi wa Kata ya Lwanima mitaa ya Isebanda, nyabahushi hawatakubali kuona mradi huu unahama unakwenda kwenye kata na wilaya nyingine kwa sababu wamekuwa wavumilivu. Wamesubiri kwa muda wa miaka minne wakiwa na matumaini na Serikali yao kwamba watalipwa fidia na ukamilikaji wa bandari hii ya nchi kavu utaongeza ajira, shughuli za uzalishaji kwenye maeneo yao na tutapata fedha kwa ajili ya wananchi wetu, lakini tutakuwa tumeendelea kuchangia pato kwa Serikali yetu na kuhakikisha mazingira haya yanaboreka zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii lazima tukubali, ndiyo maana nasema mji wa Mwanza leo itakuwa ni ajabu sana, ukitaka kuangalia tuna kilometra ngapi za lami. Mji unaoitwa wa pilli kwa ukubwa haufikishi kilometra 50 za barabara ya lami, hii ni aibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia barabara za kupunguza msongamano zinarundikwa sehemu moja tu zaidi ya kilomita mia na kitu. Hivi leo mkitupa Mwanza hata kilometra 20 peke yake kupunguza misongamano sisi hatutafurahi? Wananchi hawataona thamani kubwa ambayo na wao wanashughulika katika kuhakikisha nchi yao inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo haya mambo ni lazima tukubaliane; kasungura tunafahamu ni kadogo, tuko kwenye jithada za kukusanya mapato lakini hao hao wanaochangia mapato lazima tuwape nafasi na wao wafaidi haka kasungura kadogo hata kwenye kukagawana ukucha, kapaja na kadha wa kadha ili waweze kufikia malengo ambayo wanayokusudia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la fidia naomba litazamwe kwa kipekee sana. Nimelisema kwa haraka kwasababu ya muda lakini haikubaliki wala haiwezi kueleweka miaka minne watu wamekaa wanasubiri fidia halifu wasifikie mwisho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho, mara kadhaa tunaamini vikao vya RCC ndiyo vikao vikubwa na vinapokuwa vinatoa mapendekezo ni lazima yafikiriwe. Haiwezekani miaka minne mnatoa mapendekezo mbali ya barabara za kupunguza msongamano, kutoka Kenyatta kuendelea kwenye maeneo niliyoyataja lakini tulishawahii kupendekeza na hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, pale kwenye Jimbo la Ilemela kwa Mheshimiwa Angelina kiko kivuko kwenye Kisiwa cha Bezi ambako kuna wakazi zaidi ya 600 wamekuwa wanatumia mitumbwi ya kawaida. Hii peke yake inaonesha hali ya hewa wakati mwagine kwenye ziwa si rafiki, kuna kila sababu na kuna kila dalili kila wakati wananchi wanaendelea kupoteza maisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo baadaye walijadili kuhamisha kivuko kutoka Ukerewe ikaonekana haitakuwa sawa kwa sababu viko vingi na kadha wa kadha, lakini tumeahidiwa kupewa kivuko kipyga. Nimuombe Mheshimiwa Waziri aangalie kwa kipekee hiki Kisiwa cha Bezi kiweze kupata kivuko kipyga ambacho kitasaidia kuokoa maisha ya Watanzania zaidi ya 600 wanaoishi maeneo yale ili waweze na wao kuishi kama wananchi wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nilisema nizungumze machache haya kwa sababu naamini sote tunafahamu Mji wa Mwanza ulivyo, na asilimia kubwa hapa kila mmoja anatamani kupita Mwanza. Ni mji mzuri, tukiutengeneza vizuri utakuwa umekaa kwenye mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu akubariki sana, nakushukuru na naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka. Mheshimiwa Omari Kigua ajiandae.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na nianze kwa kuwapa hongera sana Waziri, Naibu Waziri na timu yako

ya wahandisi mlioko Wizarani na wahandisi walioko *TANROADS*, mnafanya kazi nzuri hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitakuwa na machache sana. Mheshimiwa Waziri mimi nataka kukukumbusha tu suala la kisera kwanza. Alikuwa anatukumbusha Ndugu Chenge mchana hapa, ujenzi wa barabara za nchi hii zinahitajika kila mahali sana kabisa na nchi yetu bahati nzuri ni kubwa. Naomba tujirejeshe kwenye sera ya ujenzi wa barabara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishakubaliana kwa mujibu wa Sera ya CCM ya miaka 20 kwamba tutajenga barabara za kuunganisha mkoa na mkoa, tungejielekeza katika maeneo hayo. Kuna mikoa ambayo imeunganishwa tayari na kuna mikoa mingine haujaunganishwa. Na fedha ambazo mnatenga kwenye bajeti ni kidogo mno, sasa sungura mdogo lakini fedha mnatapanya na baadhi ya maeneo kusema kweli hayana umuhimu wa kiuchumi leo. Kuna Mkoa kama Katavi kwa mfano, Mkoa wa Katavi haujaunganishwa na Kigoma, Mkoa wa Kigoma haujaunganishwa na Geita, Mkoa wa Kigoma haujaunganishwa na Shinyanga, Mkoa wa Kigoma haujaunganishwa na Tabora ingawa kuna juhudhi hizo kidogo za kilomita chache, Mkoa wa Kigoma haujaunganishwa na Kagera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Mheshimiwa Waziri wewe umetembea mpaka pale Kasangezi nilikuona siku ile, yale ndio maeneo ambayo yanazalisha chakula kingi. Sisi ndio tunalisha migodi mingi iliyoko ukanda wa ziwa. Naomba mjirejeshe kwenye sera tuweze kufanya haya mambo kwa utaratibu, *otherwise* kila mahali barabara, uwezo huo kwa mara moja hatuna. Mheshimiwa Waziri wewe unajua barabara ya Kigoma - Nyakanazi huu ni mwaka wa 20 barabara haikamiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipande cha kutoka Kidahwe mpaka Kasulu kilometra 50 huu mwaka wa tisa haikamiliki. Sasa nimeona kwenye bajeti yako umetenga

bilioni 19, lakini umesema hizo ni za Kidahwe – Kasulu hizo ni za Kabingo – Nyakanazi na unazungumza kwenye hotuba yako unasema katika fedha hizo hizo ni za upembuzi yakinifu na kuandaa ujenzi wa barabara ya Manyovu – Kasulu – Kibondo – Kakonko, na unasema ni za maandilizi ya ujenzi. Sasa nilikuwa nakuomba hizi shilingi bilioni 19 ni ngapi zinajenga barabara ya Kidahwe tujue Kasulu na ngapi zinatoka Kabingo ziende Nyakanazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sielewi kabisa jambo hili. Hili jambo mkilifanya kisera tutafanikiwa, tutaanza na barabara ambazo zina umuhimu kiuchumi si kujenga kila mahali kwa mara moja. Nilikuwa naomba hilo liwe la kwanza Mheshimiwa Waziri, nikurejeshe kwenye sera na wewe bahati nzuri umekuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya muda mrefu, hili jambo unapaswa kulismamia wewe, hili ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini hapo hapo nilishazungumza na Mheshimiwa Waziri nilikwenda ofisini kwake zaidi ya mara moja, kwamba hii barabara ya Kidahwe - Kasulu haifiki Kasulu Mjini inaishia Nyumbigwa au Kanyani karibu na njia panda ya kwenda Uvinza kwenda barabara ya Katavi. Naomba kwa sababu mkandarasi yuko *site* inakuwa ni vigumu sana kuja kum-*mobilize* baadaye apatikane kwa kilometra nane zile za kuja Kasulu Mjini, itachukua muda mwingine mrefu. Maadamu mkandarasi yuko *site* ingekuwa ni vizuri basi kuwe na *addendum* au nyongeza ya mazungumzo ili aongeze kile kipande cha kilometra nane ile barabara itoke Kidahwe ifike Kasulu Mjini. Hilo naomba sana ulizingatie na liko ndani ya uwezo wako. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nalizungumza, na nisipolizungumza kila mmoja atanishangaa, ni hii reli ya kati. Waziri Mbarawa, reli ya kati msiipotoshe, reli ya kati inatoka Kigoma kwenda Dar es Salaam si vinginevyo. Lakini zaidi ya hayo faida ya reli ya kati hasa *standard gauge* ni kwenda kubeba mzigo mkubwa na mzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri leo hata Mheshimiwa Rais wakati anazungumza na vijana wa *UDOM* hilo kalizungumza kwamba tunajenga *standard gauge* kwa ajili ya kubeba mizigo mizito ili barabara zetu ziwe salama. Sasa *economics* zake ziko hivi, ukitoka Dar es Salaam ukaenda mpaka Tabora, Isaka, Keza, Msongati na Kigali ni mbali zaidi kuliko kutoka Dar es Salaam ukaja Uvinza, ukaenda Msongati, ukaenda Bandari ya Kigoma tofauti yake ni kilometra 700, hizo ni *economics* tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uking'ang'ania hii *route* mnayotaka kuichukua mnakwenda kuinufaisha nchi ya Rwanda, maana Kigali wanataka ile *hub* itoke Isaka pale iende Keza, iende Kigali - Msongati na Msongati ni *South East* ya Burundi. Msongati ambako kuna *deposit* ya *nickel, coal, cobalt* na *copper* iko karibu na Mkoa wa Kigoma, ni *South East*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ile reli ikitoka Msongati – Uvinza ni karibu na Bandari ya Kigoma ni karibu na kwenda Bandari ya Dar es Salaam, hizo ni *economics* tu. Msihangaike na hiyo *route* ya mbali, tuanze na hii *route* ya karibu kwenye mizigo, kwenye mali na andiko la *economics of geography* inatueleza kwamba (na liko pale *TRL*, aliandika Bwana Karavina akiwa Mkurugenzi pale *TRL*) kwamba mizigo ulioko *DRC* ndiyo uatakokofanya reli ya kati ya *standard gauge* iwe na maana kiuchumi, ni tani milioni 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nashangaa eti mnaanza upembuzi yakinifu kutoka Tabora mnakwenda Shinyanga, kubeba samaki? Hizi reli ni za kiuchumi hizi. Dhamira nzuri ya Mheshimiwa Rais ya kujenga reli ya *standard gauge* itusaidie kuokoa na barabara zingine hizi ambazo zinaharibiwa kwa kubeba mizigo mizito. Tafadhalii sana mjielekeze kwenye historia ya mambo haya. Sasa sina haja ya kuzungumzia habari ya reli ya kati kwa sababu nadhani hiyo imeingia, ni *economics* tu. Bashe amezungumza asubuhi, tuma watu wako basi wafanye hizo *cost benefit analysis* tuone ni wapi kuna nafuu ya kiuchumi zaidi na tuna ushindani zaidi kuliko sehemu nyingine, *simple*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa nilisemee kidogo, nimesoma kwenye taarifa ya Kamati kwamba Shirika la ATCL ambalo tumelifufua kwa juhudhi kubwa na kila mmoja ananufaika nalo kwamba si mwachama wa IATA. Sasa swali dogo tu, kwa nini si mwanachama wa IATA na kama sio mwanachama wa IATA maana yake nini kiusalama? Kwa sababu tusifanye mambo tumefumba macho, *exactly!*

Mheshimiwa Naibu Spika, IATA ni Shirika la Usalama la Anga la Dunia, sasa *Air Tanzania* nimesoma kwenye paragraph moja kwamba ATCL sasa sio member wa IATA, kwanini sio member wa IATA? Sasa juhudhi zote hizi, zinakuja ndege kubwa, tunataka kwenda China, twende Marekani, lazima tuwe member wa IATA kwa sababu masuala ya kiusalama na masuala mengine ya anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa nizungumzie; Mheshimiwa Waziri tunaomba utupe *comfort* hii barabara ya Manyovu ambayo unasema ni barabara ya *East Africa* chini ya *NEPAD* ufadhili wa *African Development Bank* inafanyiwa upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kujua, bila shaka kuna *time frame* upembuzi yakinifu unaisha lini na ujenzi huu unaisha lini? Kwa sababu tayari kuna *problem* kwamba tayari kutoka Manyovu kuja Kasulu Mjini nyumba zimewekwa alama "X" kwamba watu watalipwa fidia. Sasa hebu mtueleze, na mimi ningeshauri *strongly* Mheshimiwa Waziri kwamba mna wataalam wengi pale, tuwe na vita ambavyo vinajulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ukifanya upembuzi yakinifu maana yake ni miaka kumi? Lazima kuna *time frame* yake; kama ni miaka miwili ama ni mwaka mmoja tuweze kujua. Ningependa Mheshimiwa Waziri utakapokuja kuhitimisha utueleze barabara ya Manyovu - Kasulu - Kibondo - Kabingo huo upembuzi yakinifu utakuwa umekamilika lini na lini barabara hiyo itaanza kujengwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa kabla kengele haijalia, nizungumzie kipande kidogo hiki cha Kanyani kwenda Uvinza hadi Katavi. Hicho kipande Mheshimiwa Waziri au Naibu wako amepita pale, kile kipande kinatoka Nyumbigwa pale ambapo ndiyo Kanyani zamani, mnaita ni barabara eti ya Nyakanazi kwenda mpaka Tunduma, mimi sielewi hii! Ile barabara inatoka pale Kanyani inakwenda Rungwe mpya, inakwenda Basazi inakwenda Uvinza, inakwenda Mishamo inakwenda Mpanda Stalike. Barabara ile ni muhimu sana kwa sababu ukijenga hii barabara ya Kidahwe - Kasulu kwenda Nyakanazi ile ndiyo *roop ya* kwenda Mkoa wa Katavi, ni barabara muhimu sana inayotuunganisha sisi na Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri tafadhali sana zingatia hayo zirejeshe kwenye sera.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa sababu mmeanza vizuri. Nashukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka atafuatiwa na Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo na mimi nitoe mchango wangu kwenye Wizara hii ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nitangulize maneno yale ambayo umetuasa jana hapa, ukatutahadharisha kwamba tusitumie maneno mengine tukaonekana ni wahaini baada ya baadhi ya Wabunge kutoka Mikoa ya Kusini wanapoeleza habari hizi kwa uchungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo siwezi kuyarudia hayo maneno usije ukonitoa njiani, lakini nataka niwape hadithi moja, hadithi hii nimeipata miaka ya 1980. Rafiki yangu mmoja aliniambia ukijenga nyumba yako usiweke *master bedroom* Kusini; ukiweka *master bedroom* Kusini kuna

28 APRILI, 2017

uwezekano hata ndoa yako isiwe vizuri na familia yako inaweza kubaki maskini. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, akanieleza yafuatayo; anasema ukiangalia ramani ya ulimwengu hebu angalia Visiwa vya *Caribbean* vinaona jua labda kwa wiki mara moja, mara mbili. Ukirudi kwenye ramani ya Afrika hebu angalia Afrika ya Kusini mpaka leo hawajapata uhuru, Rhodesia, Msumbiji hawajapata uhuru ni kwa sababu wapo Kusini. Ramani ya Tanzania, angalia Mkoa wa Lindi na Mtwara, wakati ule Mkoa wa Mkoa wa Lindi na Mtwara ndiyo adhabu ya wafanyakazi, ukipelekwa kule wewe ni adhabu. Akaniambia hii yote ni kwa sababu tuko Kusini. Kwa hiyo, ukichora ramani ya Tanzania angalia Mkoa wa Lindi na Mtwara ilivyo nyuma ni kwa sababu tuko Kusini. Akasema njoo uchore ramani ya Dar es Salaam hebu angalia Wilaya ya Temeke na Kinondoni, ana maana kwamba ukiweka *master bedroom* Kusini utabaki kuwa maskini, ndiyo maana leo mtu wa Kusini akisema anasema kwa uchungu hayo tunayoyasema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, reli inayoongelewa ya Tanga - Moshi, Mjerumani alijenga ile reli kutoka Mtwara kwenda Nachingwea. Wakati ule Mtwara na Lindi tulikuwa na pamba, katani, korosho na karanga ndiyo maana akajenga ile reli. Sisi tulipopata uhuru, tukaihamisha ile reli ikaenda Tanga na m Konge ukahamia Tanga, pamba ikahamia Tanga tukabaki maskini. Tunaposema hamtuhitaji nchi hii tunamaanisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkitaka kuona hilo, je, watu wa Kusini kosa letu kwenye nchi hii ni nini? Hiyo barabara ambayo inaongelewa ya Kibiti - Lindi, mimi wakati nasoma nikiwa *form four* ndiyo barabara ya Kibiti- Lindi imeanza kuletewa pesa. Mwaka 1984, vifaa vilikuja na Nangurukuru vya kumaliza hiyo barabara, hiyo barabara imeshajengwa na Marais wangapi? Wanne, hiyo iko Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1987 natoka Dodoma nakwenda Singida, barabara ni ya vumbi, lakini

barabara ya Singida na ya Kibiti - Lindi ipi imeanza kuisha? Mnataka tuseme nini? Naomba Serikali ya Awamu ya Tano mfungue Mikoa ya Lindi na Mtwara. Muufungue Mkoa wa Lindi na Mtwara kwa barabara na kwa mawasiliano, hapo mtakuwa mmetutendea haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nangurukuru-Liwale; Nachingwea - Liwale na Liwale - Morogoro zimeshaongelewa sana sina haja ya kuzirudia, lakini kwa sababu mimi ndiyo mwenye hizo barabara wanasesma chereko chereko na mwenye ngoma. Wabunge wengi hapa mmesema tuende kwenye sera, Mbunge aliyepita amesema tuende kwenye sera, kama tumeamua kuunganisha Mkoa hadi Mkoa basi nasi mtuunganishe na Morogoro mtungaanishe na Ruvuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, njilelekeze kwenye Wilaya ya Liwale. Walio wengi hapa wakismama wanasesma Wilaya zao mpya, mikoa mipyä, Wilaya ya Liwale ina miaka 42. Sasa kama kuna mtu Wilaya yake mpya anadai barabara na sisi ambao tuna miaka 42 hatuna barabara tuseme nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Liwale haina mawasiliano ya simu, haina mawasiliano ya barabara na leo hii Liwale hapa ninapoongea siwezi kwenda, barabara hakuna na nikienda kule wanaweza wakanipiga hata mawe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upande wa mawasiliano ya simu. Namuomba Waziri atuletee mawasiliano, kata zifuatazo ili kuweza kupata mawasiliano ya simu ni lazima uende zaidi ya kilometra tano, 10 mpaka 12. Kata ya Mpigamiti, Kikulyungu, Kimambi, Lilombe, Mlembwe, Mkutano, Ngunja, Ngongowele, Ngorongopa, Pengere, Makinda, Mirui, Mikunya, Naujombo, Nahoro, Mtawango, Makololo na Gongowele hizi zote hazina mawasiliano.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

28 APRIL, 2017

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kata ya Mpigamiti ndiyo kata anayotoka huyu anayeongea sasa hivi. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sana Serikali ya Awamu ya Tano, hebu muifungue Liwale na Lindi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nikiwa kwenye Kamati, niliambiwa vigezo vyta barabara kupata lami wakasema magari lazima yafike 300, nikawaambia kama kigezo ndiyo hicho, Liwale hatutapata barabara ya lami mpaka Yesu arudi. Kwa sababu karavati walizojenga kwenye hiyo barabara magari makubwa hayaendi na tayari wameshapunguza magari. Mfano, masika kama sasa hivi watu wanazunguka kuititia Lindi, hiyo barabara itafikia magari 300 lini? Siyo kweli kwamba hii barabara haiwezi kufikia magari 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri naomba nikuambie barabara ya Nangurukuru – Liwale ukiipa lami, hakuna msafiri atayekwenda Masasi na Tunduru, atakayepitia Lindi au Mtwara lazima wapitie Liwale kwa sababu ndiyo *shortcut*, lakini leo hii Liwale inaonekana iko kisiwani kwa sababu hatuna barabara.

Kwa hiyo, barabara hii ni barabara ya kiuchumi siyo kweli kwamba ni barabara ya huduma. Liwale tunalima korosho, Mkoa wa Lindi ndiyo tunaongoza, tunalima ufuta, tunalima viazi. Sasa kama siyo uchumi huu ni kitu gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nirejee kwenye ubora wa barabara, juzi tulipokuwa kwenye Kamati tulikagua barabara. Mimi nilisikitika sana yule *engineer alinieleza* barabara ile haina hata mwaka imeanza kuweka *crack*, namuuliza anasema unajua hapa wali-*estimate* vibaya kumbe *level* ya maji (*water table*) ile kwamba walikadria iko juu kumbe iko chini sana, kwa hiyo, barabara imebomoka wanarudia. Nikamwambia hawa wanaofanya *feasibility study*, sijui upembezi wa kina, wanafanyaaje?

28 APRIL, 2017

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninavyofahamu kila mita 50 panachukuliwa udongo wanafanya *sampling*, wanapeleka maabara kupata historia ya hiyo barabara. Ndiyo maana tunashindwa kuwakamata wakandarasi mara nyingi makosa yanakuwa siyo yao. Haya mambo ya upembuzi yakinifu, upembezi wa kina, mtu yuko ofisini anapiga simu tu, eeh bwana hiyo barabara kutoka mahali fulani, kuna mto gani hapo? Huo mto ukoje? Anachora tu, eeh, jamani tuende kwenye *field!* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haingii akilini mtu aniambie kwamba ile barabara pale maji yanafoka ndiyo maana barabara haidumu, hukuyaona? Hapa tunapoteza pesa bure, lakini tatizo siyo wakandarasi, tatizo kubwa liko kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, wataalamu wanabaki ofisini wanafanya upembuzi yakinifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa tunazungumzia upande wa bandari. Nchi hii ni ya ajabu sana, leo hii hatuna hata lengo kusema kwamba kwenye nchi yetu hii ni mizigo tani ngapi tupitishe majini na mingapi tupitishe kwenye reli. Leo hii Mtwara kuna bandari lakini hii bandari haitumiki. Juzi hapa tumepata shida na mazao ya korosho, Mtwara kumejaa korosho maghala yote, meli hakuna, hii bandari mbona hatuitumii? Tumerogwa na nani sisi? Tatizo liko wapi? Hakuna nchi ya ajabu kama hii. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Kusini hiyo.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii nchi hii bado inasafirisha mizigo mikubwa kwa malori, halafu bado tunawalaumu wakandarasi wanajenga barabara chini ya kiwango, hii si kweli, haiwezekani! Tunayo bandari ya Tanga mwambao wote ule Mtwara, Lindi, Dar es Salaam, Tanga, Bagamoyo bado tunasafirisha mizigo kwa magari, hii ni aibu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kwamba umefika wakati Serikali wapange kwamba tunataka tusafirishe mizigo...

28 APRIL, 2017

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Nikidhani unataka kuunga mkono hoja ili Liwale itembelewe. Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Ngonyani na Mheshimiwa Omary Mgumba ajiandae.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye amenijalia kusimama katika Bunge hili Tukufu ili niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia ningependa nitoe shukrani zangu za dhati hasa kwa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali yake ya Awamu ya Tano kwa jitihada kubwa sana ambazo wamechukua hususan katika ujenzi wa *flyover*, ujenzi wa barabara na *standard gauge*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa kwamba nchi hii sasa inakwenda kwenye maendeleo ambayo Watanzania wote tulikuwa tunayatarajia ndiyo maendeleo tunayoyataka. Nina imani kwamba siku atakapomaliza muda wake Watanzania watamkumbuka, kama siyo sisi watoto wetu basi watakuwa wanakumbuka historia ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi ningeomba sasa nianze kuzungumzia suala la barabara, barabara nitakayozungumzia ipo katika kitabu hiki cha hotuba yako Mheshimiwa Waziri, ukurasa 42 unazungumzia barabara hii ambayo inaanzia Handeni, inapita Kibirashi, Kijungu, inaenda Kondoa, Nchemba hadi Singida. (*Makofii*)

28 APRIL, 2017

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii inaunganisha Mikoa Minne, inaunganisha Mkoa wa Tanga, Mkoa wa Manyara, Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Singida. Mwaka jana nimezungumzia sana barabara hii. Barabara hii ina urefu wa kilometra 460 na ipo katika llani ya Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Waziri, nimeshakuja ofisini kwako kuizungumzia barabara hii, nimeona mwaka huu katika kitabu chako katika hotuba hii umesema mnatafuta fedha, lakini katika kupitiapitia nikaona mmetenga shilingi milioni 500. Sasa sijajua shilingi milioni 500 ni kwa ajili ya kufanya kitu gani. Ningependa wakati una-*wind up* niweze kupata maelezo ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kwa nini tunahitaji barabara ya kiwango cha lami. Wilaya ya Kilindi ndio Wilaya peke yake ambayo haina barabara ya kiwango cha lami, lakini Wilaya ya Kilindi ina shughuli nydingi za kiuchumi, kuna ufugaji, kilimo, madini na barabara hii ni *shortcut* sana Mheshimiwa Waziri kwa mtu anayetokea Handeni akipita Kilindi anakuja kutokea Gairo hapa kwa Mheshimiwa Shabiby. Sijaelewa ni kwa nini mliamua kutengeneza barabara ya kupitia Turiani na kuiacha hii inayotokea hapa Gairo. *Anywaysiwezi* kulaumu kwa sababu zote hizo ni barabara za Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokiomba Mheshimiwa Waziri, tafadhalii sana langalieni barabara hii, wananchi wa Kilindi wanahitaji mawasiliano kwa sababu kujenga katika kiwango cha lami maana yake mtakuwa mmeinua maisha ya wananchi wa Kilindi, Mkoa wa Tanga na Tanzania kwa ujumla. Utaruhusu upitaji kwa rahisi kwa watu wanaotoka Manyara, kwa watu wanaotoka Tanga kufika Dodoma ambako ni makao makuu ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba Mheshimiwa Waziri ufanye ziara uje uangalie ni nini kinachoendelea kule. Sasa hivi tuna kiwanda cha *tiles* kinachojengwa Mkuranga. *Material* yote yanatoka Wilaya ya Kilindi, yanapita magari mazito sana takribani tani 40 kwa siku zaidi ya malori 100. Barabara ile iko katika kiwango cha vumbi, barabara

28 APRILI, 2017

inaharibika na kipindi hiki ni kipindi cha mvua. Nikuombe Mheshimiwa Waziri najua wewe ni msikuvu, muadilifu, utaiona barabara hii, tutafutie wafadhili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hiyo naomba nizungumzie kilomita tano Makao Makuu ya Wilaya, narudia kusema tena, wananchi wa Kilindi wana kilio, mwaka jana nilikuomba tunaomba tujengewe kilometa tano ukatutengea hela ndogo sana shilingi milioni 150 ambazo hazitoshi hata kuwa na nusu kilometa, mwaka huu nimepitia kitabu hiki nimeona umetenga shilingi milioni 120. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri, ukizungumza na wataalam wanasema kiasi hicho hakitoshi. Najua mahitaji ni mengi Watanzania wanataka barabara lakini nasi wananchi wa Kilindi tunahitaji, ungeanza hata kilometa mbili tu, kwa sababu inabadilisha hata sura ya mji. Ninaomba Mheshimiwa Waziri uje makao makuu ya Wilaya uangalie hali halisi au mtume Naibu Waziri baada ya bajeti hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ningependa kuzungumzia barabara ambayo inaanzia makao makuu ya Wilaya inapita Kikunde inaenda mpaka Gairo. Barabara hii Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne aliahidi kujenga katika kiwango cha lami, wakati huo Mheshimiwa Rais sasa hivi John Pombe Magufulsi alikuwa ni Waziri wa Ujenzi aliahidi kujenga. Ninakuomba hebu iangalie katika taratibu zako baadaye ni namna gani mnaweza kujenga barabara hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni suala la minara ya simu. Leo asubuhi nilipata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, kuna matatizo ya mawasiliano Wilaya ya Kilindi, mawasiliano ni tatizo sana. Tunayo kata moja inayopakana na Simanjiro inaitwa kata ya Saunye kule kuna mbuga ya wanyama, kuna wafugaji wengi sana hawapati mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naamini Mheshimiwa Waziri mawasiliano ni biashara, hakuna sababu Wabunge tusimame hapa kulalamika. Ni juu ya makampuni

kutafuta wateja ili waweze kupata mapato, mapato yasaidie Serikali. Nakuomba Mheshimiwa Waziri uchukue Kata zifuatazo kwa ajili ya kuweka minara ambazo ni kata ya Tunguli, Saunyi, Misufuni na Kilindi Asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa Mheshimiwa Waziri kulichukua hapa ni suala la wakandarasi. Wizara inachelewa sana kuwalipa wakandarasi. Unapochelewa kumlipa mkandarasi maana yake una-*entertain* gharama kubwa zaidi kwa mfano mradi ulikuwa na shilingi billioni kumi, ukichelewesha mradi ule kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja maana yake unaruhusu gharama ya mradi iwe kubwa zaidi. Mimi naomba sasa muwe mnafanya tathmini ya muda, mnayo miradi mingi sana, lakini msianzishe miradi mingine mipya bila kuangalia ile ya zamani, nadhani hapo mtakuwa mmepunguza gharama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia sisi Kamati yetu tulienda katika barabara inayopita Turiani kupita kwa Mheshimiwa Murad, mkandarasi pale muda umepita sana na gharama anazodai ni mara mbili ya gharama ya mradi ule. Kwa hiyo, nikashauri Mheshimiwa Waziri muwe mnafanya tathmini sana kuangalia gharama za hii miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la reli ya Tanga. Waheshimiwa wengi wamezungumzia reli ya Tanga, wapo wazungumzaji waliosema kwamba ni ya muda mrefu sana na sisi watu wa Mkoa wa Tanga tunahitaji *standard gauge*. Reli ile inayotoka Tanga inaenda Moshi, inapita Kilimanjaro hadi kwenda Musoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Tanga tuna Kiwanda cha Saruji, saruji ile inayotoka Tanga ukiipeleka kwa njia ya *standard gauge* maana yake utaruhusu iuzwe kwa bei ya kiwango cha chini sana. Mimi nina uhakika kwamba mkishamaliza utaratibu wa kufika mpaka Mwanza na Kigoma basi mtarudi na Mkoa wa Tanga. (*Makofii*)

28 APRIL, 2017

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo machache naomba nikushukuru, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Stephen Ngonyani atafuatiwa na Mheshimiwa Omari Mgumba, Mheshimiwa Yahaya Omar Massare ajiandae.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayofanya, vilevile nisiache kumpongeza Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Mameneja wa Mikoa hasa Mikoa wangu wa Tanga kwa kazi nzuri wanazozifanya. Usiposhukuru kwa kidogo, hata kikubwa utakachopewa hutashukuru. (*Makof!*)

Vilevile Mheshimiwa Waziri wangu naomba nikwambie kitu kimoja ambacho kiko ndani ya msingi wangu mkubwa kwamba safari hii nitashika Mshahara wako, nasema haya kwa sababu zifuatazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka mwaka 2010 Barabara ya kutoka Korogwe kwenda Bumbuli hadi Soni, iko ndani ta llani ya Uchaguzi, barabara hii ilitengewa kwamba itawekwa lami, lakini mpaka mwaka jana barabara hii haikutengewa pesa ya aina yoyote, mwaka huu imetengewa milioni 130 tu. Mheshimiwa Waziri hata bubu wakati mwingine ukimzidia anasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatupendi sana kuwa tunaongea sana humu ndani, kubishana na viongozi, lakini inapofika mahali tunaponyamaza sana tunaonekana watu wengine hatusemi. Sasa kwa mtazamo huu safari hii nataka niwaambie ukweli kwamba nitashika shilingi ya Waziri. Kwa sababu tumevumilia mno, mahali pengine kote kunatengenezwa barabara, lakini barabara yangu miaka

28 APRIL, 2017

saba. Na miaka saba hii sioni sababu yoyote ambayo inazuia, kila kitu kimefanyika! Niliona niliseme hilo mapema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya lami ambayo iliahidiwa na Serikali ya Awamu ya Nne, kilometra 1.1 katika Mji wa Mombo, lakini barabara hii mpaka leo wala sijui kwamba mawazo yao hasa ni nini. Mpaka leo hii haioneshi kwamba inaweza kujengwa kiwango cha lami na vilevile awamu zote mbili zimesema itajengwa kiwango cha lami. Naomba Waziri mhusika muiangalie, sisi hatupendi sana tuwe watu wa kubishana, sisi ndiyo wenyewe Serikali, tunataka tuisaidie Serikali, pale mahali ambapo tunaona inakwenda tofauti tuunge mkono ili mtusaidie. Sasa tukinyamaza na ninyi wenzetu mnatuona kwamba hatuongei haileti maana nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni bandari ya nchi kavu; katika awamu iliyopita tulikuwa tunasema kwamba katika Mkoa wa Tanga kutakuwepo na bandari ya nchi kavu pale Korogwe, hili mpaka leo imekuwa kama kizungumkuti, haioneshi dalili wala hakuna dalili yoyote, tunayoisikia hapa ni reli ya kati tu na bandari nyingine, Bandari ya Tanga na Mtwara tunaziona kama vile zinasahaaulika. Mkifanya namna hii tunakuwa wanyonge kwa sababu ukitaka kuichukua Tanga lazima utaje Mkoa wa Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mara, Mwanza pamoja na Manyara hii ukijumlisha inatoa neno la Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika reli, reli ambayo ni ya mwanzo kabisa, mojawapo ni reli ya Mkoa wa Tanga. Nashangaa inakuwa ni vitu tofauti, tunapigwa chenga tu, sijui kwa sababu hatuongei au kwa sababu tumenyamaza sana. Naomba Serikali ituangalie, unaposema kwamba mpango wa biashara, uchumi, uchumi hauletwi na Mikoa ya Kati peke yake ni Tanzania nzima lazima kuwe na uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu hizi barabara za mkoa. Barabara za Mkoa Mameneja wa Mikoa wanafanya kazi nzuri sana, lakini wakandarasi wanatumiza.

Kuna sehemu inakuwa *heavy grading* ambayo ni lazima uchimbue barabara halafu ushindilie, lakini cha kushangaza kuna sehemu hawafanyi hizo kazi na hela wanapewa, halafu kibaya zaidi ni kwamba, hela ambazo zinatengwa na Serikali baadae unaambiwa zimechukuliwa tena kwenye Wizara zinapelekwa sehemu nyingine. Hivi maana yake mnaposema hela zinakwenda kwenye mikoa, halafu Wizara inakuja inazipunguza pesa zile na barabara zinakuwa zinaharibika, hivi mkifanya namna hii tutakuwa tunafika mbali? Naiomba Serikali kama tatizo hili lipo naomba litekelezwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwenye barabara yangu ya kutoka Korogwe kwenda Maguzoni - Muheza imeondolewa hela. Barabara ya kutoka Korogwe kwenda Maramba - Daruni mpaka njia panda ya kwenda Mombasa, wameondoa fedha. Sasa hivi mvua imenyesha barabara illijengwa vizuri, lakini imefumuka yote kwa sababu malengo ya kutengeneza barabara hayakufanyika. Naomba sana Serikali iangalie suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo linatusumbua sana ni mawasiliano. Katika Tanzania sehemu ambayo inatoa madini nyeti sana ni katika kata ya Kalalani katika kijiji cha Kigwasi lakini sehemu nyingine zote kuna mawasiliano, hapa pia ni Mbuga ya Mkomazi na hapa pia ndipo kunakotoka madini ya aina mbalimbali. Tumeongea, nimekuja nimeongea hapa Bungeni, yanaingia kwenye sikio hili yanatokea sikio hili. Sasa sipendi sana kubishana na Serikali kwa sababu kazi kubwa mmeshatufanyia, hizi ndogo ndogo ni kurekebishiana tu ili tuone kwamba namna gani mtatekeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wachangiaji wenzangu wameongea sana, lakini ukweli mnatuonea sana watu wa Tanga hasa Bandari ya Mwambani. Kila mwaka mnaongelea suala la bandari, mtu anatoka Tanzania anakwenda kutoa mizigo Mombasa anaacha kwenda Tanga kwenda kutoa mizigo wakati ni bandari nzuri. Mtu anaondoka anakwenda anaacha Bandari ya Mtwara yenye

28 APRIL, 2017

kina kirefu, mtu anakwenda Mombasa. Kwa nini jamani? Tuna makosa gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mkigawa, hata kama kasungura kadogo kama alivyoongea Mbunge mwenzangu wa Mwanza lakini tugawane kidogo, mnapotugawia kidogo nasi tunakuwa na nguvu. Mkinyamaza sana mwisho wake tutakuwa tunasema kwamba hawa labda hatuna imani, lakini mimi nina imani sana na Serikali ya Awamu ya Tano kwa haya mnayofanya, kwa sababu leo pia Rais amenifurahisha sana baada ya kusema yeye hataki vyeti feki, anataka mtu elimu yake aiseme ile. Mimi elimu yangu ni ya darasa la saba na ninaomba muendelee kuichunguza hivyo hivyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna minara pale kwangu kwa Mkole katika kata ya Chekelei, kijiji cha Bagai, mnara huo umefungwa toka mwezi wa kwanza mpaka leo hii haujafunguliwa sijui sababu ni nini? Kuna kata ya Kizara mmejenga mnara mzuri sana lakini mawasiliano yake yanakuwa ni hafifu.

Naomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wako, mmenisaidia sana katika mambo yangu ya kimsingi katika Jimbo langu hasa nilipokuwa naumwa. Mmefanya kazi kubwa sana ya kunipelekea fedha kwa kupitia Meneja wa *TANROADS*wa Mkoa wa Tanga na barabara zangu zinapitika vizuri, sitapenda kuwaangusha, lakini msituangushe mahali ambapo tunawaamini kwamba ni watendaji wazuri wa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya machache naunga mkono hoja, ujue usipokuja na majibu mazuri hiyo siku ya kuidhinisha ninatoa shilingi yangu mpaka uniambie barabara ya kutoka Korogwe - Kwashemshi - Dindila - Bumbuli - Soni, sasa ijengwe kiwango cha lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

28 APRIL, 2017

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Omary Mgumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Martin Msuha.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami nitoe mchango wangu katika Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Wenzangu wengi wametoa pongezi kwa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi Awamu ya Tano. Na mimi nitakuwa ni mnyimi wa fadhila kama sitashukuru kidogo walichonifanyia katika Jimbo letu la Morogoro Kusini Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, kwa nia ya dhati kwa mara ya kwanza ukiondoa ile Barabara ya lami ya Taifa, Dar es Salaam - Morogoro ya kwanza tangu miaka 50 ya Uhuru ndiyo Dkt. John Pombe Magufuli alipokuja kuzindua Uwanja wa Ndege wa Kijeshi wa pale Kizuka, ametuzawadia kilometra zaidi ya 15 kutuvekeea lami. Tunamshukuru sana nasi tunaanza kuona matunda ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa mara ya kwanza kuwa na barabara la lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Uongozi wa TANROADS Mkoa wa Morogoro ukiongozwa na *Engineer Dorothy Mtenga* na timu yake nzima, kwa usikivu mkubwa ambapo tulipopeleka maombi yetu ya kupandishwa barabara kutoka Wilaya kwenda Mkoa, barabara ya Ubena Zomozi - Ngerengere - Tununguo mpaka Mvuga, mwaka huu imepandishwa na nimeiona na imetengewa fedha. Nawashukuru sana huu ndiyo utekelezaji llani ya Chama cha Mapinduzi jinsi tulivyoahidi inaonekana namna inavyotekelawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni ombi kuhusu barabara hii ya Ubena Zomozi kwenda pale Kizuka ingawa cha kupewa hakina nyongeza na hii ilikuwa ni zawadi mahsus kwa Mheshimiwa Rais kwa Jeshi letu, kwa walinzi wetu wale wa Kizuka, walinzi wa mipaka yetu, kama mnavyofahamu

Mheshimiwa Waziri pale Kizuka tuna kambi nne, pamoja na ile ya Sangasanga ya wale wazee wa kazi mliowaona pale wakitoa burudani juzi pale uwanjani. Sasa wale barabara yao inaanzia Mdaula mpaka Sangasanga, ombi langu kwako na ninafikiria Serikali iko hapa, umfikishie Mheshimiwa Rais, tunaomba hawa nao ni wapiga kura wangu wasione kama wametengwa, basi hizi kilometra zao saba zingewekewa lami kama walivyowekewa wenzao wa Kizuka, litakuwa ni jambo jema sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo niende kwenye barabara. Kama tulivyosema barabara ya kwanza ya lami ndiyo hiyo itakuja kilometra 15 kutoka ahadi ya Rais, lakini kuna barabara muhimu kuliko yote ya Bigwa - Kisaki. Ni barabara ambayo kila wakati tunaiongelea hapa lakini bahati mbaya siaiona humu. Barabara hii ni muhimu sana kwa sababu inapita katika tarafa nne za Jimbo hilli, inapita tarafa ya Mkuyuni, tarafa ya Matombo, tarafa ya Mvuha, tarafa ya Bwakila, lakini cha muhimu barabara hii inakidhi sera. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii inaunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Pwani kwa upande wa Rufiji. Kutoka Kisaki kwenda Rufiji ni kilometra 60 tu na kutoka Morogoro Mjini kwenda Kisaki kilometra 170. Kwa hiyo, utakuwa umefika Rufiji kwa kilometra 230, itakuwa ina mchango mkubwa sana kitaifa badala ya mtu anayetoka Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kati, Kanda ya Nyanda za Juu, Morogoro yenyewe akienda Mtwara analazimika mpaka atembee kilometra 200 kwenda Dar es Salaam, baadae atoke 170 kwenda Kibiti mpaka Rufiji, ndiyo hapo tutakuwa tumeokoa gharama kubwa sana kwa kutengeneza barabara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaokoa msongamano Dar es Salaam, tutaokoa gharama za usafirishaji pia barabara hii ikitengenezwa tutarahisisha kufika katika Mbuga yetu ya Selous kupitia Kisaki kwa ukaribu zaidi kwa hiyo, tutaongeza mapato ya kiuchumi kupitia utalii. Kwa hiyo, naomba sana barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami kama

ilivyoahidiwa tangu 2005 na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete, akarudia 2010 pia 2015 na nishukuru ipo kwenye ilani, basi utekelezaji ufanyike haraka iwezekanavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kwenye barabara hii ya Bigwa - Kisaki, ningeomba hawa waliopisha barabara waliokuwa kwenye hifadhi, wamefanyiwa tathmini muda mrefu sana Mheshimiwa Waziri. Sasa ni wakati muafaka wakalipwa fidia mapema ili ikifikia wakati wa kutengeneza hiyo barabara basi iende kwa haraka sana. Naomba ukija kufunga mjadala wako ni vizuri tupate *commitment*ya Serikali tujue ni lini watu waliopisha barabara watalipwa fidia zao kwa sababu mpaka sasa hivi, zaidi ya miaka mitano wamekaa hawafanyi uendelezaji wowote, hawafanyi kitu chochote. Kama unavyoja nyumba yoyote ikiwa karibu na barabara inakuwa ni nyumba ya biashara siyo ya makazi, watu wana-frame zao, watu wana viwanda vyao vya matofali, vyote vimesimama kwa kusubiri kupisha hii barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu niende kwenye upande wa reli. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali nzima ya Awamu ya Tano kwa ujenzi wa reli ya kati. Hii reli ya kati ina manufaa makubwa sana katika Mkoa wa Morogoro, hususan katika Jimbo langu. Inapita Kidunda, Ngerengere, Mikese pamoja na Mkulazi. Kwa hiyo, itakuwa na manufaa makubwa sana kiuchumi, itaturahisishia gharama za uzalishaji, gharama za usafirishaji kwenda chini, matokeo yake itakuwa faida kubwa kwa wananchi wa Morogoro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu katika hili, kuna watu ambao wameathirika na maendeleo haya ya reli ya kati. Kuna watu wamekaa zaidi ya miaka 20 leo wamepewa *notice* wanatakiwa wahame ndani ya mwezi mmoja. Mheshimiwa Waziri, hata kama huyo mtu ahame ndani ya mwezi mmoja atapata wapi nafasi hiyo ya kwenda kujenga, muda ndani ya mwezi mmoja apate makazi. Ombi langu la kwanza wangeongezewa muda hata kama miezi sita, ili wapate nafasi ya kujenga kule ambako wanaenda, la pili

kwa wale waliokaa zaidi ya miaka 12, Shirika la Reli lilikuwepo walikuwa wanaangalia, watu walishajua pale mahali pao, leo kuja kumhamisha mtu huyu bila chochote kama sheria inavyosema kwamba mtu akikaa zaidi ya miaka 12 mahali hapo anahesabika ni pake. Ni vizuri mngewapa kifutia jasho angalau waende kurudisha pale walipokuwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, linguine ni kuhusu mawasiliano. Kuna kata zangu zaidi ya tano kwenye tarafa ya Ngerengere, kata ya Maturi, kata ya Mkulazi, kata ya Seregete, kata ya Tununguo na kata ya Kibuko, tarafa ya Mkuyuni, zote hazina mawasiliano, zaidi ya vijiji 30. Nakuomba sana hivi vijiji tuvipatie mawasiliano hasa huku Mkulazi kwenye mradi mkubwa unakotekelizwa sasa hivi na wawekezaji *NSSF* kwa ajili ya kiwanda cha sukari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika mawasiliano niongelee kuhusu *TTCL*. *TTCL* ni shirika la kwetu, nilikuwa nasikia kuna baadhi ya wenzetu hapa walikuwa wanafananisha na shirika la huko nje. Jamani hata hayo mashirika yanayosifika huko Ethiopia kwanza yaliwezeshwa mtaji na Serikali yao, pili, yalilindwa na ushindani kwa mashirika mengine kwa muda mrefu mpaka yalipokaa sawasawa ndiyo wakaruhusu mataifa mengine au mashirika mengine kwenda kufanya bisahara pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni vizuri kwa sababu shirika hili ni letu, kuititia Serikali, Serikali ni vizuri ikaongeza mtaji kama inavyofanya kwenye *ATC* ili shirika hili *li-take off* baada ya hapo na ikiwezekana hata huu mtaji tuwape kama *loan* ili kuwapa uwajibikaji hawa wafanyakazi wa *TTCL* wajue kwamba tumekopeshwa na Serikali, ni hela za Watanzania zinapaswa zirudishwe kwa wakati na hata kama siyo kwa faida, lakini zirudi Serikalini zije zifanye kazi nyingine. Lakini kuwaacha kwenye ushindani huu mkubwa, tumeona hapa mashirika mengine yamekuja kuomba huku mtaji, tukiwaacha hawa *TTCL* washindane na *ma-giant* hao sasa hivi hatuwezi kuwatendea haki na halitawezwa kwenda mbele sana. (*Makofi*)

28 APRILI, 2017

Mheshimiwa Naibu Spika, pili pia kwenye *TTCL*, wanatoa huduma zinatumika na Serikali na taasisi nyingine na sisi wengine, ni vizuri tukawalipa zile ankara zao. Mara nyingi mashirika mengi ya Serikali yanakufa ni kwa sababu hatuyaendeshi kibiashara, tunayaendesha kiserikali kama vile yanatoa huduma. Tunatumia huduma zao, wakati wa kulipa hatulipi, baadae madeni yanakuwa makubwa, shirika linashindwa kujiendesha kibiashara.

Naomba Serikali yangu ni vizuri kama tunadaiwa na *TTCL* ili tuipe nguvu i-take off hapo ilipo tuilipe madeni yao ili waweze kusimama na kwenda kwenye ushindani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kuhusu *TTCL* ni kwamba sasa...

(Hapa kengele lilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Martin Msuha atafuatiwa na Mheshimiwa Saul Henry Amon, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali ajiandae.

MHE. MARTIN M. MSUHA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kupatiwa nafasi ya kuweza kuchangia hoja iliyopo mezani ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Nichukue fursa hii kuungana na Waheshimiwa wenzangu wote waliotangulia kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa wanayoifanya, ni kazi ambazo zinaonekana, sitahitaji kurudia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niipongeze Serikali kwa kutupatia mradi wa barabara ya kutoka Longa hadi Kipololo, pia awamu nyingine Kipololo hadi Litovo kwa kiwango cha lami kuititia ufadhili wa Umoja wa Ulaya (*European Union*).

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii inazo changamoto nyingi sana, barabara hii haiendi kwa *speed* ambazo zilioneshwa kwenye mikataba na makubaliano. Kipande cha kwanza cha kutoka Longa hadi Bagamoyo, ambayo iko kata ya Kipololo mkataba wake ultakiwa ukamilike tarehe 30 Septemba, 2016 bahati mbaya hadi ninavyosema hakuna hata futi moja iliyoweza kutiwa lami mpaka sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kipande cha pili cha kutoka hapo kijiji cha Bagamoyo kwenda Litovo baada ya kufanya mabadiliko ya mkataba walitakiwa Wakandarasi wamalize kazi ile tarehe 31 Januari, 2017, bahati mbaya hadi nasimama hapa leo hii, barabara hii katika vipande vyote viliwili haijaweza kuwekewa hata nukta moja ya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa barabara hii sijaiona kwenye kitabu cha mawasilisho ya Mheshimiwa Waziri, sasa sijajua iko mpango wa nje ya hii programu iliyoletwa ya 2017/2018 kwa mwendelezo au vinginevyo nitaomba tupate ufanuzi baadaye ili iturahisise pia ufuatiliaji wa ujenzi wa barabara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu walitangulia pia kuchangia asubuhi Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi lakini pia kupitia swali la nyongeza Mheshimiwa Mpakate juu ya barabara inayotoka Kitahi kwenda Lituhi kupitia kwenye Mgodi wa Makaa Ngaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi si tu wa Mbinga lakini pia uchumi wa Taifa letu kwa ujumla. Barabara hii ya Kitahi - Lituhi ni barabara kubwa sana ikizingatia na upanuzi unaoendelea kufanyika kule kwenye makaa ya mawe Ngaka. Jambo linalofanyika sasa hivi kwa sababu madaraja ya ile barabara kutoka Kitahi kwenda Ngaka, kata ya Ruanda ni membamba wametengeneza bandari kavu karibu na Kitahi. Kwa hiyo, utakuta pana msururu mkubwa sana wa malori yanayotakiwa sasa kwenda kuchukua mzigo unaotoka machimboni na kuletwa kwenye bandari kavu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuiombe Serikali iangalie, mwaka jana nilikuwa na swali juu ya barabara hii, nililambiwa kuwa upembuzi yakinifu ulikwisha fanyika. Bado kwenye kitabu cha mawasilisho ya Mheshimiwa Waziri barabara hii sioni kama inapewa kipaumbele cha kujengwa kwa lami. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba barabara hii ni ya kitega uchumi na bahati nzuri lazima niwe muwazi kwamba Mkuu wa Mkoa jana alinipigia simu baada ya kupata taarifa kwamba barabara hii haijatengewa fedha kuweza kujengwa kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa ziarani Mkoani Ruvuma, mwezi Januari 2017; tukiwa kwenye makaa ya mawe ilionekana kwamba katika mkataba wa mwekezaji *TANCOAL component* mojawapo ya mkataba wake ni kujenga barabara hii kwa kipande cha kutoka Kitahi mpaka pale machimboni Ngaka. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ifanye mapitio ya mkataba huu kama ilikuwa ni makubaliano ya yule mwekezaji atujengee barabara kwa kiwango cha lami, basi kazi hii aweze kufuatiliwa na atimize wajibu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na barabara hizi ambazo nimezitaja pia tulikuwa na ombi, ile barabara ambayo ilikuwa inatoka Kitai kuititia Ruanda kwenye makaa ya mawe Lituhi kipaumbele sasa kisogezwe mpaka Ndumbi ambako tunajenga bandari mpya kando ya Ziwa Nyasa kwa Mheshimiwa Stella Manyanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo pia barabara ya kimkakati pia kiulinzi pia ambayo inatoka Lituhi mpaka Mbamba bay. Barabara hii ni muhimu sana siyo tu kwa uchumi ni kwa watu wa Nyasa na Mbinga pia ile barabara ndiyo ulinzi wa Ziwa Nyasa ukizingatia tunapakana na Malawi ambao hatuwaamini sana sasa hivi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo barabara zingine muhimu ambazo tungeomba pia Wizara ingalie namna gani ya kuzipeleka kwenye ujenzi wa kiwango cha lami. Tunayo hospitali moja ambayo tunaitumia kama hospitali ya Rufaa

ya Litembo, ili kufika kwenye ile hospitali tunazo barabara mbili, hii inayotoka Mbinga inapita Myangayanga kwenda Litembo tunayo inayotoka Nyoni - Mbaji kwenda Litembo. Barabara hii bahati mbaya sana kipindi cha masika haipitiki. Wiki iliyopita tu Diwani alinipigia simu kwa sababu ya barabara hii ile hospitali imeshindwa kubeba *supplies* kutoka Mbinga Mjini kupeleka kule Litembo ili watu waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikiri nilimpigia simu Meneja wa *TANROADS* na alikuwa ameshamtuma mhandisi kwenda kukagua maeneo ambayo ni korofii ili watu waendelee kupata huduma, niombe Wizara walau barabara mojawapo kati ya hizi mbili ifikiriwe kwenye kiwango cha lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo barabara nyingine iliongelewa pia hapo awali ipo chini ya *Mtware corridor*, barabara ya kipande cha Mbinga kwenda Mbamba bay. Barabara hii kwa majibu ya mwaka jana upembuzi yakinifu umekwishafanyika lakini pia uzinduzi wa barabara hii ulifanyika Katavi mwezi wa tatu mwaka jana kwa barabara inatoka Sikonge - Mpanda na hii ya Mbinga Mbamba bay. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mawasilisho ya kitabu cha Wizara ukurasa 28, *item* namba 50 inaongelea hii ya Katavi, ukienda kwenye ukurasa 244 inapoongelea sasa barabara ya Mbinga - Mbamba bay msimamo wa wizara unatofautiana. Kwenye kipande cha Mbinga - Mbamba bay kitabu kinaeleza kwamba upembuzi yakinifu zimeshafanyika zinatafutwa fedha kwa ajili ya ujenzi. Kwa kipande kile cha kutoka Sikonge - Mpanda unasema kwamba fedha zilikwishapatikana kuitia *African Development Bank*. Ninachofahamu miradi hii inatekelezwa kwa pamoja kwa nini huku kuwe na *status* tofauti na huku *status* tofauti? Mara ya mwisho wakati nafuatilia kwa Meneja wa *TANROADS* Songea walichoniambia mwezi wa kwanza mwaka huu walikuwa wanarekebisha *design* ya barabara ya Mbinga - Mbamba bay na hapakuwa na suala la fedha.

28 APRILI, 2017

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wakati tutakapokuja kufanya *Windup* utuambie *statusya* upatikanaji wa fedha hizi, kwa sababu wananchi walishapisha maeneo ili ujenzi wa barabara hii uweze kufanyika mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo barabara zingine ambazo ni za ngazi ya Mkoa ambazo *TANROADS* hawakuwahi kupita tangu zipandishwe hadhi

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wako umekwisha.

MHE. MARTIN M. MSUHA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Saul Henry Amon atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi ajiandae.

MHE. SAUL H. AMON: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hii Wizara ya Miundombinu, vilevile namshukuru Mungu kwa kunipa huu muda wa kuchangia Wizara hii ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niazé kushukuru na kumpongeza Rais kwa uamuzi wa kuanzisha hii *standard gauge*. Nimpongeze Rais vilevile kwa ununuzi wa ndege bila kujali watu watasema nini, kuna watu wanakebehi kwamba ndege hazina maana, lakini tunavyojuwa kwa llani ya Chama cha Mapinduzi zile ndege zilizonunuliwa ni manufaa ya Taifa zima pamoja na utalii wa ndani kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Waziri wa Miundombinu ambaye nimemwona kwenye *tv* akizunguka kila kona ya Tanzania kuangalia ujenzi wa miundombinu ya nchi hii, nakupongeza sana. Vilevile nimpongeze Naibu wake

na Katibu wake ambao wote huwa nawaona kwenye vyombo vya habari wakizunguka na kuzungukia kuangalia miundombinu ya nchi hii.

MBUNGE FULANI: Anasoma.

MBUNGE FULANI: Endelea achana nao, usiwasikilize hao endelea.

MHE. SAUL H. AMON: Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nipongeze pia ujenzi wa *flyover* zilipo Dar es Salaam kwani zitapunguza msongamano mkubwa uliopo Dar es Salaam ambao umesababisha shughuli nydingi za kimaendeleo zisiende. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa *standard gauge* ambao utaharakisha maendeleo ya nchi yetu kwa kubeba mizigo, abira na sasa Mwanza tutakuwa tunaenda kwa saa nane badala ya siku mbili. Kigoma tutakuwa tutakwenda kwa saa nane mpaka tisa badala ya siku mbili. Hivyo nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake na watendaji wake wakuu wakiwemo Mawaziri pamoja na Manaibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, nia yangu ambayo nimeijia hapa hasa kwa Mkoa wangu wa Mbeya. Mkoa wa Mbeya kama mnavyoujua na wote Mawaziri mmeshafika pale, barabara ya kuingia katikati ya mji ni tatizo kubwa sana. Kama alivyozungumza mchangiaji aliyeppita amesema kwamba mahali pa dakika kumi tunatumia saa mbili, ni kweli mtu ukifika Uyole kama ndege itaondoka baada ya saa mbili na nusu itakuacha, mahali ambapo tunaweza kutumia nusu saa tu kutoka Uyole mpaka Songwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya *bypass* ya Mbeya ambayo ni Uyole *bypass* kwenda mpaka Songwe tunaomba wananchi wa Mbeya ifanyiwe upembuzi yakinifu haraka ili iweze kujengwa kwani Mbeya ni lango kuu kabisa ambalo linatumia nchi zaidi ya nane kwa kutumia barabara

28 APRIL, 2017

hiyo. Barabara hiyo ni kwa ajili ya kwenda Zambia, Malawi, Congo, Zimbabwe wote wanapita njia hiyo lakini usumbufu ni mkubwa sana, naomba mtusaidie. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nina ombi kwa Waziri kuhusu uwanja wa ndege tumewahi kurudi zaidi ya mara mbili, kwa sababu tu uwanja hauna taa za kuongozea ndege pale chini. Gharama yake sijajua ni kiasi gani kikubwa, mwaka huu naona ni mwaka wa pili tukizungumzia suala hilo wakati huo huo Serikali ilishaahidi kwamba itatoa hela ingawa nimeona bajeti ya mwaka jana sijaona hata senti tano ilioenda Songwe, kama ipo nitaomba kuiona. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi kwenye Jimbo langu la Rungwe. Jimbo la Rungwe ni moja kati ya majimbo ambayo yanatoa chakula, viazi vingi mnavyoviona vinatoka Rungwe pamoja na ndizi zote zinatoka Rungwe, lakini Katika Wilaya ya Rungwe kuna kata tatu hazina barabara kabisa, hivi ninavyozungumza saa hizi zimekatika ukienda kata ya Swaya, kata ya Kinyala hakupitiki. Matokeo yake wakulima wa kule wanapata taabu kweli, tungeomba hizo barabara badala ya kuendelea kushughulikiwa na Halmashauri barabara ya kutoka Igogwe - Lubala - Vibaoni - Malangali mpaka Mbeya Vijiji tungeomba iwe barabara ya mkoa kwani pale pana mazao mengi, nazungumza sasa hivi hata tukiongozana na Waziri ataenda kukuta mazao yanavyoharibika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuyatoa mazao katika eneo hilo inabidi urudi umbali mrefu kilometra 40 halafu ndiyo uanze kupandisha nayo kwenda Mbeya kiasi kwamba wakulima wa eneo hilo pamoja na kwamba wanalima sana viazi, mahindi, maharage yananunuliwa kwa bei rahisi kiasi kwamba hawapati faida na gharama ya kilimo kile inakuwa ni kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba hiyo barabara uiangalie. Narudia hiyo barabara kama hujaandika, barabara ya Igogwe kwenda Lubala - Vibaoni - Malangali ambayo inakwenda Swaya kwenda kutoka Mbeya Vijiji.

Hiyo ni barabara muhimu sana na kuna vyakula vingi sana, wakati kuna sehemu zingine watu wanakufa kwa njaa wanaumia kwa njaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna barabara ambayo imepandishwa daraja, ninawashukuru sana Waziri pamoja, Naibu Waziri na Watendaji wako kwa kuipandisha daraja kuwa ya Mkoa. Barabara ya kutoka Pakati - Njugilo - Masukuru kwenda mpaka mpakani. Ile barabara wenzetu upande wa Kyela wamefika mpaka kwenye mpaka. Ni sehemu ndogo ili uweze kwenda Kyela kutoka eneo la Matwebe inabidi uzunguke utumie saa mbili badala ya kutumia dakika 20, vyakula, matunda, mpunga hapo vinaaribika kwa sababu hakuna mtu ambaye anaweza akazunguka kwa kiasi kikubwa wakati huu wa mvua. Ikifika kipindi cha mvua pale mahali panakuwa ni kisiwa, huwezi tena kuenda, hizo Kata mbili zinakuwa zimebaki na kila tunapokwenda kwa ajili ya kampeni tatizo ni hilo hilo.

Naomba Waziri kwa vile umeipandisha hadhi hiyo barabara naomba uifanyie angalau ukarabati kwa sababu kule hata *material* ile *moram* ni nyingi sana maeneo yale ambayo ni kazi ndogo, kwa sababu daraja ni moja na sehemu korofii hazizidi tatu ambazo ukisizimamia zinaweza zikawa zinakapitika moja kwa moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine haya ninaishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuendeleza kujenga barabara ya Tukuyu kwenda mpaka Lwangwa kujenga barabara ya njia panda mpaka Matema hiyo nashukuku na tunaomba kila mwaka tuendelee kuzitafutia hela zile barabara, kwani zitafunguka, utalii ni mkubwa ukizungumza Matema ni utalii mkubwa sana na pale mnajenga bandari kwa ajili ya meli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka niishukuru na kuipongeza Wizara hii ni kwa kutengeneza na kutimiza ahadi. Ahadi ya kutengeneza meli katika Ziwa Nyasa. Zile meli tumeziona zimeshaingia majini na meli ya tatu ya abiria inakaribia kuisha.

28 APRIL, 2017

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwashukuru sana na kuwapongeza sana (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda umeisha.

MHE. SAUL H. AMON: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia mia moja na moja kabisa wameniongezea kidogo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, naamini Waziri alikuwa anaandika kama ambavyo umependekezea.

Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, atafuatiwa na Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Mheshimiwa Riziki Lulida ajiandae.

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina ugomvi na Waziri lakini najua dhamira yake pia katika maslahi ya Taifa. Nataka niishauri Wizara pamoja na nchi kwa ujumla, nikumbushe kwamba mwaka 1997 Waziri Amani Karume wakati huo akiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na Waziri William Kusila kwa upande wa Tanzania Bara waliunda kamati ambayo ilikuwa ikiongozwa na Profesa Mahalu. Kamati ile pamoja na mambo mengine ilikuwa ikichunguza mambo ya *Maritime Law*. Kamati ile ilitoka na mapendekezo kwamba kuwe na chombo cha pamoja ambacho kitaweza kusimamia mambo ya *marine* kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, kwa sababu kujumla mambo ya *marine* siyo mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lile lilidharauliwa na wala halikufanyiwa kazi, kwa hiyo, mwaka 2001 *SUMATRA* wakatunga Sheria ya *SUMATRA* na wenzao Zanzibar wakawa wamenyamaza kimya. Lakini mwaka 2003 wakatunga ile sheria ya *The Merchant Shipping Act*. Sheria ya *SUMATRA* ikatoa mamlaka kwa Mamlaka ya *SUMATRA* kuweza kusajili meli. Mwaka 2006 Zanzibar walivyoona kwamba aah, hawa

28 APRIL, 2017

wenzetu tayari wameshatunga sheria na mambo yanaendelea na wao wakatunga Sheria ya *Maritime Transport Act* ambayo ilifuatiwa na sheria baadae mwaka 2009 ya *Zanzibar Maritime Authority* (ZMA).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ushauri ule ulidharauliwa kilichotokea *SUMATRA* wakawa wanasaliji meli inapeperusha bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Zanzibar wakawa wanasajili meli zinapeperusha bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini katikati hapa hakuna chombo chochote ambacho kinawaongoza, kila mmoja anafanya vyake. Kama kuna chombo kilikuwa kinawaongoza nafikiri Mheshimiwa Waziri atuambie.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar wakasajili meli za Iran ambazo ziliwekewa vikwazo na Umoja wa Mataifa, meli zile zikaleta mzozo mkubwa. Kwa hiyo, baada ya kusajiliwa kwa meli zile wakafanya ujanja ujanja wenyewe kwa wenyewe wakalimaliza lile suala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, baadaye Zanzibar wakasajili tena meli ambazo zilikamatwa na *cocaine* katika Bahari ya maji ya Uingereza ikiwa na tani tatu za *cocaine*. Kile chombo hakipo, baada ya kudharau ule ushauri haikupita muda sana, ikakamatwa meli ya *Gold Star* kule Italy ikiwa na tani 30 za bangi. Kwa hiyo, kile kitendo cha kukataa ule ushauri kwa sababu hili jambo siyo la kimungano ukitoka katika *foreign affairs* linaingia jambo la Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania imekuwa ikiendelea kupata aibu na wanaofanya hivyo mimi nawajua na wanafanya kwa lengo gani. Viongozi waandamizi wa Zanzibar wanashiriki kikamilifu katika kuhamkisha kwamba wanajipatia fedha kwa njia ambazo hata Taifa kuligharimu haina tatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa nazungumza na viongozi wa Zanzibar kuhusu hili jambo, wakaniambia kwamba baada ya matukio hayo kwanza wakaweka mfumo

28 APRILI, 2017

wa kielektroniki ambao sasa *IMO* wanakuwa wanaziona meli zikisajiliwa. Ule mfumo *password* waliyonayo *SUMATRA*, Zanzibar wakaitaka *password* *SUMATRA* hakuwapa. Nakubaliana nao wasiwe kabisa, kimsingi hapo sina tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar wanasema ukipitia sheria yao ile ya *Maritime Transport Act*, kifungu namba 8 wanadai kwamba 8(1) ukija (e) ukisoma huku kinasema kama ni Zanzibar wenyewe mamlaka ndiyo waliosajiliwa na *International Maritime Organisation (IMO)*, *SUMATRA* wao hawajasajiliwa na *IMO*, kwa hiyo haki ya kupata *password* ni ya kwao. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshauri tu Mheshimiwa Waziri kwamba kwanza *password* wasipewe, pili; lazima tutengeneze chombo katikati hapa ambacho kitatusaidia kufanya mambo haya yasitokee tena. Kwa sababu kuna watu pale kazi yao wanatumia hii sehemu ya kusajilia meli kwa kujipatia kipato binafsi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikushauri kwamba ukae na timu yako mambo haya ni hatari kwa Taifa ili uweze kulitatua tatizo hili kiuangalifu kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni bandari kuhusu suala la *flow meter*. Tatizo la *flow meter* lilikuwa ni kubwa sana katika nchi hii, mafuta yakiibwiwa kulikuwa kuna vituo vya mafuta havina idadi. Bandari sasa na watu wengine wameanza wanataka pale *flow meter* iliyopo pale Kigamboni iondolewe ipelekwe *TIPER*, maana yake mahali ambako palikuwa pakiibwiwa mafuta ndipo sasa wanataka *flow meter* iondolewe wapate kuiba mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ujajiuliza *flow meter* hii tumeifunga kwa dola za kimarekani milioni 16 mwaka mmoja uliopita, bandari wamepeleka watu sita *training*, wawili kutoka *TRA*, wawili kutoka Vipimo na wawili kutoka Bandari, wamepelekwa *training* kwa ajili ya *operation* ya *flow meter*, lakini watu hao hawapo wamehamishwa kwenye *flow meter*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *flow meter* ile wanashusha mafuta machafu, *flow meter* inapiga *alarm* wanakwenda kuzima *alarm*, wanashusha mafuta machafu. Hawana dhamira njema, ukiwaliza wanakwambia pale *flow meter* ilipo itaharibika mara moja kwa sababu mafuta yanakuwa hayajatulia machafu, nani kawambia walete mafuta machafu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema kwa sababu ya Kenya zile bomba ziko mbali na matenki yako mbali ndiyo *flow meter* ina uwezo wa kudumu siyo kweli. Kenya kwanza mabomba yote ni ya Serikali kutoka Mombasa mpaka Nairobi. Mabomba yanayopitisha mafuta ya Kenya tena yapo juu yanaonekana, ya Tanzania yako chini yamejificha yako chini kabisa, sasa watu wana uwezo mkubwa wa *ku-bypass* mafuta yale wakayachukua. Mheshimiwa Waziri hili usilikubali hawa wanataka kuiba mafuta kwa shinikizo la makampuni ya mafuta ili waweze kuiba mafuta. Kwa hiyo, suala hili Mheshimiwa Waziri lazima uwe mwangalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kwa nini watu mmewasomesha, Uingereza, *South Africa*, mmewasomesha Marekani kuhusu *flow meter* halafu mnakwenda kuchukua watu wengine mbali mnakuja kuwaweka sasa ambao hawajaenda *training* mahali popote. Wamepelekwa *training* miezi mitatu, kwa hiyo, lengo hasa ni kuiba mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri hili ukilikubali basi utaingia kama yule Waziri mmoja aliyeandika kwa maandishi kwamba suala la *flow meter* zisimamishwe ili wapime kwa kijiti wapime kwa kijiti, wanapima kwa kijiti halafu nchi hii bwana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri, dhamira yako najua vizuri sana. Ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Saidi Lulida na Mheshimiwa Zitto Kabwe ajiandae.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Naibu Spika, Nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo ili nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu sana katika maendeleo ya watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na eneo hili la kisera. Suala la kuunga mikoa limesemwa jana katika hotuba zote tatu, wachangiaji tangu jana na leo na hata ripoti zote hizo zimebainisha kwamba kuna mikoa yetu mingi bado hajiaungwa. Ukienda Kaskazini, ukienda Magharibi, ukaenda na Kusini hali ni hiyo hiyo. Kwa hiyo, naishauri Serikali kama tulikubaliana tuanze na kuunga mikoa hebu tuunge hiyo mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina uhakika kama miradi yote iliyopo kwenye vitabu hivi ni ya mikoa, kuna miradi ya Wilaya, tusichanganye kama tulikubaliana tuunge mikoa tumalize kuunga mikoa kwanza halafu tushuke kwenye hizo ngazi zingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haiingii akili ya kawaida mtu uko Mahenge, uko Ifakara unataka kwenda Lindi na Mtwara urudi Morogoro, uende Dar es Salaam ndiyo ushuke kwenda kule chini, haiingii akilini kwa kawaida. Mnavyofahamu barabara ya kwenda Dar es Salaam jinsi ambavyo ina changamoto zake nyingi. Hivyo, naishauri Serikali hebu tufanye jambo hilo kwanza. Watanzania wengi tena wale wa hali ya chini usafiri wao siyo ndege, usafiri wao siyo meli, usafiri wao ni treni na barabara. Treni haipiti maeneo yote, twendeni tukajenge hizo barabara zinazounga mikoa yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Chenge asubuhi ya leo, ameongea vizuri sana kuhusu barabara inayounga Mkoa wa Simiyu na Mkoa wa Arusha. Ukiwa Arusha ukitaka kwenda Musoma ni budi upitie Singida - Mwanza - Musoma. Hakuna barabara inayounga Arusha na Musoma, hakuna barabara inayounga Arusha na Simiyu, hakuna barabara inayounga Manyara na Simiyu, hakuna barabara inayounga Manyara na upande huu wa Tanga.

Tunafanya nini? Kwa hiyo, nadhani tufanya jambo hilo la kisera ambalo tumekubaliana. Barabara ya *Oldeani Junction*, Mang'ola, Matala hadi Mkoa wa Simiyu na baadae Mkoa wa Shinyanga ni barabara ya siku nydingi sana. Mzee wangu asubuhi ameiongelea vizuri. Mheshimiwa Chenge ule muziki uliousema wa kuuchenza, wewe ukianza kuchenza huko Simiyu na sisi tutaanza kuchenza huku Arusha, halafu Mheshimiwa Mbarawa utatuona. Tufanye mambo ambayo tumekubaliana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mbarawa barabara ya *Oldeani Junction*, Matala hadi Simiyu siyo barabara ya Karatu - Mbulu - Haydom kwenda Simiyu, hizi ni barabara mbili tofauti. Barabara hii kwenye vitabu vyenu mmeiita *The Southern Serengeti bypass. Southern Serengeti bypass* hata siku moja haiwezi kupita Mbulu ni hii ambayo Mzee Chenge asubuhi ameiongelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri juzi nikiwa Jimboni nimekutana na vijana wa ofisiini kwenu, hii taarifa sijui wameitoa wapi, sasa wakati mnahitimisha mtuambie hili badiliko la kwamba barabara sasa ni kama inataka kutelekezwa, barabara ambayo imetumia mabilioni ya pesa kwenye upembusi yakinifu, sasa wanaanza upembusi yakinifu mwingingine utakaotumia mabilioni ya hela mnapitisha Mbulu - Haydom, Huku ni kuchenza hela. (*Makofii*)

Mmetumia over bilioni tano kwa ajili ya upembusi yakinifu na hata sasa hivi pamoja na kwamba kazi ile ya upembusi yakinifu ilikamilika, bado mmeipa hela iendelee kutumika vibaya. Kwa hiyo, barabara ya kuunga Arusha na Simiyu ni *Oldeani Junction* - Matala - Mwanhuzi - Lalago na kwenda huko kwingine siyo hii ya Mbulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Karatu - Mbulu - Haydom na kwenda Mto Sibiti, Mheshimiwa Waziri Mbarawa ni barabara iliochelewa nayo pia kujengwa kwa kiwango cha lami. Wale Wabunge wa siku nydingi mlioko kwenye jengo hili mmesikia, tangu enzi ya Marehemu Mzee Patrick Qorro, akaja Mzee Philip Marmo akaja Mheshimiwa

Dkt. Wilbrod Slaa na hawa wengine wa majuzi wameendelea kuongea barabara hiyo lakini hadi leo barabara hiyo ni ya vumbi. Viongozi wote tena wengine wameanzia awamu ya akina Kikwete, barabara ya Karatu - Mbulu - Haydom Marehemu Mzee Rashid Kawawa alipokwenda Maghang miaka hiyo ya 1980 alisema barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami, hadi leo ni barabara ambayo kupitika kwake wakati wa mvua ni shida kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nakushauri Mheshimiwa Mbarawa, haya mambo nadhani mengine mnayapata mkiwa ofisini, hebu mje *field*, sijakuona ukija Kanda ile na Naibu wako pia sijamuona, hebu mtembee ili muonejiografia ili muweze kujua hiki ambacho tunakiongea. Naomba barabara hizo mbili mztambue ni barabara mbili tofauti na zote zina umuhimu wa tofauti. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kuhusu suala la kupandisha hadhi barabara. Mheshimiwa Waziri tunaomba barabara zipande hadhi ili zipunguze mzigo kwenye Halmashauri zetu. Fedha zinazokuja kwenye Halmashauri kwa ajili ya matengenezo ya barabara ni fedha kidogo sana.

Mwaka jana Karatu tulipitishiwa shilingi bilioni 1.5, lakini hadi sasa tunavyoongea tumeletewa shilingi milioni 300, *thirty percent* na tuna mtandao wa barabara unaozidi kilometa 500, hivi utafanya nini kwa shilingi milioni 300? Kwa hiyo, tunaomba zipande juu ili huu mzigo utoke kwetu uende huko kwako ambako kuna fedha nyngi, huko ambako unapata asilimia kubwa ya fedha.

Kwa hiyo, tunaomba hizi barabara zipande hadhi ili mtusaidie ndugu zetu kubeba mzigo huu, siamini sana kama hoja ya kuanzisha Wakala ndiyo itakuwa suluhisho la kumaliza tatizo hili, tuleteeni fedha, Halmashauri zetu zina uwezo na wataalamu wa kutosha wa kufanya kazi ya barabara. Jambo hili leo mkilitoa pale Halmashauri, wale wataalamu tulionao watakuwa *redundant*. Kwa hiyo, nadhani suala hili tuleteeni hela sisi tuwasaidie kufanya hizo kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema kidogo kuhusu Reli ya *TAZARA*, miaka ya 1970 nchi hii ilipata neema ya kupata reli ya kisasa kwa wakati ule. Ilikuwa reli pekee katika Ukanda huu wa Kusini iliyojengwa kwa usasa wa kiasi kile, yaliyoendelea *TAZARA* tunayafahamu, yanayoendelea *TAZARA* tunayafahamu. leo kama Nchi tumejitiwisha kubeba kujenga reli nyininge ya *standard gauge* hii inayopita katikati ya nchi. Naomba hayo yaliyotokea kwenye reli ya *TAZARA* yawe ni somo na darasa kwa ajili ya uendeshaji wetu kwenye reli hii ya katи tunayokwenda kujenga. Tusipoangalia miaka 40 mingine inayokuja tutaimba muziki huu huu ambao leo tunauimba kwenye reli ya *TAZARA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, naamini nchi hii bado inaihitaji reli ya *TAZARA*, tena inaihitaji reli ya *TAZARA* sana. Reli ya *TAZARA* kwa sasa kinachohitajika ni uwekezaji na kupata viongozi wenye weledi basi reli ile inaweza ikajiendesha. Machimbo ya makaa ya mawe yaliyopo pale Songwe yanatosha kabisa kuendesha reli hii. Kwa hiyo, Serikali ikubali kuwekeza fedha kidogo ili reli hii iweze kujijendesha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kidogo tena kuhusu reli ya katи....

NAIBU SPIKA: Muda umeisha Mheshimiwa.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofii*).

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Riziki Said Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Yahaya Omar Masare ajiandae.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii, nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijaalia nami kupata nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mezani, na kukiombea rehema Chama changu cha Wananchi CUF kupitia kwa Katibu Mkuu wangu Maalif Seif aendelee kuwa

na subira na Mwenyezi Mungu amesema, *Innallah Maa'swabiriina* (kila mwenye subira yuko pamoja na Mwenyezi Mungu). (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia hotuba na hoja zilizopo mezani kwangu hazihitajiki kuungwa mkono na Wabunge wa Mkoa wa Lindi na Mtwara. Nina sababu za msingi ukienda ukurasa 188, bajeti ya miradi ya Mkoa wa Lindi, ukichanganya na Mkoa wa Mtwara basi zinazidi Mkoa wa Kilimanjaro. Mkoa wa Lindi na Mtwara ukichanganya tunapata shilingi bilioni 1.7; wakati ukizingatia Mkoa wa Lindi ni Mkoa wa mwisho. Leo Mbunge wa Liwale hawesi kwenda Liwale hana nafasi barabara hakuna. Mbunge wa Liwale anatoka Dar es Salaam mpaka Lindi - Masasi - Nachingwea anakwenda Liwale na hawesi kufika kwa siku moja. Ameanzia Mheshimiwa Kawawa akashindwa, wamekuja Wabunge akina Hassan Chande Kigwallilo wameshindwa, halafu utasema tuna sera ya barabara, siikubali sera hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni sera ambayo inabagua, ni sera ambayo ina upendeleo, ni sera ambayo haitaki maendeleo ya watu wa Kusini. Wameitengeneza sera hii maksudi watendaji kuhakikisha Kusini inadhalilika. Nazungumzia hivi kwa sababu Mkoa mzima wa Lindi una miradi minne tu. Je, jiulizeni ukiangalia Jimbo la Lindi Vijiji la Mchinga na Mtama hawajaweka mradi hata mmoja, tuijulize kuna nini? Kujuliza maana yake unapata maswali mengi ukijiuliza, eti kweli barabara za Mchinga hakuna hata mahali pa kufanya *rehabilitation?* Hakuna ndani ya kitabu hiki. Mtama kwenye Jimbo la mdogo wangu au mwanangu Nape Nnauye hakuna hata mradi mmoja, ninyi ni wabaguzi! Mnaibagua Kusini kwa maksudi kuwfanya wananchi wa Kusini waichukie nchi yao kwa ajili ya miradi yenu mibovu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani watu mikoa mingine wana lami mpaka katika kata, leo Mkoa wa Lindi hauna mawasiliano ya aina yoyote sasa hivi. Nakwambia utasikia wanakwenda mikoa mingine siyo Lindi, viongozi

wakuu juzi wametembelea kwenda Lindi wameshindwa kwenda Liwale, wameshindwa kwenda Nachingwea, kwa nini wameshindwa? Hakuna njia ya kupita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ubaguzi huu ndiyo unaofanya wananchi wa kule kuichukia CCM. Na mimi naungana nao kuichukia CCM kwa vile hawataki kuwatendea haki, barabara iliyopo ni ya kitaifa ambayo ni lazima mujenge, jiulize unatoka Nanganga kwenda Nachingwea haipitiki, unatoka Nachingwea kwenda Liwale haipitiki, unatoka Liwale kwenda Nangurukuru haipitiki, unatoka Lindi - Ngongo mpaka kwenda Ruangwa hakupitiki, halafu mtasemaje sisi tuko katika Tanzania, sisi tuko Tanganyika. Ndiyo maana tunaidai Tanganyika na makao makuu ya Tanganyika yatakuwa Liwale. (*Makofi/Kicheko*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kumetokea mafuriko, Jimbo linaloongoza kwa mafuriko ni Lindi Vijijini. Jiulizeni wapi wameweka bajeti ya Lindi Vijijini. Hawakuweka hata barabara moja ambayo itarekebishwa angalau wananchi wale wapate hifadhi, hakuna. Wanawake wanatembea na miguu hakuna daraja, wanawake wanataka kwenda kujifungua hospitalini hakuna daraja watapita wapi kama siyo ubaguzi mkubwa unafanyika namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wanaosifia wamefaidika na hili, ukimuona mtu anasifia anafaidika na hili lakini mimi nitasifia kwa lipi hapa? Hakuna cha kusifia hapa. Tunadhalilika, nitashangaa kusikia Mbunge wa kutoka Lindi anaisifia bajeti hii, hakuna kitu hapa. Huu ni udhalilishaji wa muda mrefu, mimi niko humu ndani kipindi cha tatu kila mwaka ni barabara, wakienda kutafuta kura wanawadanganya, mwaka huu kutoka Nangurukuru mpaka Liwale mpaka Nachingwea ni lami na tayari tulishatenga fungu. Tupo katika *feasibility study* zaidi ya miaka 40 hamna *feasibility study*. Ifike mahali mdanganye watoto wadogo sisi ni watu wazima sasa hivi, hata wale walioko kule ndiyo maana wamegeuka wameona kabisa maeneo ambayo yamedhalilishwa, hawapewi manufaa yoyote.

28 APRILI, 2017

Mheshimiwa Naibu Spika, leo katika mazingira haya, nani atakwenda kufanya kazi Liwale? Ndiyo maana unaambiwa Mkoa wa Lindi na Mtwara ni Mikoa ya mwisho kwa elimu. Kiwango cha elimu kimekuwa chini walimu hawataki kwenda. Sasa mnataka kutuweka mpaka lini tuwe tunadhalilika tukiwaangalia tunawabembelezeni, bajeti bajeti, sera iko wapi ya barabara?

Naomba kama kweli wale Wabunge wa Kusini wana ukereketwa tukutane Jumatatu, tufanye kikao tuikatae hii bajeti haifai kabisa. Ni bajeti ambayo haimsaidii mwananchi wa Lindi wala mwananchi wa Mtwara. Kama hutafanya vile pengine unataka Uwaziri, huwezi kupata Uwaziri katika kipindi hiki. tunachoomba tuungane, tuikatae bajeti, ili itusaidie. (*Makofii*)

TAARIFA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda.

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kutoa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba msemajii aliyekaa chini, aangalie ukurasa wa 259 katika hotuba ya bajeti ya Waziri wa Ujenzi, Mkoa wa Lindi wamepangiwa shilingi milioni 875 katika ukarabati wa barabara zao anazozizungumzia hazipitiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa Mheshimiwa Mbunge.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lulida unaipokea hiyo taarifa?

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Hajitambui na mtu asiyejitambua hakuna haja ya kubishana naye. Unajua wakati mtu yuko *serious* yeeye anataka kuleta mzaha, Bunge siyo sehemu ya kufanya mzaha, tupo hapa *serious* tunatetea mikoa yetu ambayo iko nyuma kielimu, kiafya, kupata maji,

maendeleo ya barabara, tunatetea sasa yeye anatafuta nafasi ya kupata sifa hapa siyo mahali pa kupata sifa, sikubali hoja yake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la wizi katika mitandao na hasa katika kampuni ya Airtel. Wananchi wanaibiwa vibaya sana pesa hasa kipindi cha sikukuu na kipindi cha *weekend*. Wizi huu unafanywa na wafanyakazi na ninao ushahidi nitakuletea. Bahati mbaya walinfanyia hata mimi mwenyewe, lakini nikawaambiwa ninyi mmechezea choo cha kike na leo mtakiona. Walifanya wizi baada ya kuletewa pesa za Mbunge mwenzangu alifiwa wakanitumia pesa katika simu yangu. Wale kule wanaona kama imeingia na ilikuwa ni kipindi cha sikukuu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikapigiwa simu; mama kuna pesa ilikuwa zimekatwa kimakosa tuanaomba tukuingize, wakanipeleka nikashtukia sielewi maana yake ilikuwa siku mtandao haufanyi kazi, nika- *qoute agent code* namba nikai-*qoute*, ghafla nikashtukia milioni moja laki tano wameziiba.

MBUNGE FULANI: Duh!

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Walipoziiba hela zile nikakimbia nikaenda Dar es Salaam nika *block*, kinachosikitisha watu wa *cyber crime* wakishirikiano na taasisi hizi hazina mawasiliano. Sasa jiulize kama watu ambao wanaweza kujitambua wakajua wafanye nini ili waweze kurudisha hela zao, je, watu wa vijijini wanafanya nini, ni kuibiwa tu. Wizi umekuwa mkubwa sana tunataka tupate majibu hawa watu wa *cyber crime* wanafanya nini, mbona wizi umekuwa mkubwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano ukienda India unaambiwa utakaa kwa siku ngapi ukipewa ile *card chip* ya kukaa pale, unasema nakaa wiki mbili, siku unaondoka ikifika saa sita usiku jina lako limeshapotea na mawasiliano yamepotea. Tanzania acha simu yako nenda kakae Marekani miaka miwili ukirudi unakuta matandao uko *online* tu, mpaka

28 APRILI, 2017

leo hawajahakiki kama kweli jina lile linalotoka katika namba ndiyo kweli, wenzetu Uganda wameshaanza sasa hivi kuhakikisha yule aliyepewa namba kweli ni mwenyewe, ndiyo maana wizi wa mtandao hautaweza kuisha kutokana na uhakiki wa majina haukufanyika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Wizara yenye dhamana ifanye kazi ya kuhakiki vizuri.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa, kengele ya pili tayari.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Bado dakika zangu alichukua yule.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Serikali naipongeza Serikali kwa kupitia mtandao wa mwendokasi wameshinda tuzo kwa kwa kuweweza kufanya uwekezaji mzuri katika Afrika Tanzania ni nchi ya pili. (*Makof/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa kwa hizo pongezi nadhani zimefika mahali pake. Mheshimiwa Zitto Kabwe atafuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare kama tutakuwa na muda bado, Mheshimiwa Kiswaga Destery.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara hii muhimu sana, ambazo ni Wizara tatu kwa pamoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda niwashukuru sana Mamlaka ya Bandari kwa kazi ambayo wanaifanya Kigoma, nimeona zabuni ya bandari ya Kibirizi, ninaamini kabisa bandari ya Ujiji zabuni yake itakuwa ama imetoka leo au Jumatatu na pili bandari ya Kagunga imekamilika, kwa hiyo, napenda niwashukuru sana, nataraji kwamba hatua zitakazofata bandari ya Mwamgongo na bandari ya Mtanga zitaweza kufanyiwa kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nimeona ukurasa wa 102 wa hotuba ya Waziri kuhusiana na uwanja wa ndege wa Kigoma, nashukuru sana kwamba sasa zabuni itatangazwa tena na kuhakikisha kwamba tunapata mkandarasi kwa ajili ya kujenga jengo la abiria na njia zinazoenda pale. Hii ni ishara kwamba naungana mkono na juhudzi za Mkoa wa Kigoma na Wabunge na wananchi wa Mkoa wa Kigoma kutaka kuubadilisha Mkoa wetu ule uweze kuwa na maendeleo ya kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo nataka kuzungumzia ni reli, wenzangu wamezunguka hapa kuhusu reli na ukitazama hotuba ya Waziri wameendelea toka mwaka jana tumelalamika kuhusu jambo hili, kwamba wametoa tafsiri mpya ya reli ya kat. Reli ya kat tafsiri yake ni Kigoma - Dar es Salaam au Dar es Salaam - Kigoma, maeneo mengine yote ni matawi ya reli ya kat. Ukitoka Ruvu kwenda Tanga ni tawi, kutoka Tabora kwenda Mwanza ni tawi, kutoka Manyoni kwenda Singida ni tawi, ukitoka Kaliua kwenda Mpanda ni tawi, mengine yote hayo ni matawi. Reli ya kat ni Dar es Salaam – Kigoma na Kigoma - Dar es Salaam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa *standard gauge* kwa hatua hizi wanazoziita hatua za awali unatoka Dar es Salaam kwenda Mwanza. Nilikuwa namuomba Waziri atafute andiko ambalo Mbunge wa zamani Mheshimiwa Ali Karavina aliandika, alikuwa *Transport Economist* Shirika la Reli wakati ule *TRC*, angalia takwimu ni wapi ambapo utapeleka reli upate fedha za kujenga maeneo mengine. Kwa sasabu lango la mashariki la nchi yetu ni Dar es Salaam, lango la magharibi la nchi yetu ni Kigoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonyesha kwamba mizigo ambayo Tanzania inahudumia kwa nchi za Maziwa Makuu, nchi ambazo zinaizunguka Tanzania ni tani milioni tano kwa mwaka, kwa taarifa ya hali ya uchumi ya mwaka 2015/2016. Katika hizo asilimia 34 ni Zambia, asilimia 34 Congo, asilimia 12 Rwanda, asilimia sita Burundi, asilimia 2.6 Uganda. Unapoanza na *standard gauge* matrillioni ya

fedha, ukaipeleka Isaka na Mwanza maana yake ni kwamba unaenda kuhudumia mizigo asilimia 15 ya mizigo yote ambayo tunaipitisha unaacha kwenda kuhudumia mizigo asilimia 40, kwa maana ya Congo na Burundi ambayo yote inapita Kigoma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *economics* gani ambazo mmezitumia katika kuhakikisha kwamba reli inaelekea mahala ambapo hakuna mizigo, *economics* gani ambazo mmezitumia? Sipendi kusema kwamba Kigoma inatengwa siyo lugha ambayo mimi kama kiongozi napenda kuzungumza. Suala hili takwimu zote za kiuchumi zinaonesha reli inapaswa kwenda kule ambapo kuna faida. Hampeleki kule ambapo kuna faida hii maana yake nini? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu Waziri, kuna fedha za Benki ya Dunia ukurasa wa 187 wa hotuba yako kwa ajili ya ukarabati wa reli, hata hizi bilioni 200 za ukarabati wa reli ambao upo sasa, hivi na zenyewe mmepeleka kule ambako mnapeleka *standard gauge*, mnashindwa hata kutudanganya kwa pipi? Hata kutudanganya Diamond aliiomba nidanganye nidanganye nidanganye tu, mnashindwa! Angalau mngetupa hizi bilioni 200 mkakarabati reli ikafanya kazi mkapata fedha za kujenga huko ambako mnataka kupeleka *standard gauge*. Hili jambo naomba mlitazame vizuri, mliangalie kwa sababu haliendani kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukiangalia Waziri bandari zako, angalia takwimu za mwaka jana, bandari zipi ambazo zinakua, bandari ya Kigoma *growth rate* yake mwaka jana *twelve percent*, bandari zingine zote ni *negative growth*. Bandari ya Mwanza mwaka jana *negative 41 percent* mnapeleka reli huko, mnaacha kupeleka reli mahali ambapo mtapata fedha ili mpeleke reli sehemu nyngine. Hebu mtueleze hizi ni siasa, huu ni ukanda au ni uchumi katika maamuzi ambayo mmeyafanya kwa sababu hamueleweki.

Ninaomba jambo hili muweze kulitazama vizuri kwa sababu jambo hili linaleta hisia ya kwamba hamuendeshi nchi kwa mujibu wa Katiba. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba Ibara ya 9(d) Serikali ihakikishe kwamba maendeleo ya uchumi ya Taifa yanakuzwa na kupangwa kwa ulinganifu na kwa pamoja. Hizi *sentiments* mnazisikia za watu wa Kusini, *sentiments* mnazisikia za watu wa Magharibi hazijengi umoja wa Taifa, hili jambo naomba miltazame vizuri ili liweze kufanyiwa kazi inavyotakiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pili katika reli ambalo nataka kulizungumzia leo nataka kuongea na reli tu. Pili, *what are offsets agreements* katika uchumi huu wa reli? Tunatenga fedha nydingi sana kwa ajili ya ujenzi wa reli. Tunawezaje *ku-link* ujenzi huu, kipindi hiki cha ujenzi na ukuaji wa sekta ya viwanda. *Forwards na backwards linkages* kwenye mikataba mmezitazama namna gani? Waziri nakuomba *google* tu kwenye Ipad yako hapo kitabu cha *Transport and Developing Countries* kimeandikwa na Dr. David Hilling. Kineneza namna ambavyo *in 18th century* ujenzi tu wa reli ulivyoeweza *ku-transform* uchumi wa Italy.

Nheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kabisa juhudzi zetu za ujenzi wa viwanda tukazi-*link* na ujenzi wa reli, tusifanye makosa tuliyoyafanya kwenye bomba la gesi la Mtwara, ambapo kila kitu kilichofunga lile bomba kilitoka China. Leo bomba linatumika *only six percent* hamna maendeleo yoyote ambayo tumekuja kuyapata kama nchi mpaka sasa. Kwa hiyo, naomba hili jambo mliangalie *forward and backward linkages*, iangalieni hiyo mikataba upya. *Offsets agreements* ni muhimu sana kwenye mikataba mikubwa namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho katika hili la reli ni suala la kwa nini wenzetu Ethiopia walikosa fedha kama sisi tunahangaika kutafuta fedha, wakatoa *bond* ya wananchi, *sovereign bond* ya wananchi, *especially diaspora* wakanunua kujenga *The Millennium Dam* ambayo inatengeneza *ten thousand megawatts* za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hussein Bashe ameongea asubuhi hapa, ili tufaidike vizuri badala ya reli kuishia Morogoro, kipande hiki na kipindi hiki cha miezi hii reli

ingefika Makurupora na mkaweka *dry port* pale Makutupora, kwa sababu mnakuwa na *long haulage*, unakuwa na *economies of scale* kwenye reli, lakini tunajua hatuna fedha, shirkisheni wananchi tupate fedha ya kufanya kipande hiki kwa kutoa *bond, fifteen years.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leteni sheria hapa kwenye Bunge, tutunge sheria ambayo kila mwaka tuta-allocate a certain amount of budget kwa ajili ya kulipia hizo percent ambazo tutaliwapa hao watu, ambao ni *bond holders*, after fifteen years tutakuwa tumefanya hiyo kazi, tumejenga reli na hamtakuwa mnahangaika. (*Makofi*)

Mheshimia Naibu Spika, ninyi mnajifungia ndani wenyewe, hamtaki kusikia mawazo ya watu wengine, watu wengine wakizungumza mnaona kama wanapingga, hakuna mtu ambaye anaweza kupinga maendeleo ya nchi kwa sababu ni maendeleo yetu wote. Kwa hiyo, nilikuwa nawaomba mtazame jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, angalieni uwezekano wa kuwa na *railways bond* angalau kipande ambacho mnataka kiishie Morogoro, kiishie Makutupora ili tuweze kupata fedha za kujenga maeneo mengine, vinginevyo hatutaweza kwenda huko tunakotaka kwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yangu mengine nimeyaandika kwa maandishi, nadhani nimeshaleta, mtawea kuangalia namna gani mtakavyoweza kujibu. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Destery Kiswaga.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia.

Kwanza nianze na barabara yangu ya kutoka Magu - Kabila - Mahaha. Barabara hii ina kilometra 58, lakini mwaka huu haijatengewa fedha, matengenezo maalum au

matengenezo ya mara kwa mara haina fedha. Nashukuru kwamba imetengewa fedha kwa ajili ya daraja ambalo Serikali inagharamika kila mwaka kwa ajili ya matengenezo ya daraja hili. Ninajua kwamba tayari upembuzi yakinifu umeshakamilika na mkandarasi ameshapatikana, tatizo ni fedha za kuendelea. Niiombe Serikali nikiamini kwamba bajeti ambayo tunayo tulitenga fedha kwa ajili ya kulijenga lile daraja angalau zitoke fedha za kuanzia lile daraja Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuomba tu Waziri kwa sababu sihitaji kulalamika, aiandike barabara hii ili aiwekee fedha angalau ipate fedha za matengenezo kwa mwaka huu wa fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii pia ni ahadi ya Rais kuwekewa lami alipokuwa kwenye kampeni Mheshimiwa Rais alipotembea aliona ametembea umbali mkubwa zaidi sana. Alipofika kule Kabilia akasahau kwamba yuko Magu akasema yuko Kwimba, baada ya pale akasema basi barabara hii tutaijenga kwa kiwango cha lami, naomba ahadi hii nayo iheshimiwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara hii ya Isandula - Ngudu ni barabara muhimu iko kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi tangu 2005, hebu tupeni fedha ili iweze kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo barabara ambazo tuliziomba *Road Board* zipande kutoka Wilaya kwenda Mkoa, bahati nzuri Wizara yako Mheshimiwa Waziri ililetta wataalam wa kuzipitia, zikaonekana hizi zina *qualify*, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri sasa uzipandishe hizi barabara kwa sababu uwezo pekee wa Halmashauri hatuwezi kuzigharamia. Hizi ni barabara ya Kisamba - Sayaka - Salama na Simiyu kule Bariadi ni barabara muhimu sana ya kufungua uchumi. Tunayo barabara ya llungu kuelekea Kwimba mpaka Maswa ni barabara muhimu sana kiuchumi, tunayo barabara ya Kisesa - Kayenze - Illemela inaweza kupunguza pia msongamano wa kuingia Jiji la Mwanza, tonayo barabara

28 APRILI, 2017

ya Nyanguge - Kwimba hizi barabara zote zime-*qualify*, ningetegemea kwamba bajeti hii zingeweza kupatiwa fedha, naomba zipatiwe fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo barabara muhimu inayotoka *Airport* - Ilemela ambayo ikitengenezwa kwa kiwango cha lami mpaka Nyanguge inapunguza msongamano kabisa wa wananchi wote kutoka Musoma kuelekea Mwanza hawatapita Mwanza Mjini watakwenda *airport* itapunguza msongamano. Hebu muiweke vizuri kwa sababu tumeomba kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo barabara ya kilometra 1.2 ya Kisesa – Bujora, barabara hii inapitiwa na viongozi wote wa kitaifa kila mwaka kwa ajili ya kwenda kwenye makumbusho, tumeiomba kama *Road Board* kila mwaka klongozi wa kitaifa lazima apite, naomba na hii iingie ni kilometra 1.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya Rais ya kilometra tano za lami Magu Mjini, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri ulikuja Magu nikakutembeza kwenye barabara zile ukaziona zilivyo, hebu tusaidie kwenye bajeti hii angalau ahadi hii ya kilometra tano za lami ianze ili wananchi waweze kupata huduma inayokubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengi nataka nijikite kwenye taasisi hii ya *marine*. Taasisi hii ya *Marine Services* ina uhakika wa kuingiza kipato kwenye nchi hii, nina uhakika mkijiali inaweza kuchangia uchumi kwenye nchi hii pia shirika hili linaweza kujidesha. Mheshimiwa Waziri hili shirika ni kama limetelekezwa, tunazo meli 15 katika maziwa yetu haya matatu, sekta binafsi wako ambao wana meli kule Ziwa Victoria wanafanya vizuri wana meli na kila mwaka wanaongeza meli, kwa nini *Marine* isihudumiwe? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti iliyopita tulitenga fedha, lakini mpaka leo fedha hizi *Marine* hawajapewa taasisi hii. Ni kama dhahabu ambayo iko ndani

28 APRIL, 2017

hatujaipeleka sokoni, hebu tuisaidie *Marine* ili iweze kuchangia uchumi na iweze kujiendesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya kabisa wapiga kura wetu kule ni wafanyakazi wa taasisi hii mishahara hawalipwi, bima ya afya wamefungiwa, kuna mambo kede wa kede. Ushauri wangu ni kwamba kwa sababu hii ni taasisi ambayo iki-link na bandari; ika-link na reli naamini mizigo yote ambayo inakwenda Uganda inaweza ku-support sana kupata fedha nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunacho kivuko ambacho alikiongelea hapa Mheshimiwa Mabula, Ilemala pale tumeomba kivuko cha Kayanze, Bezi na Ijinga. Wananchi waliloko visiwa vile ni zaidi ya wananchi huku wako 600,000 Bezi lakini na Ijinga wapo zaidi ya 400,000. Kwa hiyo, wakipata kivuko hiki kinatasaidia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ambayo Serikali imefanya, makubwa sana kwa muda mfupi na wala hayawezi kuelezeaka. Na mimi nilikuwa najiuliza sana, Mheshimiwa mmoja alikuwa anasema kwamba kipindi hiki tumepata Rais wa ajabu, nilishindwa kumuelewa, lakini sasa nimeanza kumuelewa kwamba kweli tumepata Rais wa ajabu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kinaitwa *Bombardier* ndege mbili zimekuja, nne bado zinakuja jumla ndege sita, kwa muda mfupi, huyu ni Rais wa ajabu haijawahi kutokea! Kuna kitu kinaitwa *standard gauge* tukitafakari kidogo Waheshimiwa Wabunge hili ni jambo kubwa la kihistoria, nasema huyu ni Rais wa ajabu. Kupambana na ujisadi haijawahi kutokea, kupambana na dawa za kulevyia haijawahi kutokea, kupambana na rushwa haijawahi kutokea, huyu ni Rais wa ajabu lazima, tumpe hongera zake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yote haya yanayofanywa na Serikali kwa miradi yote ya kiuchumi na huduma za kijamii hili ni tendo la huruma, na sisi viongozi tunapaswa kuwa na

28 APRILI, 2017

huruma. Mithali ya pili maandiko matakatifu ambayo siyo ya kwako wewe sura ya 19:17 unasema, amhurumiaye maskini anamkopesha Mungu naYe atamlipa kwa tendo lake jema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa huruma hii ya Mheshimiwa Rais na Serikali yake na Waheshimiwa Mawaziri na watendaji wake wakuu wa Serikali, wanafanya kazi ya huruma wanamkopesha Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Washehimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji wa siku ya leo. Ninayo matangazo machache.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la semina ya kesho tunarudia tena ili msije mkawa mmesahau. Kesho tarehe 29 Aprili, 2017 kutakuwa na semina ya mambo ya UKIMWI kwenye ukumbi huu wa Bunge saa 4.00 asubuhi, mnaombwa kuhudhuria.

Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Pauline Gekul amepoteza simu yake, aina ya *Infinix* anaomba Mbunge ye yeyote aliyeiona maana anasema ameipoteza maeneo ya Bunge, ama kama kuna Mbunge alimpa halafu amesahau.

MAJIBU YA MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, asubuhi leo nillahidi kutoa mwongozo alioomba Mheshimiwa Masoud, Mwongozo huu umeombwa leo tarehe 28 Aprili, 2017 na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim kuhusu kutofautiana kwa majibu ya Naibu Waziri na majibu ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu swali namba 115.

Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi katika Kikao cha Kumi na Nne cha tarehe 28 Aprili, 2017 Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim aliuliza swali la msingi namba 115

kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kuhusu Serikali kuweka mkakati wa kuanzisha meli ya mizigo kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara ili kuinusuru barabara ya Dar es Salaam - Mtwara isiharibike. Swali hilo lilijibiwa na Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Baaada ya majibu ya swali hilo la msingi, Mheshimiwa Masoud aliuliza maswali ya nyongeza mawili ambayo yalijibiwa na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Baada ya kumalizika kwa kipindi cha maswali, Mheshimiwa Masoudi alioomba Mwongozo wa Spika akitumia Kanuni ya 68(7) na Kanuni ya 46(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, katika maelezo yake alidai kuwa majibu ya Naibu Waziri na Majibu ya Waziri wake yanatofautiana, hivyo aliomba kupata ufanuzi kuhusu majibu hayo na lipi kati ya hayo ilikuwa sahihi.

Waheshimiwa Wabunge, nilisema kuwa nitapitia Taarifa Rasmi za Bunge kuangalia majibu hayo yanatofautiana vipi ili niweze kutoa majibu ya mwongozo huo. Baada ya kuzipitia Taarifa Rasmi za Bunge, nimeridhika kuwa majibu ya Naibu Waziri wakati akijibu swali la msingi namba 115 na majibu ya Waziri wakati akijibu swali la nyongeza hayatofautiani kama alivyodai Mheshimiwa Masoud.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake alieleza kuwa Serikali inaendelea kujenga mazingira wezeshi na kuhamasisha sekta binafsi kutumia fursa ya kutoa huduma za usafiri wa majini katika mwambao kwa kutumia meli za kisasa. Aliendelea kueleza, nanukuu; "Hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa kwa lengo la kuchochoe sekta binafsi nchini kufanya uwekezaji katika huduma hii."

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri naye katika majibu yake kwa swali la nyongeza alifafanua kuwa ni muhimu kuwa na usafiri wa baharini na akaeleza kuwa sasa hivi ipo meli ambayo inasafirisha saruji ya Dangote kutoka Mtwara kwenda Zanzibar.

28 APRILI, 2017

Wakati akiomba Mwongozo wa Spika Mheshimiwa Masoud alieleza kuwa Naibu Waziri alijibu kuwa meli hiyo haipo lakini Waziri alijibu kuwa meli hiyo ipo.

Waheshimiwa Wabunge, hata hivyo nilipopitia Taarifa Rasmi za Bunge, hakuna mahali popote ambapo Naibu Waziri alisema kuwa meli hiyo haipo. Ni Mheshimiwa Waziri aliyesema kuwa meli hiyo ipo, hata hivyo hakusema kuwa meli hiyo ni ya kutoka Mtwara kwenda Dar es Salaam, bali alisema inatoka Mtwara kwenda Zanzibar.

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wangu ni kuwa majibu ya Naibu Waziri na majibu wa Waziri yanakamilishana (hayatofautiani). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Waziri alieleza kuwa Serikali imeweka mazingira ya kuchochea sekta binafsi kuwekeza katika utoaji wa huduma za usafiri majini na Mheshimiwa Waziri akakamilisha kwa kutoa majibu ya ziada kuwa ni muhimu kuwa na usafiri wa baharini kulinda barabara zetu, na kwamba kwa sasa kuna meli inayosafirisha saruji ya Dangote kutoka Mtwara kwenda Zanzibar. Hivyo, majibu yaliyotolewa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa swali namba 115 ni sahihi na hayatofautiani.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwongozo wangu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirishi Bunge hadi siku ya Jumanne tarehe 2 Mei, 2017 saa tatu asubuhi.

(*Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 2 Mei, 2017 Saa Tatu Asubuhi*)